# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU


## IMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYA

## IMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA

### IMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED

### IMEPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU


### UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI

Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako hivi sasa ni juhudi ya miaka mingi sana ya watu waliojitolea kuona kazi hii imefanikiwa bila ya kumsahau Marhum Abu Muhammad wa London.

Kama lilivyo jina la Tafsiri ndivyo ilivyo Tafsiri yenyewe ambayo mwanachuoni huyu mahiri kabisa aliyeifafanua ni mtu aliyebobea katika fani zote ambazo mfasiri (Mfafanuzi) anatakiwa awe nazo.

Sheikh Muhammad Jawad Mughniyya ameonesha cheche zake katika vitabu vingi alivyoviandika katika maudhui mbali mbalimbali na hivyo kujipatia wasomaji wengi sana.

Msomi huyu, mwenye fikra huru na anayetetea kile anachokiamini, ni mtu mwenye mawazo mapana na kuyaangalia mambo kwa undani sana, kipaumbele chake ni katika maslahi ya umma huu na amejaribu sana kwenda na wakati.

Sifa kubwa pekee ya mwanachuoni huyu ni kuwa yeye hakujihusisha sana na kung'ang'ania madhehebu fulani tu, labda hii yatokana na wadhifa wake wa ukadhi aliokuwa nao katika nchi ya Lebanon ambayo ina madhehebu mengi, ambapo sula la madhehebu ni nyeti nchini humo, hata hivyo yeye aliweza kuamua matatizo ya watu kwenye ofisi yake kulingana na madhehebu yao pale walipomwendea. Hiyo ilimsaidia sana hata kuweza kutoa kitabu kitwacho Al-Fiqh a'laa madhaahabil-khamsah (Fikhi ya madhehebu matano) yaani ya Hanafi, Maaliki, Shafi, Hambali na Shia (ambacho twataraji kitatoka kwa lugha ya kiswahili hivi karibuni Inshaallah).

Jambo lililotupa msukumo wa kukifasiri kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ni zile faida nyingi atakazozipata msomaji na kujua mambo mengi na ya ajabu yaliyo mapya kwake ambayo si rahisi kuyapata kwa wafasiri wengine. Msomaji atapata faida katika fani za Sayansi, Siasa, Historia, Mashairi, visa vizuri, na Saikolojia miongoni mwa mengine; ndiyo maana msomaji atashangaa kidogo anapoisoma Tafsiri hii atakapoona mwandishi amewataja na kuwanukuu watu kama kina Mfalme Edward, wanasayansi kama kina Enstein, wasanii kama Charlie Champlin (Mchekeshaji maarufu), na wengineo, hali inayoifanya tafsiri hii kuwa ni ya kipekee kabisa.

Mtindo alioutumia mwandishi ni sahali uliokusudiwa watu wa tabaka mbalimbali, wanavyuoni na watu wa kawaida.

Nia yetu ni kukigawanya kitabu hiki bure lakini tumelazimika kukiuza kwa bei nafuu ili kurudisha gharama za uchapishaji.

**Mwisho**: Shukrani kubwa iwaendee bila ya kuwataja watu waliojitolea usiku na mchana, jopo la wafasiri, wahariri, wachapaji, waliotupa moyo na kutoa maoni yao na walioisimamia ili kuhakikisha kwamba kitabu kimemfikia msomaji.

## MAKOSA YA CHAPA

Sikumbuki kama nimewahi kusoma kitabu kilichotoka kupigwa chapa, cha zamani au cha sasa, bila ya kukuta makosa ya chapa. Nafikiri sitasoma kitabu kisichokuwa hivyo. Nimejaribu sana kuliepuka hilo katika tungo zangu, lakini sikufanikiwa.

Nilikuwa sifikirii kama ninaweza kuona makosa haya katika maandishi ya msahafu mtukufu, kama yale yaliyo katika baadhi ya chapa; kwa mfano neno yabswutu kwa swad, badala ya yabsutu kwa sin, na katika chapa ya Tafsir Arrazi ya Misr ya mwaka 1935, Sura ya (2:146). Imeandikwa La Ya'alamuun, (hawajui) badala ya Ya'alamuun (wanajua). Mfano wa makosa haya hausameheki.

Katika Tafsir Al-Manar, chapa ya Pili, sura (5:212), imeandikwa Fawqahum ila yawmil qiyama badala ya Fawqahum yawamal qiyama. Hatuwezi kusema kosa hili ni kubwa zaidi kuliko lile.

Lakini mkosaji atatuletea udhuru kwa msemo mashuhuri huko kwetu Jabal amil 'Makosa ya chapa.'

Katika Tafsiri Majmau chapa ya Urfan, Sura (46:15), imeandikwa: Hatta idha balagha arbai' na sanah badala ya: Hattaidha balagha ashuddahu arbai ' na sanah"

Kusema hivi sio kama ninajitetea kutokana na makosa ya chapa atakayoyakuta msomaji katika kitabu hiki, ijapokuwa naomba msamaha kama litatokea hili, lakini makusudio yangu hasa ni kumwambia yule atakayefungua macho yake kwenye makosa ya matamko na kuufungia macho uzuri wa maana.

Vilevile ninamwambia yule ambaye siku moja aliniambia: "Vitabu vyako vimejaa makosa ya chapa." Kama kwamba hakuna kitu chochote katika vitabu hivyo isipokuwa makosa ya chapa tu. Wote hao ninawaambia: Mungu awasamehe na aniongoze mimi na nyinyi.

Vyovyote iwavyo, mimi ninaomba msamaha kutokana na makosa ya kifikra na ya chapa. Anasema Amirul Muminiin (a.s): **"Watu wote ni wapungufu wenye kuchanganyikiwa, isipokuwa yule aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu."** Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye mwenye jukumu la kunikubalia yale niliyoyapatia na kunisamehe niliyakosea, kwa jaha ya Mtume na kizazi chake, ziwashukie rehema na amani (Amin).

**MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYAH**

1

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

## Mwendelezo Wa Sura Ya Kumi na Mbili: Surat Yusuf

وَمَا أُبَرِّئُ نَفْسِي ۚ إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ بِالسُّوءِ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي ۚ إِنَّ رَبِّي غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٥٣﴾

53. Nami sijitakasi nafsi yangu; hakika nafsi ndiyo iamrishayo mno uovu, isipokuwa ile ambayo Mola wangu ameirehemu. Hakika Mola wangu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

### NAFSI

**Aya 53**

Mwanadamu ni mnyama mwenye akili na dini. Yeye kwa unyama wake au kwa nafsi yake anapondokea sana kwenye matamanio na starehe, hajali akili wala dini. Lakini kwa dini yake na akili yake anaizuia nafsi yake na akili yake isipetuke mipaka ya sharia.

Kwa hiyo mwenye kuiachia nafsi yake ifanye vile itakavyo, basi yeye ni mnyama katika sura ya binadamu, bali ni afadhali mnyama, kwa vile binadamu ana majukumu na ataulizwa, lakini mnyama hana majukumu yoyote. Ndio maana Mwenyez Mungu akasema:

إِنْ هُمْ إِلَّا كَالْأَنْعَامِ ۖ بَلْ هُمْ أَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٤٤﴾

"Hawakuwa wao ila ni kama wanyama, bali wao wamepotea zaidi njia" (25:44).

Ni kweli kwamba wakati mwingine mtu anaweza kuwa dhaifu mbele ya matamanio, lakini muumin mwenye akili anarudi kwenye uongofu wake na kutubia; Mwenyezi Mungu naye humsamehe, kwa sababu ni Mwingi wa Maghufira, Mwenye kurehemu.

Kauli yake Mwenyezi Mungu: "Ispokuwa ile ambayo Mola wangu ameirehemu." Maana yake ni kuwa nafsi yoyote haiwezi kusalimika na kasoro isipokuwa ile aliyoihifadhi Mwenyezi Mungu kutokan na makosa na madhambi (isma) kama nafsi za mitume na maimamu. Muhimu ni kutong'ang'ania mkosaji na kuachana kabisa na Mola wake. Imam Ali (a.s) anasema: **"Dhambi kubwa ni ile ambayo mwenyewe ameipuuza"** yaani ameing'ang'ania na wala asiombe msamaha.

وَقَالَ الْمَلِكُ ائْتُونِي بِهِ أَسْتَخْلِصْهُ لِنَفْسِي ۖ فَلَمَّا كَلَّمَهُ قَالَ إِنَّكَ الْيَوْمَ لَدَيْنَا مَكِينٌ أَمِينٌ ﴿٥٤﴾

54. Akasema mfalme: Mleteni awe wangu mwenyewe. Basi alipozungumza naye alisema: Hakika wewe leo kwetu ni mwenye heshima, mwenye kuaminika.

قَالَ اجْعَلْنِي عَلَىٰ خَزَائِنِ الْأَرْضِ ۖ إِنِّي حَفِيظٌ عَلِيمٌ ﴿٥٥﴾

55. Akasema (Yusuf): Nifanye mweka hazina wa nchi, hakika mimi ni mlinzi, mjuzi.

وَكَذَٰلِكَ مَكَّنَّا لِيُوسُفَ فِي الْأَرْضِ يَتَبَوَّأُ مِنْهَا حَيْثُ يَشَاءُ ۚ نُصِيبُ بِرَحْمَتِنَا مَن نَّشَاءُ ۖ وَلَا نُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٦﴾

56. Na hivyo ndivyo tulivyompa cheo Yusuf katika nchi akae humo popote apendapo. Tunamfikishia rehema zetu tumtakaye, wala hatupotezi ujira wa wafanyao mema.

وَلَأَجْرُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِّلَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿٥٧﴾

57. Na ujira wa akhera ni bora kwa wale walioamini na wakawa wanamcha (Mungu).

## YUSUF NI MUHESHIMIWA MISR

**Aya 54-57**

### MAANA

Akasema mfalme: "Mleteni awe wangu mwenyewe." Basi alipozungumza naye alisema: "Hakika wewe leo kwetu ni mwenye heshima, mwenye kuaminika."

Baada ya mke wa waziri na wale wanawake wengine kukiri na watu wote kujua kuwa Yusuf hana hatia, Yusuf alikubali kutoka gerezani na mfalme alipokutana naye na kumsikiza, alimpenda na akamtaka awe kiongozi katika serikali yake aweze kumsaidia kuendesha serikali, akamwambia: "Wewe ni mwenye heshima na mtu mwenye kuaminiwa kwenye kila kitu katika serikali."

Mfalme hakuyasema haya ila baada ya kuwa na uhakika wa uwezo wake, ujuzi wake na hekima yake. Inasemekana umri wa Yusuf wakati huo ulikuwa ni miaka 30. Katika Majmaul bayan imeelezwa kuwa Yusuf alimsalimia mfalme kwa lugha ya kiarabu.

Mfalme alipomuuliza umeipata wapi lugha hii, alisema ni lugha ya ami yangu Ismail. Katika tafsir Al-manar imeelezwa kwamba mfalme aliyekuweko wakati wa Yusuf alikuwa ni katika wafalme wa kiarabu walio maarufu kwa jina la Hyksos.

Tabari anasema alikuwa akiitwa Walid bin Rayyan.

Akasema (Yusuf): "Nifanye mweka hazina wa nchi, hakika mimi ni mlinzi, mjuzi."

Baada ya mfalme kumwachia Yusuf afanye atakavyo na achague cheo, basi alichagua cheo cha wizara ya hazina na uchumi.

Alichagua cheo baada ya kuhiyarishwa na wala hakuanza yeye, isije ikaonekana kuwa anataka cheo. Hata kama tukisema ameanza yeye, basi itakuwa sio kwa maslahi yake bali ni kwa maslahi ya umma na kulinda haki za wanyonge; hasa kwenye mwaka wa kahati na njaa.

Yusuf alijua kuwa nchi inakabiliwa na janga; ikiwa mweka hazina si mjuzi na asiyekuwa mlinzi imara, basi watu hawatapata haki yao; hasa mafukara na maskini.

Zaidi ya hayo ni kuwa wizara hiyo ni nyeti sana; ikishikwa na watu wasio na ujuzi na uamnifu, umma utaangamia tu; hata ikiwa sio wakati wa shida. Lakini ikiwa mikononi mwa wajuzi na walio na uaminifu, umma utaongoka kidunia na kiakhera.

Wengi wamenukuu kuwa Yusuf aliposhikilia hazina, na watu kuona uamnifu wake na kumpa kila mtu haki yake, waliamini utume wake; hata mfalme pia alishahadia kuwa hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Yusuf ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Ismail Haqqiy, anasema katik Rawhul bayan:

“Amesema Mujahid: Mfalme alisilimu kupitia kwa Yusuf, pamoja na watu wengi.” Mwenye Tafsir al-bayan, aliongezea juu ya kauli hii ya Mujahid kwa kusema: Ikiwa hisani na ukarimu wa Yusuf ni sababu ya imani, basi unaonaje yule aliyemsaidia mtume **(s.a.w.w)** na akamkinga na kumhami muda wa uhai wake. Ambaye ni ami yake, Abu Twalib? Kwa hiyo ukweli hasa, yeye ni katika wale ambao Mwenyezi Mungu amewahuyisha kwa imani, kama ilivyotangulia kuelezwa.”

Yametangulia maelezo ya kusilimu Abu Twalib katika Juz. 11 (9:113).

Hakika mimi ni mlinzi, mjuzi.

Nitailinda mali isipotee bure na kufanyiwa israf, na ninajua wale wanaostahiki kupewa na kila kitu nitakiweka mahali pake panapostahiki.

Imepokewa kutoka kwa Imam Jafar As-Sadiq, amesema: “Inajuzu kwa mtu kujisifu ikibidi kufanya hivyo, kwani Yusuf alisema: “Nifanye mweka hazina wa nchi; hakika mimi ni mlinzi, mjuzi.”

Katika baadhi ya Tafsiri imeelezwa kuwa Yusuf hakuwahi kumnyenyekea Mfalme kwa kumwambia: uishi ewe mfalme! Mimi ni mtumwa wako mnyenyekevu; kama wafanyavyo leo wale wanaojipendekeza kwa wakubwa; isipokuwa alitaka yale ambayo anaamini kuwa anayamudu; kama maandalizi ya kukabiliana na majanga na kulinda nchi kutokana na uharibifu. Laiti wale wanaojipendekeza kwa wakubwa wangelisoma Qur’an wakajua kuwa heshima haiji kwa kujipendekeza

Razi anasema: Yamepokewa masimulizi kuwa Mfalme alimwambia Yusuf: “Napenda kukushirikisha kwenye kila kitu isipokuwa katika watu wangu wa nyumbani na kula na mimi.” Yusuf akamwambia: “Siwezi kula pamoja nawe na mimi ni Yusuf bin Ya’qub bin Is-haq bin Ibrahim kipenzi cha Mungu!”

Na hivyo ndivyo tulivyompa cheo Yusuf katika nchi akae humo popote apendapo. Tunamfikishia rehema zetu tumtakaye, wala hatupotezi ujira wa wafanyao mema.

Yusuf alivumilia kutupwa kisimani, kuuzwa utumwani, kutumikia nyumba ya waziri, kutuhumiwa na kufungwa gerezani. Aliyavumilia yote hayo na mengine kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu na kutosheka naye. Je, natija yake ilikuwa ni nini? Alitoka gerezani kishujaa akiwa ni mshindi wa vita vya uvumilivu; ni mtu huru na akawa mmoja wa viongozi wa nchi. Hivi ndivyo wanavyolipwa wavumilivu ujira wao katika dunia.

Na ujira wa akhera ni bora kwa wale walioamini na wakawa ni wenye kumcha (Mungu).

Malipo ya akhera ni Pepo ambayo “Haikatiki neema yake, haondoki mkazi wake, hazeeki anayedumu, wala kukata tamaaa anayekaa humo” kama alivyosema Imam Ali.

Sasa iko wapi neema hii na ile ambayo mfalme anazeeka kwa taabu na maumivu. Baadhi ya mapokezi yanasema kuwa mke wa mheshimiwa alimjia Yusuf siku za kahati akitafuta chakula, mumewe akiwa amekufa na yeye dunia imemwinamia, yakawa yamempata yaliyompata.

Yusuf alipomuona alimwambia imekuwaje kuwa katika hali hii, naye akasema:

Ametakataka na maovu ambaye anawafanya wafalme kuwa watumwa kwa kwa sababu ya kumwasi na anayewafanya watumwa kuwa wafalme kwa sababu ya kumtii.

وَجَاءَ إِخْوَةُ يُوسُفَ فَدَخَلُوا عَلَيْهِ فَعَرَفَهُمْ وَهُمْ لَهُ مُنكِرُونَ ﴿٥٨﴾

58. Wakaja ndugu zake Yusuf wakaingia kwake. Yeye akawajua na wao hawakumjua.

وَلَمَّا جَهَّزَهُم بِجَهَازِهِمْ قَالَ ائْتُونِي بِأَخٍ لَّكُم مِّنْ أَبِيكُمْ أَلَا تَرَوْنَ أَنِّي أُوفِي الْكَيْلَ وَأَنَا خَيْرُ الْمُنزِلِينَ ﴿٥٩﴾

59. Alipowatengenezea mahitaji yao aliwaambia: "Nileteeni ndugu yenu kwa baba. Je hamuoni kuwa mimi ninatimiza kipimo na kwamba mimi ni mbora wa wakaribishao?

فَإِن لَّمْ تَأْتُونِي بِهِ فَلَا كَيْلَ لَكُمْ عِندِي وَلَا تَقْرَبُونِ ﴿٦٠﴾

60. Msiponiletea basi hampati kipimo chochote kwangu wala msinikurubie.

قَالُوا سَنُرَاوِدُ عَنْهُ أَبَاهُ وَإِنَّا لَفَاعِلُونَ ﴿٦١﴾

61. Wakasema: "Tutamrairai baba yake, na hakika sisi tutafanya."

وَقَالَ لِفِتْيَانِهِ اجْعَلُوا بِضَاعَتَهُمْ فِي رِحَالِهِمْ لَعَلَّهُمْ يَعْرِفُونَهَا إِذَا انقَلَبُوا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٦٢﴾

62. Akawaambia watumishi wake: "Tieni bidhaa zao katika mizigo yao ili wazione watakaporudi kwa watu wao ili wapate kurejea."

## WAKAJA NDUGUZE YUSUF

**Aya 58-62**

### MAANA

Wakaja ndugu zake Yusuf wakaingia kwake, Yeye akawajua na wao hawakumjua.

Kahati ilienea mpaka miji ya jirani, ikiwemo Palestina na Kanani aishipo Nabii wa Mungu, Ya'qub. Ikawa imeenea habari kwamba waziri wa Misr amejiandaa vizuri kuikabili njaa na kwamba yeye anagawanya chakula kwa uadilifu bila ya kumbagua yeyote.

Nyumbani kwa Ya'qub kukawa na shida, kama iliyoko katika majumba mengine, Hivyo akawaamrisha wanawe waende Misr kuhemera chakula.

Basi wakaondoka kuelekea Misr wakiwa ni watu kumi. Walipofika huko waliingia makao ya waziri wakamkuta Yusuf, kwa sababu alikuwa akisimamia kazi yeye mwenyewe, Yusuf akawatambua, lakini wao hawakumatambua.

Alipowatengenezea mahitaji yao

Baada ya kuwaandalia mahitaji yao yote pamoja na yale ya safari, aliwaambia: "Nileteeni ndugu yenu kwa baba."

Wafasiri wanasema kuwa Yusuf aliwakirimu sana ndugu zake mpaka wakawa hawana wasiwasi naye; wakazungumza naye kuhusu maisha yao na ya baba yao na kwamba wao wana ndugu yao mdogo wa baba mmoja, Ndipo Yusuf akawaambia basi nileteeni huyo ndugu yenu mdogo.

Katika Aya hakuna linalofahamisha kuwa walizungumza naye, lakini kuhusu kuwakirimu kunafahamishwa na kauli:

Je hamuoni kuwa mimi ninatimiza kipimo na kwamba mimi ni mbora wa wakaribishao? Msiponiletea basi hampati kipimo chochote kwangu wala msinikurubie

Maana yako wazi, Kwa mnasaba wa Aya hii, wamekongamana mafakihi kwamba inafaa kwa muuzaji na mnunuzi kuweka sharti lolote apendalo katika biashara, maadam haliharamishi halali wala kuahalalisha haramu. Na sharti la Yusuf ni katika aina hii.

Wakasema: Tutamrairai baba yake; na hakika sisi tutafanya.

Wao walikuwa wanajua kuwa baba yao si rahisi kumtoa, ndio maana wakasema kuwa watamrairai; yaani watajitahidi na kumbembeleza baba yao; pamoja na ugumu wa jambo lenyewe.

Akawaambia watumishi wake: “Tieni bidhaa zao katika mizigo yao.

Yusuf aliwaamrisha watumishi wake warudishe vile vitu walivyonunulia chakula kwenye mizigo yao, bila ya wao kutambua.

Ili wazione watakaporudi kwa watu wao wapate kurejea tena kwa kuwa na tamaa ya ukarimu wa Yusuf. Sio mbali kuwa lengo la Yusuf ni kumtuliza baba yake ili asione uzito kumwachia ndugu yake aje kwake.

فَلَمَّا رَجَعُوا إِلَىٰ أَبِيهِمْ قَالُوا يَا أَبَانَا مُنِعَ مِنَّا الْكَيْلُ فَأَرْسِلْ مَعَنَا أَ خَانَا نَكْتَلْ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ
﴿٦٣﴾

63. Basi waliporudi kwa baba yao, walisema: “Ewe baba yetu! Tumenyimwa chakula, basi mtume ndugu yetu pamoja nasi ili tupate kupimiwa na kwa hakika sisi tutamlinda.

قَالَ هَلْ آمَنُكُمْ عَلَيْهِ إِلَّا كَمَا أَمِنتُكُمْ عَلَىٰ أَخِيهِ مِن قَبْلُ فَاللَّـهُ خَيْرٌ حَافِظًا وَهُوَ أَرْحَمُ
الرَّاحِمِينَ ﴿٦٤﴾

64. Akasema: Je nikuaminini kwa huyu kama nilivyokuaminini kwa nduguye zamani? Basi Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa kulinda, na ndiye anayerehemu zaidi kuliko wanaorehemu.

وَلَمَّا فَتَحُوا مَتَاعَهُمْ وَجَدُوا بِضَاعَتَهُمْ رُدَّتْ إِلَيْهِمْ قَالُوا يَا أَبَانَا مَا نَبْغِي هَـٰذِهِ بِضَاعَتُنَا رُدَّتْ
إِلَيْنَا وَنَمِيرُ أَهْلَنَا وَنَحْفَظُ أَخَانَا وَنَزْدَادُ كَيْلَ بَعِيرٍ ذَٰلِكَ كَيْلٌ يَسِيرٌ ﴿٦٥﴾

65. Wailpofungua mizigo yao wakakuta bidhaa zao wamerudishiwa. (Wakasema): Ewe baba yetu! Tutake nini zaidi? Hizi bidhaa zetu tumerudishiwa. Na tutaleta chakula kwa ajili ya watu wetu na tutamlinda ndugu yetu na tutapata ziada ya kipimo cha ngamia mmoja. Hicho ni kipimo kidogo.

قَالَ لَنْ أُرْسِلَهُ مَعَكُمْ حَتَّىٰ تُؤْتُونِ مَوْثِقًا مِّنَ اللَّـهِ لَتَأْتُنَّنِي بِهِ إِلَّا أَن يُحَاطَ بِكُمْ فَلَمَّا آتَوْهُ
مَوْثِقَهُمْ قَالَ اللَّـهُ عَلَىٰ مَا نَقُولُ وَكِيلٌ ﴿٦٦﴾

66. Akasema: Sitampeleka nanyi mpaka mnipe ahadi kwa Mwenyezi Mungu kwamba mtamleta kwangu ila ikiwa mmezungukwa. Basi walipompa ahadi yao, alisema: Mwenyezi Mungu ndiye mtegemewa kwa tuyasemayo.

## MTUME NDUGU YETU PAMOJA NASI

**Aya 63-66**

**MAANA**

Basi waliporudi kwa baba yao, walisema: Ewe baba yetu! Tumenyimwa chakula.

Wakiashiria kauli ya Yusuf Msiponiletea basi hampati kipimo chochote kwangu, Kisha wakamwambia baba yao:

Basi mtume ndugu yetu pamoja nasi ili tupate kupimiwa na kwa hakika sisi tutamlinda.

Walitoa ahadi ya kumlinda na kumhifadhi ili baba yao asiwanyime.

Je nikuaminini kwa huyu kama nilivyokuaminini kwa nduguye zamani? Mlivyomfanyia?

Kisha akaelekea kwa Mwenyezi Mungu na akasema:

Basi Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa kulinda na ndiye anayerehemu zaidi kuliko wanaorehemu.

Mimi namtegemea Mwenyezi Mungu katika uhifadhi na ulinzi wa mwanagu sio hifadhi yenu. Na yeye Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuhurumia unyonge wangu na uzee wangu. Inasemekana kuwa jina la huyo mtoto wake mdogo lilikuwa ni Bin-yamin (Benjamin).

Wailpofungua mizigo yao wakakuta bidhaa zao wamerudishiwa.

Wakamkimbilia baba yao wakiwa na furaha na wakasema:

Ewe baba yetu! Tutake nini zaidi?

Yaani tutatoa sababu gani kwake kama hatukwenda na ndugu yetu na ametukirimu namna hii kama uonavyo ameturudishia mali yetu.

Hizi bidhaa zetu tumerudishiwa.

Inasemekana mali yenyewe ilikuwa ni viatu na ngozi.

Baadhi ya wafasiri wa kisasa wanasema kuwa walikuta mali yao tu, sio chakula na kwamba Yusuf alifanya hivyo ili walazimike kurudi na ndugu yao. Lakini hayo ni makosa kwa sababu yanapingana na dhahiri ya Qur’an amabayo ni: “Je hamuoni kuwa mimi ninatimiza kipimo na kwamba mimi ni mbora wa wakaribishao?”

Zaidi ya hayo kuwanyima ndugu chakula wakati wanakihitajia ni roho mbaya na ngumu sana, jambo ambalo liko mbali sana na Yusuf. Ama kauli yao “Tumenyimwa chakula” ni kunyimwa mara ya pili watakaporudi.

Na tutaleta chakula kwa ajili ya watu wetu na tutamlinda ndugu yetu na kila jambo baya.

Na tutapata ziada ya kipimo cha ngamia mmoja.

Kwa sabbu Yusuf alikuwa akimpa kila mtu kipimo cha ngamia mmoja tu, ili watu wote wapate chakula. Kwa hiyo wakienda na ndugu yao watazidisha mzigo wao.

Hicho ni kipimo kidogo.

Yaani ziada itapatikana kwa kuweko ndugu yetu; vinginevyo, hatupati. Yaqub akaona haja ya chakula imezidi na kile walichokuja nacho kinakaribia kwisha. Hivyo akakubali kwa sababu ya haja si kwa sababu ya shinikizo la wanawe, kuongezea kumwamini waziri kutokana na sifa nzuri alizozisikia na jinsi alivyowafanyia wanawe.

Akasema: Sitampeleka nanyi mpaka mnipe ahadi kwa Mwenyezi Mungu kwamba mtamleta kwangu ila ikiwa mmezungukwa.

Aliwaruhusu kuondoka na Bin-yamin kwa sharti la kutoa ahadi madhubuti kuwa watamrudisha salama isipokuwa wakitokewa na sababu zisizoweza kuzuilika.

Basi walipompa ahadi yao alisema: Mwenyezi Mungu ndiye mtegemewa kwa tuyasemayo.

Yaani walipompa ahadi aliyoitaka, kwamba watamfidia kwa roho zao, alisema Mungu peke yake ndiye shahidi wa haya tuyasemayo. Mkitekeleza, Mungu atawalipa mema na mkihalifu atawalipa adhabu kubwa.

وَقَالَ يَا بَنِيَّ لَا تَدْخُلُوا مِن بَابٍ وَاحِدٍ وَادْخُلُوا مِنْ أَبْوَابٍ مُّتَفَرِّقَةٍ وَمَا أُغْنِي عَنكُم مِّنَ اللَّـهِ
مِن شَيْءٍ إِنِ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّـهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَعَلَيْهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٦٧﴾

67. Akasema: "Enyi wanangu! Msiingie mlango mmoja, bali ingieni kwa milango mbalimbali. Wala mimi siwafai na chochote mbele ya Mwenyezi Mungu; hukumu haiko ila kwa Mwnyezi Mungu tu, juu yake yeye ninategemea na juu yake yeye wategemee wanaotegemea."

وَلَمَّا دَخَلُوا مِنْ حَيْثُ أَمَرَهُمْ أَبُوهُم مَّا كَانَ يُغْنِي عَنْهُم مِّنَ اللَّـهِ مِن شَيْءٍ إِلَّا حَاجَةً فِي نَفْسِ
يَعْقُوبَ قَضَاهَا وَإِنَّهُ لَذُو عِلْمٍ لِّمَا عَلَّمْنَاهُ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٨﴾

68. Walipoingia kama alivyowaamrisha baba yao, haikuwafaa kitu kwa Mwenyezi Mungu; isipokuwa ni haja tu iliyo katika nafsi ya Ya'qub aliitimiza. Na hakika yeye ana elimu kwa tulivyomfundisha, lakini watu wengi hawajui.

## MSIINGIE MLANGO MMOJA

**Aya 67-68**

### MAANA

Akasema: Enyi wanangu! Msiingie mlango mmoja, bali ingieni kwa milango mbalimbali.

Baada ya kusisitiza ahadi yao kwa baba yao, aliwaruhusu kuondoka na ndugu yao mdogo na akawapa wasia huu. Inaonekana kuwa huo mji ulikuwa na milango mingi ya kuingilia, Baadhi ya tafsiri zinasema ilikuwa milango mine.

Wametofautiana wafasiri kuhusu lengo la Ya'qub kwenye wasia huu, Hakuna maelezo ya kutegemewa, Pengine inawezekana kuwa kama wataingia pamoja nao ni genge la watu 11, watu wanaweza kuanza kujiuliza uliza.

Au pengine ni kwa lengo la kuujua mji na kuchunguza habari za Yusuf. Kwa vyovyote iwavyo, sisi hatukalifiwi kutafiti lengo la wasia huo, maadamu Aya haikulidokeza.

Katika tafsir Bahrul Muhit, imeelezwa kuwa Ya'qub aliwatuma wanawe wamplekee salaam waziri kwamba baba yetu anakuombea rehema na anakushukuru ulivyotufanyia. Yusuf aliposikia ujumbe huu alilia. Hayo hayako mbali na maudhui haya.

Wala mimi siwafai na chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Hukumu haiko ila kwa Mwnyezi Mungu tu.

Katika kufasiri Juz.12 (12:40) kifungu 'Hakuna hukumu sipokuwa ya Mwenyezi Mungu' tulibainisha kwamba hukumu yake Mwenyezi Mungu inaweza kuwa ni halali na haramu, inayoitwa hukumu ya sharia.

Vile vile inaweza kuwa ni kadha yake na kadari ambayo haiepukiki. Mfumo wa Aya unafahamisha kuwa hayo ndio makusudio yake hapa. Na maana yake ni kuwa mimi ninawapa nasaha na kuwatakia mema, lakini yote hayo hayawezi kuzuia kadari na hukumu ya Mwenyezi Mungu.

Lengo lake katika hilo ni kuwabainishia wanawe kwamba mtu asitegemee vitendo peke yake wala imani peke yake; bali afanye vitendo na kujitahidi huku akimtegemea Mwenyezi Mungu na kuitakidi kuwa yeye ndiye msaidizi wake. Ndio maana akasema:

Juu yake Yeye ninategemea na juu yake Yeye wategemee wanaotegemea.

Yaani mimi ninamwamini Mwenyezi Mungu na ninamtegemea Yeye na kila anayemwamini mwenyezi Mungu anatakikana kuwa hivyo.

Walipoingia kama alivyowaamrisha baba yao, haikuwafaa kitu kwa Mwenyezi Mungu.

Yaani watoto wa Ya'qub waliingia mjini Misr kwa kupitia milango mbalimbali, kwa kufuata amri ya mzazi wao, lakini hilo halikuwafaa kitu wala kuzuia balaa, kama alivyotangulia kusema baba yao: "Wala mimi siwafai na chochote mbele ya Mwenyezi Mungu" amabapo walituhumiwa wizi na kuchukuliwa Bin-yamin wakarudi kwa baba wakiwa hoi; kama itakavyoelezwa.

Ispokuwa ni haja tu iliyo katika nafsi ya Ya'qub aliitimiza.

Wamatofautiana wafasiri kuhusu haja ya Ya'qub iliyotimizwa na Mwenyezi Mungu. Kuna aliyesema kuwa ni kuwa watoto wa Ya'qub wasipatwe na jicho watakapoingia Misr. Mwingine akasema kuwa ni waziri asiwapate na jambo baya.

Tuanavyo sisi, kulingana na hali ilivyo, na kulingana na Aya inayoonyesha kuhangaika kwa Ya'qub juu ya Yusuf na nduguye, ni kwamba haja ya kwanza na ya mwisho ya Ya'qub, katika maisha haya, ni usalama wa Yusuf na nduguye na kuwa pamoja nao ni kitulizo cha moyo wake. Na mwenyezi Mungu alimtimizia aliyoyataka kwa uzuri.

Na hakika yeye ana elimu kwa tulivyomfundisha.

Yeye ni mtume na kila mtume anafundishwa na kupata elimu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na miongoni mwa mafunzo hayo kwa Ya'qub ni uvumilivu wake wa misukosuko na kumtegemea kwake Mwenyezi Mungu na kuacha kukata tamaa na rehema ya mwenyezi Mungu. Na miongoni mwa elimu yake ni kuwa mambo yote ya waja yako kwa Mwenyezi Mungu.

Lakini watu wengi hawajui kwamba hukumu ni ya Mwenyezi Mungu na kwamba mipango yote ya waja bila ya msaada wa Mwenyezi Mungu haina manufaa yoyote.

2

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

وَلَمَّا دَخَلُوا عَلَىٰ يُوسُفَ آوَىٰ إِلَيْهِ أَخَاهُ ۖ قَالَ إِنِّي أَنَا أَخُوكَ فَلَا تَبْتَئِسْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٦٩﴾

69. Walipoingia kwa Yusuf alimkumbatia ndugu yake akasema: Hakika mimi ni nduguyo, Basi usihuzunike kwa waliyokuwa wakiyafanya.

فَلَمَّا جَهَّزَهُم بِجَهَازِهِمْ جَعَلَ السِّقَايَةَ فِي رَحْلِ أَخِيهِ ثُمَّ أَذَّنَ مُؤَذِّنٌ أَيَّتُهَا الْعِيرُ إِنَّكُمْ لَسَارِقُونَ ﴿٧٠﴾

70. Alipokwisha watengenezea mahitaji yao akaweka kopo katika mzigo wa ndugu yake. Kisha mnadi akanadi: “Enyi wasafiri! Hakika nyinyi ni wezi.”

قَالُوا وَأَقْبَلُوا عَلَيْهِم مَّاذَا تَفْقِدُونَ ﴿٧١﴾

71. Wakasema na hali wamewaelekea: “Mmepoteza nini?”

قَالُوا نَفْقِدُ صُوَاعَ الْمَلِكِ وَلِمَن جَاءَ بِهِ حِمْلُ بَعِيرٍ وَأَنَا بِهِ زَعِيمٌ ﴿٧٢﴾

72. Wakasema: “Tumepoteza kopo la mfalme na atakayelileta atapata shehena nzima ya ngamia na mimi ni mdhamini.

قَالُوا تَاللَّهِ لَقَدْ عَلِمْتُم مَّا جِئْنَا لِنُفْسِدَ فِي الْأَرْضِ وَمَا كُنَّا سَارِقِينَ ﴿٧٣﴾

73. Wakasema: “Wallahi mnajua vyema kwamba sisi hatukuja kufanya ufisadi katika nchi hii wala sisi si wezi.”

قَالُوا فَمَا جَزَاؤُهُ إِن كُنتُمْ كَاذِبِينَ ﴿٧٤﴾

74. Wakasema: “Malipo yake yatakuwa ni nini ikiwa nyinyi ni waongo?”

قَالُوا جَزَاؤُهُ مَن وُجِدَ فِي رَحْلِهِ فَهُوَ جَزَاؤُهُ ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٧٥﴾

75. Wakasema: “Malipo yake ni yule ambaye litaonekana katika mzigo wake, basi huyo ndiye malipo yake, Hivyo ndivyo tunavyowalipa madhalimu.”

فَبَدَأَ بِأَوْعِيَتِهِمْ قَبْلَ وِعَاءِ أَخِيهِ ثُمَّ اسْتَخْرَجَهَا مِن وِعَاءِ أَخِيهِ ۚ كَذَٰلِكَ كِدْنَا لِيُوسُفَ ۖ مَا كَانَ لِيَأْخُذَ أَخَاهُ فِي دِينِ الْمَلِكِ إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ ۚ نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مَّن نَّشَاءُ ۗ وَفَوْقَ كُلِّ ذِي عِلْمٍ عَلِيمٌ ﴿٧٦﴾

76. Basi akaanza na mizigo yao kabla ya mzigo wa ndugu yake; kisha akalitoa katika mzigo wa ndugu yake, Hivyo ndivyo tulivyomfanyia hila Yusuf hakuweza kumchukua ndugu yake katika sharia ya mfalme, isipokuwa alivyotaka Mwenyezi Mungu, Tunawatukuza kwenye vyeo tuwatakao, Na juu ya kila mwenye elimu yuko ajuaye zaidi.

## MIMI NI NDUGUYO, USIHUZUNIKE

**Aya 69-76**

**Maana**

Walipoingia kwa Yusuf, alimkumbatia ndugu yake akasema: “Hakika mimi ni nduguyo, Basi usihuzunike kwa waliyokuwa wakiyafanya.”

Watu wa tafsiri akiwemo Tabari, Razi, Tabrasi na Abu Hayani al-andalusi, wametaja ufafanuzi wa Aya hii ambao hauna dalili katika

Qur'an, lakini unaoana nayo na kunasibiana nayo. Kwa ajili hii tutafupiliza kauli zao, kama ifuatavyo:

Ndugu wa Yusuf walipofika Misr aliwaalika kwenye chakula na akawaweka wawili wawili, kwa lengo la kuwa yeye abakie na ndugu yake Bin-yamin akae naye kwenye meza yake ya chakula; sawa na alivyofanya Muhammad **(s.a.w.w)** baina ya maswahaba zake wawili wawili kuwa ndugu na akambakisha Ali awe wake yeye.

Baada ya chakula, Yusuf aliwapangia vyumba vya kulala wawili wawili na ndugu yake Bin-yamini akalala naye chumba kimoja. Walipokuwa peke yao akamwambia: "Je, unapenda mimi niwe ndugu yako?" Akamjibu ni nani anaweza kuwa na ndugu mfano wako? Lakini wewe hukuzaliwa na Ya'qub wala Rahel. Basi akamkumbatia na kumwambia: "Mimi nimezaliwa na Ya'qub na Rahel. Basi mimi ni ndugu yako, Wala usuhuzunike na waliyotufanyia ndugu zetu." Bin-Yamin akafurahi sana na akamshukuru Mwenyezi Mungu.

Alipokwisha watengenezea mahitaji yao akaweka kopo katika mzigo wa ndugu yake. Kisha mnadi akanadi: Enyi wasafiri! Hakika nyinyi ni wezi.

Yusuf alitaka kumtenga Bin-yamin na ndugu zake na kubaki naye, lakini hakuwa na njia ila kufanya ujanja. Katika sharia ya watu wa Ya'qub ni mwizi kufanywa mtumwa. Ndio watumishi wakaweka chombo cha kupimia kwenye mzigo wa Bin-yamin, kwa amri ya Yusuf. Akanadi mnadi kuwa nyinyi wana wa Ya'qub! Ni wezi, kwa hiyo msiendelee na msafara hadi tuangalie mambo yenu.

Wakashangaa watoto wa Ya'qub kwa mshtukizo huu.

Wakasema na hali wamewaelekea: Mmepoteza nini?

Walisema hivi wakiwa na yakini kuwa hawana hatia yoyote. Na hii ni mara yao ya kwanza kusikia tuhuma hii.

Wakasema watumishi wa Yusuf:

Tumepoteza kopo la mfalme na atakayelileta atapata shehena nzima ya ngamia na mimi ni mdhamini.

Mdhamini huyu ndiye aliyewaambia nyinyi ni wezi, kama walivyosema wafasiri, na akadhamini kwa sharti ya kuwa mtu aliye na hicho chombo akirudishe yeye mwenyewe.

Aya hii inaingia kwenye milango miwili ya Fiqh: Jaala, ambayo ni kutangaza zawadi kwa atakayeleta kilichopotea na Dhamana ambayo ni kutekeleza ahadi; kama vile kauli ya alisema: 'Na mimi ni mdhamini.' Yaani nadhamini kutekeleza ahadi ya shehena ya ngamia, Kuna hadithi isemayo: "Mdhamini ni mwenye kugharimika."

Wakasema watoto wa Ya'qub: Wallahi mnajua vyema kwamba sisi hatukuja kufanya ufisadi katika nchi hii wala sisi sio wezi.

Walibishana wakajadiliana na kuleta hoja za kutokuwa na hatia na usafi wao; miongoni mwa waliyoyasema ni: Vipi mnatutuhumu na mnajua nasabu yetu na sera yetu katika safari yetu ya kwanza na hii ya pili kwamba hatukuja kufanya ufisadi au hiyana; isipokuwa tumekuja kuwanunulia chakula watu wetu.

Kwenye tafsiri nyingi imeelezwa kuwa watoto wa Ya'qub, kwenye safari yao ya kwanza, walipokuta bidha zao zimerudishwa walidhani kuwa

zimesahaulika, kwa hiyo hawakuzitumia, bali walizirudisha Misr. Kwa hiyo wakawa mashuhuri kwa wema na uamnifu wao.

Kauli hii ya wafasiri haiku mbali; bali inaashiria kauli ya watoto wa Ya'qub: Wallah mnajua vyema kwamba sisi hatukuja kufanya uharibifu katika nchi hii

**Unaweza kuuliza**: Imekuwaje kwa Yusuf kufanya njama hizi za kuwaelekezea tuhuma ndugu zake na hali anajua kuwa hawana hatia?

**Jibu**: Kwanza, tukio hili ni maalum, lina sababu zake, haifai kulipima na matukio mengine. Pili, aliyelengwa na tuhuma za wizi ni Bin-yamin, ndugu wa Yusuf kwa baba na mama, na hilo lilikuwa kwa makubaliano yao na kuridhika kwake, kwa hekima iliyotaka hivyo; wakati huohuo hilo halipingi msingi wowote katika misingi ya sharia; kama vile kuhalalisha haramu au kuharamisha halali.

Zaidi ya hayo, tendo la watoto wa Ya'qub la kumtoa Yusuf kwa baba yake na kumtupa kisimani kwa lengo la kumuua ni zaidi ya wizi.

**Swali la pili**: Vipi Yusuf kumtenganisha nduguye na baba yake na kumzidishia baba yake majonzi juu ya majonzi?

**Jibu**: Kila alilolifanya Yusuf lilikuwa kwa maslahi ya ndugu yake na baba yake; akiwa na uhakika kuwa baba yake atamkubalia na hata kumshukuru atakapojua uhakika wake. Na lilifanyika hilo. Kimsingi ni kuwa mambo hupimwa kwa matokeo yake sio kwa mfumo wake. Katika hali nyingine mitume hawatuhumiwi katika upande wa haki.

Wakasema: "Malipo yake yatakuwa ni nini ikiwa nyinyi ni waongo?"

Watumishi waliwaambia watoto wa Ya'qub ili waseme wenyewe kwamba mwizi atachukuliwa mateka au mtumwa, kama malipo ya tendo lake hilo. Ili iwe ni hoja juu yao pale Yusuf atakapomchukua ndugu yake.

Wakasema: "Malipo yake ni yule ambaye litaonekana katika mzigo wake, basi huyo ndiye malipo yake, Hivyo ndivyo tunavyowalipa madhalimu.

Kusema 'basi huyo ndiye malipo yake' ni kuzidisha ufafanuzi; sawa na kusema: malipo ya muuaji ni kuuliwa, hayo ndiyo malipo yake.

Ndugu wa Yusuf walisema hiyo ndiyo sharia yetu, ambaye mtamkuta nalo mtamchukua mtumwa au mateka. Walisema hivyo wakiwa na uhakika kuwa wao hawana hatia

Basi akaanza na mizigo yao kabla ya mzigo wa ndugu yake; kisha akalitoa katika mzigo wa ndugu yake.

Mtafutaji alianza na mizigo yao kabla ya ndugu yao madogo, ili kuificha hila. Mpaka alipoishia kwenye mzigo wa Bin-yamin akalitoa na akawaonyesha; wakapigwa na butwa na wakawa na wakati mgumu, lakini ni wapi haya na waliyomfanyia Yusuf katika giza la shimo akiwa peke yake?

Hivyo ndivyo tulivyomfanyia hila Yusuf.

Yaani tulimpa wahyi wa mpango huu, ili ndugu zake waseme wenyewe, kuwa waziri amchukue nyara au mtumwa. Imeitwa hila kwa sababu dhahiri yake sio hali halisi; na ilijuzu kisharia, kwa sababu haikuhalalisha haramu wala kuharamisha halali.

Hakuweza kumchukua ndugu yake katika sharia ya mfalme.

Yaani sharia na hukumu ya mfalme. Maana ni kuwa lau si mipango hii ingelikuwa uzito kwa Yusuf kumchukua ndugu yake, kwa sababu sharia ya

mfalme wa Misr sio kuchukua mateka, bali ni kumfunga au kupigwa, na Yusuf hakutaka kumdhuru ndugu yake. Hayo ndio makusudio ya kauli yake:

Isipokuwa alivyotaka Mwenyezi Mungu.

Kwa ufupi ni kuwa hekima ilikuwa ni kutosema Yusuf kuwa yule ni ndugu yake na wakati huo huo asipatwe na sharia ya mfalme ya kufungwa au kupigwa; bali apatwe na hukumu ya watu wa Ya'qub.

Tunawatukuza kwenye vyeo tuwatakao Kwa elimu na utume kama tulivyomfanyia Yusuf juu ya ndugu zake.

Na juu ya kila mwenye elimu yuko ajuaye zaidi mpaka ishie kwa aliye juu zaidi.

Hiyo ni ishara kuwa ndugu wa Yusuf walikuwa ni maulama, lakini Yusuf alikuwa na elimu zaidi na mkamilifu zaidi.

قَالُوا إِن يَسْرِقْ فَقَدْ سَرَقَ أَخٌ لَّهُ مِن قَبْلُ ۚ فَأَسَرَّهَا يُوسُفُ فِي نَفْسِهِ وَلَمْ يُبْدِهَا لَهُمْ ۚ قَالَ أَنتُمْ شَرٌّ مَّكَانًا ۖ وَاللَّـهُ أَعْلَمُ بِمَا تَصِفُونَ ﴿٧٧﴾

77. Wakasema: Kama ameiba, basi ndugu yake pia ameiba zamani." Yusuf aliyaweka siri moyoni mwake wala hakuwadhihirishia; akasema: "Nyinyi mko katika hali mbaya zaidi; na Mwenyezi Mungu anajua zaidi mnayoyasema.

قَالُوا يَا أَيُّهَا الْعَزِيزُ إِنَّ لَهُ أَبًا شَيْخًا كَبِيرًا فَخُذْ أَحَدَنَا مَكَانَهُ ۖ إِنَّا نَرَاكَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٧٨﴾

78. Wakasema: "Ewe mheshimiwa! Hakika anaye baba mzee sana, Kwa hiyo mchukue mmoja wetu badala yake, Hakika sisi tunakuona wewe ni katika watu wema.

قَالَ مَعَاذَ اللَّـهِ أَن نَّأْخُذَ إِلَّا مَن وَجَدْنَا مَتَاعَنَا عِندَهُ إِنَّا إِذًا لَّظَالِمُونَ ﴿٧٩﴾

79. Akasema: "Mwenyezi Mungu apishe mbali kumchukua ila yule tuliyekuta mali yetu iko kwake, Hivyo basi tutakuwa ni wenye kudhulumu."

فَلَمَّا اسْتَيْأَسُوا مِنْهُ خَلَصُوا نَجِيًّا ۖ قَالَ كَبِيرُهُمْ أَلَمْ تَعْلَمُوا أَنَّ أَبَاكُم قَدْ أَخَذَ عَلَيْكُم مَّوْثِقًا مِّنَ اللَّـهِ وَمِن قَبْلُ مَا فَرَّطتُمْ فِي يُوسُفَ ۖ فَلَنْ أَبْرَحَ الْأَرْضَ حَتَّىٰ يَأْذَنَ لِي أَبِي أَوْ يَحْكُمَ اللَّـهُ لِي ۖ وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ ﴿٨٠﴾

80. Walipokata tamaa naye walikwenda kando kunong'ona. Akasema mkubwa wao: "Je, hamjui kuwa baba yenu amechukua ahadi kwenu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Na hapo zamani mlikosea katika Yusuf? Basi sitaondoka nchi hii mpaka baba yangu aniruhusu au Mwenyezi Mungu anihukumie; naye ni mbora wa mahakimu.

## KAMA AMEIBA BASI NDUGUYE PIA ALIIBA ZAMANI

**Aya 77-80**

### MAANA

Wakasema: Kama ameiba, basi ndugu yake pia ameiba zamani.

Ndugu zake Yusuf ndio waliosema hivyo, wakimkusudia Bin-yamin na Yusuf. Hizo ni tuhuma walizombadika nazo Yusuf. Hakuna ishara yoyote katika Aya yoyote kwamba Yusuf kuanzia utotoni aliwahi kuiba yai au kuku au kuiba sanamu ya babu yake mzaa mama yake, au mkanda wa shangazi yake n.k.

Lakini Qur'an imesajili waziwazi uwongo wa ndugu zake Yusuf, pale waliposema kuwa ameliwa na mbwa mwitu. Kuongezea hasadi na chuki yao iliyowapelekea kufanya waliyoyafanya. Kwa hiyo basi wao ni waongo katika kumnasibishia kwao Yusuf wizi alipokuwa mtoto.

Kusema hivi, ingawaje ni natija ya uchambuzi, lakini ndio mantiki ya sawa, au angalau ndio kauli ya karibu na maana.

Wafasiri wameichukulia kauli ya nduguze Yusuf kuwa ni ya kweli, kama kwamba uwongo unastahili. Wakawa wanafanya utafiti wa hicho alichokiiba Yusuf. Kuna aliyesema kuwa aliiba yai akampa mwenye njaa; mweingine akasema ni kuku.

Wa tatu akasema aliiba sanamu la babu yake mzaa mama yake na akalivunja. Wa nne akasema kuwa alikuwa akilelewa na shangazi yake, bint wa Is-haq, alipokuwa na baba yake, akataka kumchukua, kwa hiyo akamtuhumu kuiba mkanda wa mume wa shangazi yake ili abaki naye kama mtumwa; kwa vile adhabu ya mwizi ilikuwa ni kufanywa mtumwa.

Wafasiri wengi wako juu ya kauli hii ya mwisho, Lakini jambo la ajabu ni kuwa hakuna hata mmoja wao aliyezinduka kuwa hukumu ya watoto sio ya wakubwa katika sharia zote, Ajabu zaidi ni kauli ya baadhi ya Masufi kwamba ndugu zake Yusuf walimtuhumu na wizi wa kuiba roho ya baba yake!

Yusuf aliyaweka siri moyoni mwake wala hakuwadhihirishia.

Aliapuuza maneno yao kwa upole na ukarimu; kama asemavyo mshairi: Nampitia mlaumu akinitusi Namsamehe nasema hanihusi

Akasema: Nyinyi mko katika hali mbaya zaidi.

Haya aliyasema kisirisiri, kwa dalili ya kauli yake: "Wala hakuwadhihirishia."

Na Mwenyezi Mungu anajua zaidi mnayoyasema ya kuninasibishia wizi mimi na ndugu yangu, kwamba ni uwongo na uzushi.

Wakasema: Ewe mheshimiwa! Hakika anaye baba mzee sana, Kwa hiyo mchukue mmoja wetu badala yake, Hakika sisi tunakuona wewe ni katika watu wema.

Baada ya mambo kudhihirika na kwamba hukumu ni kuchukuliwa mtumwa ndugu yao Bin-yamin, walielekea kutaka kuhurumiwa kwa kusamehewa au kuchukuliwa fidia ya mmoja wao badala yake. Walibembeleza sana kwa kutumia wema wa Yusuf na uzee wa baba yao na cheo chake na jinsi anavyompenda sana mwanawe Bin-yamin.

Walifanya hivyo sio kwa kumpenda ndugu yao, bali ni kujitoa kwenye lawama kutokana na ahadi waliyoichukua kwa baba yao.

Akasema: Mwenyezi Mungu apishe mbali kumchukua ila yule tuliyekuta mali yetu iko kwake, Hivyo basi tutakuwa ni wenye kudhulumu.

Yusuf alikataa ombi lao na matarajio yao na akashikilia kumchukua ndugu yake, kwa jambo ambalo Mwenyezi Mungu alitaka kulitimiza baada ya kupita mtihani na balaa.

Yusuf alitumia ibara ya ndani sana na yenye hekima ya kumwepusha ndugu yake na wizi, alposema: Yule tuliyekuta mali yetu iko kwake, ambapo ndugu zake walifahamu: 'aliyeiba mali yetu.' Na tofauti hapo ni kubwa sana.

Walipokata tamaa naye walikwenda kando kunong'ona.

Baada ya kukata tamaa watoto wa Ya'qub ya kumpata ndugu yao walijitenga ili washauriane jinsi watakavyomwambia baba yao.

Akasema mkubwa wao: Je, hamjui kuwa baba yenu amechukua ahadi kwenu kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Baadhi ya wafasiri wanasema kuwa makusudio ya mkubwa wao ni mkubwa kiakili si kimiaka. Wengine wakasema ni kiakili na kimiaka.

Kauli hii ndiyo inayokuja haraka akilini, Vyovyote iwavyo ni kwamba mkubwa huyo aliwaambia ndugu zake mtafanyaje mtakapofika kwa baba yenu bila ya Bin-yamin nanyi mliapa kuwa mtamrudisha?

Na hapo zamani mlikosea katika Yusuf?

Anaashiria walivyomtupa shimoni na baba yao alivyokuwa mkali.

Basi sitaondoka nchi hii mpaka baba yangu aniruhusu au Mwenyezi Mungu anihukumie; naye ni mbora wa mahakimu.

Mkubwa wao aliamua abakie karibu na ndugu yake kwa kumwonea haya baba yake na kwamba hataondoka kwenye nchi aliyo Bin-yamin mpaka apewe idhini na baba yake au apate faraja yoyote, kutoka kwa Mwenyezi Mungui hata kama ni mauti. Muda haukuwa mrefu ikaja faraja kwa wote; kama yatakavyokuja maelezo.

ارْجِعُوا إِلَىٰ أَبِيكُمْ فَقُولُوا يَا أَبَانَا إِنَّ ابْنَكَ سَرَقَ وَمَا شَهِدْنَا إِلَّا بِمَا عَلِمْنَا وَمَا كُنَّا لِلْغَيْبِ حَافِظِينَ ﴿٨١﴾

81. Rudini kwa baba yenu, na mwambieni: Ewe baba yetu! Hakika mwanao ameiba, na hatutoi ushahidi ila tunayoyajua; wala hatukuwa wenye kuhifadhi mambo ya ghaibuu.

وَاسْأَلِ الْقَرْيَةَ الَّتِي كُنَّا فِيهَا وَالْعِيرَ الَّتِي أَقْبَلْنَا فِيهَا ۖ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿٨٢﴾

82. Na waulize watu wa mji tuliokuwako na msafara tuliokuja nao, Na hakika sisi tunasema kweli.

قَالَ بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنفُسُكُمْ أَمْرًا ۖ فَصَبْرٌ جَمِيلٌ ۖ عَسَى اللَّـهُ أَن يَأْتِيَنِي بِهِمْ جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٨٣﴾

83. Akasema: "Bali nafsi zenu zimewashawishi jambo fulani. Basi subira ni njema. Huenda Mwenyezi Mungu akaniletea wote pamoja, Hakika Yeye ni Mjuzi, Mwenye hekima.

وَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَا أَسَفَىٰ عَلَىٰ يُوسُفَ وَابْيَضَّتْ عَيْنَاهُ مِنَ الْحُزْنِ فَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٨٤﴾

84. Na akajitenga nao, na akasema: Oh! Masikitiko yangu juu ya Yusuf! Na macho yake yakawa meupe kwa huzuni naye akawa anaizuia.

قَالُوا تَاللَّـهِ تَفْتَأُ تَذْكُرُ يُوسُفَ حَتَّىٰ تَكُونَ حَرَضًا أَوْ تَكُونَ مِنَ الْهَالِكِينَ ﴿٨٥﴾

85. Wakasema: "Wallahi huachi kumkumbuka Yusuf mpaka uwe mgonjwa au uwe katika wenye kuaangamia."

قَالَ إِنَّمَا أَشْكُو بَثِّي وَحُزْنِي إِلَى اللَّـهِ وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّـهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨٦﴾

86. Akasema: "Majonzi yangu na huzuni yangu ninamshtakia Mwenyezi Mungu Na ninajua kwa Mwenyezi yale msiyoyajua.

يَا بَنِيَّ اذْهَبُوا فَتَحَسَّسُوا مِن يُوسُفَ وَأَخِيهِ وَلَا تَيْأَسُوا مِن رَّوْحِ اللَّـهِ ۖ إِنَّهُ لَا يَيْأَسُ مِن رَّوْحِ اللَّـهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْكَافِرُونَ ﴿٨٧﴾

87. Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye wala msikate tamaaa na faraja ya Mwenyezi Mungu. Hakika hawakati tamaa na faraja ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri.

## HATUTOI USHAHIDI ILA TUNAYOYAJUA

**Aya 81-87**

### MAANA

Rudini kwa baba yenu, na mwambieni: Ewe baba yetu! Hakika mwanao ameiba na hatutoi ushahidi ila tunayoyajua; wala hatukuwa wenye kuhifadhi mambo ya ghaibu.

Hii ni kauli ya mkubwa wao akiwausia ndugu zake kuwa waseme ukweli kwa baba yao. Wampe habari kuwa wamewaona watumishi wa waziri wakitoa chombo cha kupimia cha mfalme katika mzigo wa Binyamin, Na kwamba waziri aling'ang'ania kumchukua, Hayo ndiyo tuliyoyashuhudia.

Na Mwenyezi Mungu anajua yaliyo nyuma ya hayo, Na lau tungelijua ghaibuu, basi tusingemchukua wala kukupa ahadi ya kurudi naye, Tumefanya bidii sana. Tunaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na kwako.

Na waulize watu wa mji tuliokuwako.

Yaani waulize watu wa Misr, jambo hili la wizi limeenea kwao.

Na msafara tuliokuja nao.

Yaani vile vile uliza msafara tuliokuja nao kutoka Misr ambao uko jirani yako katika nchi ya Kanaan.

Na hakika sisi tunasema kweli kwa haya tunayokusimulia. Mara hii walikuwa wakisema kwa kujiamini kwa sababu walikuwa na uhakika wa wanayoyasema kinyume na mara ya kwanza walipokuja na damu ya uwongo kwenye kanzu ya Yusuf.

Akasema: Bali nafsi zenu zimewashawishi jambo fulani.

Walipomweleza baba yao aliwaambia mmefanyia vitimbi kama mlivyomfanyia ndugu yake, Yusuf.

Wafasiri wamejiuliza kuwa vipi Ya'qub aliwatuhumu wanawe kwa vitimbi kabla ya kuthibitisha na yeye ni mtume ma'asum?

Kisha wakajbu kwa njia nyingi zisizotegemea msingi wowote. Njia nzuri zaidi waliyoitaja ni ile kuwa makusudio ya Ya'qub ni kuwa nafsi zenu zimewapa picha ya kuwa Bin-yamin ni mwizi na hali yeye si mwizi.

Tuonavyo sisi ni kuwa Ya'qub aliwatuhumu na vitimbi kwa kuchukulia walivyomfanyia Yusuf, lakini yeye hakuchukulia moja kwa moja, kwa kukosa dalili ya uwongo wao. Vile vile hakuwachukulia hatua yoyote kwa dhana, Kwa sababu dhana haitoshelezi kitu.

Hiyo haipingani na cheo cha utume. Kwa sababu mtume hajui ghaibu, naye ni kama mtu mwingine anadhania na kuchukulia uwezekano. Tofauti ni kuwa kwake yeye dhana haina athari yoyote, kama afanyavyo asiyekuwa ma'sum.

Subira ni njema.

Yaani 'subira yavuta heri, Haya aliwahi kuyasema zamani alipopotea Yusuf na sasa anayasema kwa Bin-yamin.

Huenda Mwenyezi Mungu akaniletea wote pamoja.

Yaani Yusuf, Bin-yamin na kaka yao aliyebakia Misr karibu na ndugu yake. Neno 'huenda' ni mwangaza wa matumaini; hasa likiwa linatoka kwa anayeamini ghaibu kikwelikweli; kama mitume na wasadikishao. Katika Nahjulbalagha imeelezwa: "Haiwi kweli imani ya mja mpaka yawe yaliyo kwa Mwenyezi Mungu ni ya kutegemewa zaidi kuliko yaliyo mikononi mwake" Kuna Hadith nyingi zenye maana haya.

Hakika yeye ni Mjuzi Mwenye hekima.

Anajua huzuni yangu na machungu yangu na anapanga mambo kwa hekima yake.

Na akajitenga nao, na akasema: Oh! Masikitiko yangu juu ya Yusuf!

Alijitenga na watu ili aomboleze peke yake, ambapo huzuni na kilio kilizidi kwa kumkosa mwanawe, Bin-yamin (Benjamin) na macho yake yakawa meupe kwa huzuni.

Yaliathirika kwa sababu ya kulia.

Naye akawa anaizuia.

Yaani anameza uchungu kwa mwili na mishipa yake.

Wakasema: Wallahi huachi kumkumbuka Yusuf mpaka uwe mgonjwa au uwe katika wenye kuaangamia.

Yaani wanawe walimwambia bado unamkumbuka Yusuf mpaka uwe mgonjwa au ufe bure, kwa sababu Yusuf amekwenda harudi tena.

Akasema: Majonzi yangu na huzuni yangu ninamshtakia Mwenyezi Mungu, sio kwenu kwa sababu ni udhalili na usafihi kumshtakia ambaye haondoi dhara. Imam Ali (a.s) anasema: **"Allah Allah! Na kumshatakia ambaye hawezi kuondoa mashaka yenu, wala hawezi kupunguza kwa rai yake yale mliyokwishayapitisha"**

Na ninajua kwa Mwenyezi yale msiyoyajua.

Yaa'qub ameteseka kwa kumkosa Yusuf, lakini wakati huo huo bado anamtegemea Mwenyezi Mungu na kumwekea dhana nzuri wala hakati tamaaa na rehema yake huku akiamini kuwa mwisho wa subra ni faraja (baada ya dhiki faraja); kama ilivyofahamisha kauli yake kuwaambia wanawe "Wala msikate tamaa na faraja ya Mwenyezi Mungu."

Tukiunganisha kumtegemea kwake Mwenyezi Mungu katika ndoto ya Yusuf udogoni mwake natija ni kuwa Yaa'qub ana matumaini ya uhai wa Yusuf hadi atakapokuwa mkubwa, lakini hajui yuko wapi na ana hali gani, Yuko utumwani au kwenye uhuru, Huo ndio ulikuwa wasiwasi wake.

## HAKUNA KUNGOJA MEMA YAJE YENYEWE WALA MABAYA

Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye wala msikate tamaaa na faraja ya Mwenyezi Mungu. Hakika hawakati tamaa na faraja ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri.

Nendeni mkatafute wala msikate tama, Amekutanisha matumaini na kutenda. Maana yake ni kuwa. Ikiwa hakutakuwa na matendo basi Aya itakwenda kinyume; na uvivu utaambatana na kukata tamaa na yatakuwa matarajio bila ya kufanya kitu ni ujinga na upumbavu. Neno tafuteni linawajibisha kutenda kwa hisia zote dhahiri na batini.

Ndivyo alivyo mwenye akili akitokewa na janga lolote anajitahidi kuondoa visababishi vyake, ni sawa viwe ni ufisadi au uzembe.

Na anapopatwa na mazuri huhofia asijisahau akapetuka mpaka kwa utajiri au cheo kikamletea kiburi. Kwa hiyo hujikinga kwa takua:

فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ اللَّـهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٩٩﴾

"Hawaaminishi hila ya Mwenyezi Mungu ila watu wenye hasara." Juz. 9 (7:99).

Kwa ufupi ni kuwa mwenye kutaraji mabaya ni yule asemaye hakuna faida ya kujisumbua, na mvivu ni yule mwenye kutaraji mazuri yaje yenyewe.

3

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَيْهِ قَالُوا يَا أَيُّهَا الْعَزِيزُ مَسَّنَا وَأَهْلَنَا الضُّرُّ وَجِئْنَا بِبِضَاعَةٍ مُّزْجَاةٍ فَأَوْفِ لَنَا الْكَيْلَ
وَتَصَدَّقْ عَلَيْنَا إِنَّ اللَّـهَ يَجْزِي الْمُتَصَدِّقِينَ ﴿٨٨﴾

88. Basi walipoingia kwa Yusuf walisema: “Ewe mheshimiwa! Imetupata shida sisi na watu wetu na tumeleta mali kidogo, basi tupimie kipimo na fanya kama unatupa sadaka; hakika Mwenyezi Mungu huwalipa wanaotoa sadaka.”

قَالَ هَلْ عَلِمْتُم مَّا فَعَلْتُم بِيُوسُفَ وَأَخِيهِ إِذْ أَنتُمْ جَاهِلُونَ ﴿٨٩﴾

89. Akasema: “Je, mnajua mlivyomfanyia Yusuf na ndugu yake mlipokuwa wajinga?”

قَالُوا أَإِنَّكَ لَأَنتَ يُوسُفُ قَالَ أَنَا يُوسُفُ وَهَـٰذَا أَخِي قَدْ مَنَّ اللَّـهُ عَلَيْنَا إِنَّهُ مَن يَتَّقِ وَيَصْبِرْ
فَإِنَّ اللَّـهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٩٠﴾

90. Wakasema: “Je, wewe ni Yusuf?” Akasema: “Mimi ni Yusuf na huyu ni ndugu yangu! Mwenyezi Mungu ametuneemesha, Hakika mwenye takua na akasubiri basi Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa wafanyao mema.

قَالُوا تَاللَّـهِ لَقَدْ آثَرَكَ اللَّـهُ عَلَيْنَا وَإِن كُنَّا لَخَاطِئِينَ ﴿٩١﴾

91. Wakasema: “Wallah! Mwenyezi Mungu amekufadhilisha kuliko sisi na hakika sisi tumekuwa ni wenye hatia.

قَالَ لَا تَثْرِيبَ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ يَغْفِرُ اللَّـهُ لَكُمْ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿٩٢﴾

92. Leo hapana lawama juu yenu, Mwenyezi Mungu atawasamehe naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wenye kurehemu.”

اذْهَبُوا بِقَمِيصِي هَـٰذَا فَأَلْقُوهُ عَلَىٰ وَجْهِ أَبِي يَأْتِ بَصِيرًا وَأْتُونِي بِأَهْلِكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٩٣﴾

93. Nendeni na kanzu yangu hii na muirushe usoni mwa baba yangu atakuwa ni mwenye kuona, na mje nao watu wenu wote wa nyumbani.

## MIMI NI YUSUF

**Aya 88 – 93**

## MAANA

Basi walipoingia kwa Yusuf walisema: Ewe mheshimiwa! Imetupata shida sisi na watu wetu na tumeleta mali kidogo, basi tupimie kipimo na fanya kama unatupa sadaka, Hakika Mwenyezi Mungu huwalipa wanaotoa sadaka.

Yaa’qub aliwausia wanawe warudi Misr, wakakubali na wakarudi mara ya tatu, wakaingia kwa mheshimiwa wakiwa hoi, wakiomba wahurumiwe na wakaanza kulalamika njaa: tumepatwa na shida pamoja na watu wetu, tupe sadaka, mali yetu ni kidogo, Mungu anawapenda wanaotoa sadaka, Zama huwa zinageuka. Walisema haya wakiwa ni wajukuu wa Ibrahim [a.s] lakini shida imewazidia mambo yakawa kwa namna ambayo hawakutegemea.

Akasema: Je, mnajua mlivyomfanyia Yusuf na ndugu yake mlipokuwa wajinga?

Baada ya Yusuf kusikia malalamiko ya ndugu zake na kusikia shida ya watu wake alishikwa na huruma za udugu, akawaambia kuwalaumu au kuwapa mawaidha kuwa mnakumbuka mlipomwitikia shetani mkamtupa ndugu yenu Yusuf kisimani. Baadae mkamsumbua sana mdogo wake Bin-yamin. Juzijuzi tu mlisema kuwa kama ameiba basi nduguye pia aliiba huko nyuma? Je, mjinga anaweza kufanya zaidi ya mlivyofanya?

Wakasema: Je, wewe ni Yusuf?

Wafasiri hapa wana maneno yasiyoafikiana na Aya, lakini yanaafikiana na maudhui na yanasaidia kuzingatia. Kwa ufupi ni haya: Nduguze Yusuf waliposikia maneno ya Yusuf, walianza kukumbuka umbile la Yusuf, uso wake, sauti yake na ishara za mikono yake.

Kwa vyovyote iwavyo wao au baadhi yao walianza kufikiria kuwa huyo ni Yusuf ndipo wakaanza kusema Je, wewe ni Yusuf? Walisema hivi wakiwa wanangoja jawabu, Basi likawa jawabu ambalo hawakulitegemea:

Akasema: Mimi ni Yusuf na huyu ni ndugu yangu, Mwenyezi Mungu ametuneemesha.

Namtaka msomaji asimame hapa kidogo alinganishe walikuwaje walipoambiwa hayo kulinganisha na walivyokuwa siku walipomtupa kisimani wakiwa hawana dini wala huruma ya udugu?!

Hakika mwenye takua na akasubiri basi Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa wafanyao mema duniani na Akhera.

Makusudio ya wafanyao mema ni wale waliofanya na wakavumilia na kuwa na subira kwenye misukosuko waliyoipata na wakawa mara kwa mara wanazidiwa na waovu, lakini mwisho ni wa wacha Mungu. Ushahidi wa hilo hauanzii kwenye zama za Namrud na kuishia kwa Hitlar tu.

Binadamu leo anakabiliwa na mitihani ya Uzayuni na ukoloni wa Amerika ambao ndio washari wakuu na wafisadi. Hatuna shaka kwamba mwisho wa wote hao utakuwa kama mwisho wa mataghuti waliotangulia.

Hatusemi hivi kwa ushabiki, isipokuwa hiyo ni hali halisi ya kihistoria. Haki ina wenyewe wanaoitafuta na kujitolea mhanga na kwamba heri ina nguvu inayoisaidia, na iko siku itashinda dhidi ya dhulma na utaghuti.

Wakasema: Wallah! Mwenyezi Mungu amekufadhilisha kuliko sisi na hakika sisi tumekuwa wenye hatia.

Walikiri kuwa Mwenyezi Mungu amemfadhilisha kuliko wao kimali, elimu, akili, uzuri na hatimae kwa cheo na heshima. Wakakiri makosa na kuomba msamaha. Yusuf mkarimu na mwana wa mkarimu alisema:

Leo hapana lawama juu yenu, Mwenyezi Mungu atawasamehe

Yusuf alisamehe yaliyopita bila ya nguvu wala lawama na akawaombea Mungu awasamehe waliyoyakosea naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wenye kurehemu, kwa yule anayetubia na akarudi nyuma. Katika Nahjul balagha imesemwa: **“Hasira hazimfanyi kuacha huruma wala huruma hamufanyi kuacha kuadhibu”.**

Kuna hadith Mutawatir kutoka kwa Mtume kwamba alipopata ushindi wa kuiteka Makka aliwaambia makuraish: “Je, mnadhani nitawafanya nini?” Wakasema: “Sisi tunadhania heri tu, ndugu mkarimu na mwana wa ndugu mkarimu.” Akasema: “Basi nendeni zenu nimewaachia huru, leo hapana lawama juu yenu; kama alivyosema ndugu yangu Yusuf.”

Nendeni na kanzu yangu hii na muirushe usoni mwa baba yangu atakuwa ni mwenye kuona na mje nao watu wenu wote wa nyumbani.

Hebu turudi nyuma kwenye Aya 18 ya Sura hii iliyoko Juz, 12, ili tulinganishe kati ya kanzu ya kwanza na hii ya pili: Ya kwanza ilimletea Ya'qub balaa na ugonjwa. Ya pili ikamletea raha na dawa. Vile vile tulinganishe baina ya hali ya wanawe walipoleta ya kwanza walijiomboleza na walipoleta ya pili walikuwa na furaha.

Kama mtu atauliza: iweje kanzu irushwe usoni na kuponyesha? Tutajibu kuwa hatupati tafsiri nyingine isipokuwa muujiza; sawa na moto wa Ibrahim, fimbo ya Musa na kuzungumza kwa Isa akiwa mchanga.

وَلَمَّا فَصَلَتِ الْعِيرُ قَالَ أَبُوهُمْ إِنِّي لَأَجِدُ رِيحَ يُوسُفَ ۖ لَوْلَا أَن تُفَنِّدُونِ ﴿٩٤﴾

94. Na ulipoondoka msafara, baba yao alisema: "Hakika mimi ninasikia harufu ya Yusuf, lau kama hamtanipuuza."

قَالُوا تَاللَّـهِ إِنَّكَ لَفِي ضَلَالِكَ الْقَدِيمِ ﴿٩٥﴾

95. Wakasema: Wallah hakika wewe bado uko katika upotevu wako wa zamani.

فَلَمَّا أَن جَاءَ الْبَشِيرُ أَلْقَاهُ عَلَىٰ وَجْهِهِ فَارْتَدَّ بَصِيرًا ۖ قَالَ أَلَمْ أَقُل لَّكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ مِنَ اللَّـهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٩٦﴾

96. Alipomfikia mbashiri aliirusha kanzu usoni pake akarejea kuona, Akasema: Je, sikuwaambia kuwa mimi ninajua kutoka kwa Mwenyezi Mungu yale msiyoyajua?

قَالُوا يَا أَبَانَا اسْتَغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا إِنَّا كُنَّا خَاطِئِينَ ﴿٩٧﴾

97. Wakasema: "Ewe baba yetu! Tuombee maghufira kwa dhambi zetu, hakika sisi tulikuwa ni wenye hatia.

قَالَ سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّي ۖ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٩٨﴾

98. Akasema: Nitawaombea msamaha kwa Mola wangu. Hakika yeye ni Mwingi wa msamaha, Mwenye kurehemu.

## NASIKIA HARUFU YA YUSUFU

**Aya 94-98**

### MAANA

Na ulipoondoka msafara, baba yao alisema: Hakika mimi ninasikia harufu ya Yusuf, lau kama hamtanipuuza.

Kuondoka msafara ni kuondoka pale ulipokuwa, ambapo ni Misr na kuelekea nchi ya Kanani alipokuwa akikaa Ya'qub. Kupuuza ni kumtuhumu na upotofu.

Dhahiri ya Aya inafahamisha kuwa Ya'qub alinusa harufu ya kanzu ya Yusuf kwa mbali mara tu msafara ulipoanza kuondoka, kabla ya kumaliza nchi ya Misr; ingawaje masafa yalikuwa marefu.

Aliyechukua kanzu ya Yusuf alikuwa masafa ya mwendo wa siku nane, na imesemekana ni siku kumi. Wafasiri wamelibakisha neno na dhahiri yake, wakasema kuwa Ya'qub alipata harufu ya Yusuf hasa pamoja na umbali wa masafa na wakazingatia huo ni muujiza aliomuhusisha nao Mwenyezi Mungu Ya'qub.

Sio mbali kuwa harufu ya Yusuf ni fumbo la makisio ya kutokata tamaa amabayo, huwapata baadhi ya watu; hasa wale wenye nyoyo safi. Na kwamba moyo wa Ya'qub ulihisi kukurubiana kukutana na Yusuf, kwa hiyo akalifasiri hilo kwa harufu.

Maana hayo yanatiwa nguvu na kwama Ya'qub hakukata tamaa ya kukutana na Yusuf hata mara moja. Hilo linatolewa ushahidi na kauli zake katika Sura hii; kama ifuatavyo:

Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye wala msikate tamaa na faraja ya Mwenyezi Mungu, Aya 87 Huenda Mwenyezi Mungu akaniletea wote pamoja. Aya 83 Ewe mwanangu! Usiwasimulie ndugu zako ndoto yako wasije wakakufanyia vitimbi, Aya 5, Juz.12 "Na kadhalika Mola wako atakuteua na atakufundisha tafsiri ya mambo na atatimiza neema yake juu yako, Aya 6, Juz.12 "Mimi ninajua kutoka kwa Mwenyezi Mungu yale msiyoyajua Aya 96.

Wakasema: Wallah hakika wewe bado uko katika upotevu wako wa zamani.

Waliosema ni wale waliokuwepo alipokaa Ya'qub aliposema nasikia harufu ya Ya'qub. Maana ni kuwa waliokuwepo walimwambia Ya'qub kuwa wewe unakosea katika kung'ang'ania kwako kumngoja Yusuf ambaye amekwishakwenda, kama walivyokwenda wengine waliokufa.

Alipomfikia mbashiri aliitupa kanzu usoni pake akarejea kuona.

Ya'qub hakukosea katika hisia zake, Mbashiri (Mwenye kuleta habari njema) alimjia akiwa amechukua kanzu ya Yusuf; mara tu, ile kanzu ilipogusa uso wa Ya'qub, neema ya kuona ikarudi na furaha ya maisha. Inasemekana kuwa aliyechukua kanzu ya Yusuf ni yule yule aliyechukua kanzu iliyotapakazwa damu ya uwongo, miaka arubaini iliyopita, ili afute uovu kwa wema. Vile vile inasemekana kuwa hakuna ajabu ya Ya'qub kurudiwa na macho kwa furaha, kwani mara nyingi raha na furaha huponyesha magonjwa. Majaribio ya tiba yanathibitisha hilo.

Akasema: Je, sikuwaambia kuwa mimi ninajua kutoka kwa Mwenyezi Mungu yale msiyoyajua?

Hii inaashiria kauli yake katika Aya 86 ya Sura hii: "Akasema: Majonzi yangu na huzuni yangu ninamshtakia Mwenyezi Mungu Na ninajua kwa Mwenyezi Mungu yale msiyoyajua"

Wakasema: "Ewe baba yetu tuombee maghufira kwa dhambi zetu, hakika sisi tulikuwa wenye hatia."

Ndugu zake Yusuf walijuta kwa kitendo chao, wakatubia makosa yao, na wakamuomba baba yao awaombee kwa Mwenyezi Mungu kuwatakabalia toba yao na awaghufurie dhambi zao na wakajiwekea sharti la kutorudia maasi.

Akasema: Nitawaombea msamaha kwa Mola wangu. Hakika yeye ni Mwingi wa msamaha, Mwenye kurehemu.

Mmojawapo wa wafasiri wa kisasa anasema: "neno 'nita' haliepuki kuwa kwenye moyo wa mtu aliyejeruhiwa" anamaanisha kuwa moyo wa Ya'qub bado una kitu kwa watoto wake, pamoja na toba yao na kuomba kwao masamaha.

Lakini huku ni kutatizika na kufanya makisio kwa nyoyo za mitume na za watu wengine. Ilivyo hasa ni kuwa Ya'qub, aliahirisha kuwaombea dua

mpaka awe faragha katika mkesha wenye giza aweze kumwomba Mola wake awatakabalie toba. Kwa sababu hilo linapelekea kukubaliwa dua. Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

وَبِالْأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿١٨﴾

Na wanaomba msamaha nyakati za kabla ya Alfajiri (51:18)

وَالْمُسْتَغْفِرِينَ بِالْأَسْحَارِ ﴿١٧﴾

Na wanaoomba maghufira kabla ya Alfajiri Juz.3 (3:17)

فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَىٰ يُوسُفَ آوَىٰ إِلَيْهِ أَبَوَيْهِ وَقَالَ ادْخُلُوا مِصْرَ إِن شَاءَ اللَّـهُ آمِنِينَ ﴿٩٩﴾

99. Na walipoingia kwa Yusuf aliwakumbatia wazazi wake na akasema: Ingieni Misr, Inshallah, mko katika amani.

وَرَفَعَ أَبَوَيْهِ عَلَى الْعَرْشِ وَخَرُّوا لَهُ سُجَّدًا وَقَالَ يَا أَبَتِ هَـٰذَا تَأْوِيلُ رُؤْيَايَ مِن قَبْلُ قَدْ جَعَلَهَا
رَبِّي حَقًّا وَقَدْ أَحْسَنَ بِي إِذْ أَخْرَجَنِي مِنَ السِّجْنِ وَجَاءَ بِكُم مِّنَ الْبَدْوِ مِن بَعْدِ أَن نَّزَغَ الشَّيْطَانُ
بَيْنِي وَبَيْنَ إِخْوَتِي إِنَّ رَبِّي لَطِيفٌ لِّمَا يَشَاءُ إِنَّهُ هُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿١٠٠﴾

100. Na akawapandisha wazazi wake kwenye kiti cha enzi na wakapomoka kumsujudia Na akasema: "Ewe baba yangu! Hii ndio tafsiri ya ile ndoto yangu ya zamani, Mwenyezi Mungu ameijaalia iwe ya kweli, Na Mwenyezi Mungu alinifanyia wema kunitoa gerezani na kuwaleta nyinyi kutoka jangwani baada ya shetani kuchochea kati yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu ni Mpole kwa alitakalo. Hakika yeye ni Mjuzi, Mwenye hekima.

رَبِّ قَدْ آتَيْتَنِي مِنَ الْمُلْكِ وَعَلَّمْتَنِي مِن تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ فَاطِرَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ أَنتَ وَلِيِّي
فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ تَوَفَّنِي مُسْلِمًا وَأَلْحِقْنِي بِالصَّالِحِينَ ﴿١٠١﴾

101. Ewe Mola Wangu! Hakika umenipa utawala na umenifunza tafsiri ya matukio. Ewe mvumbuzi wa mbingu na ardhi! Wewe ndiye walii wangu katika dunia na akhera. Nifishe hali ya kuwa ni Mwislamu na unikutanishe na watu wema."

ذَٰلِكَ مِنْ أَنبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ وَمَا كُنتَ لَدَيْهِمْ إِذْ أَجْمَعُوا أَمْرَهُمْ وَهُمْ يَمْكُرُونَ ﴿١٠٢﴾

Hayo ni katika habari za ghaibu tulizokupa wahyi. Na hukuwa pamoja nao walipoazimia shauri lao wakipanga njama.

## KUKUTANA YUSUF NA YA'QUB

**Aya 99–102**

### MAANA

Na walipoingia kwa Yusuf aliwakumbatia wazazi wake na akasema: "Ingieni Misr, Inshallah, mko katika amani."

Ya'qub alihuzunika sana kwa kumkosa Yusuf, alilia sana huku akijua kuwa kilio hakitafanya kitu, lakini alikuwa akipunguza joto la kufarikiana. Huzuni yake iliendelea kwa muda mrefu sana. Kwa sababu Yusuf alikaa miaka kadha katika nyumba aliyonunuliwa, miaka gerezani, miaka ya kuwa mtumishi wa serikali, ikafuata miaka saba ya mavuno ndipo ikaja miaka ya ukame.

Kila muda ulivyokuwa ukizidi kuendelea ndipo huzuni ya Ya'qub ilivyoendelea; kama inavyoashiria kauli ya waliomwambia: "Wallah hakika wewe bado uko katika upotevu wako wa zamani."

Tukijua kiwango cha huzuni aliyokuwa nayo Ya'qub kwa kumkosa mwanawe, ndipo tutakapojua kiwango cha furaha aliyokuwa nayo kwa kukutana na Yusuf. Kwa sababu furaha ya kupona ugonjwa inakuja kwa kiwango cha maumivu yalivyokuwa au kuzidi furaha.

Baadhi ya wafasiri wamesema kuwa makusudio ya wazazi wake ni baba yake na mama yake mdogo (khalat), kwa sababu mama yake alikuwa ameshakufa. Wengine wakaenda mbali, kwamba mama yake alifufuliwa kaburini, ili aone utukufu wa mwanawe na aweze kumsujudia. Wala hakuna haja ya uhakiki huu na mfano wake; isipokuwa ni kurefusha maneno tu.

**Unaweza kuuliza**: kuwa kifua cha Aya hakiafikiani na mgongo wake, kwa sababu kifua kinasema, Walipoingia kwa Yusuf aliwakumbatia wazazi wake, na inajulikana kuwa Yusuf alikuwa Misr. Mgongo nao unasema: Ingieni Misr, wakati wao tayari wako Misr kwa Yusuf?

**Jibu**: Imesemekana katika jawabu kuwa Yusuf, aliwajengea hema wazazi wake karibu na mpakani huko ndiko walikoingia na akawakumbatia, na walipoanza mwendo wa kutoka kwenye hema wakielekea Misr ndipo alipowaambia ingieni Misr, Jawabu hili linachukua tamko la Aya zaidi ya inavyochukulika. Sio mbali kuwa makusudio ya ingieni Misri ni kaeni humo kwa amani; kama ilivyotokea. Ambapo mfalme aliwakatia ardhi yenye rutuba na kizazi cha Ya'qub kikandelea hapo kwa muda mrefu.

Imelezwa katika Majmaul-bayan "Aliwaambia mko katika amani, kwa sababu wao hapo mwanzo walikuwa wakimuhofia mfalme wa Misr, wala hawawezi kuingia ila kwa Pasipoti yake – yaani pasi za safari kama hivi sasa – Amesema Wahab: kwamba watu wa Ya'qub waliingia Misr wakiwa ni watu 73 na wakatoka pamoja na Musa wakiwa ni watu 600570" Vilevile imeelezwa katika Majmaul-bayan kuwa baina ya Yusuf na Musa kuna miaka 400.

Na akawapandisha wazazi wake kwenye kiti cha enzi.

Aliwakalisha kwenye kiti ambacho alikuwa akikaa yeye akiwa anaendesha mambo ya serikali, kwa ajili ya kuwaadhimisha.

Na wakapomoka kumsujudia.

Waliopomoka ni wazazi pamoja na ndugu zake na aliyesujudiwa ni Yusuf, yaani wazazi wake pamoja na ndugu zake walimsujudia Yusuf. Makusudio ya kusujudi hapa ni kiasi cha kuinama kwa kumuadhimisha na kumtukuza. Na ilikuwa kuinama ndio maamkuzi ya heshima wakati huo, kama ilivyoelezwa katika baadhi ya tafsir.

Imesekana kuwa waliyemsujudia ni inamrudia Mungu na kwamba sijda ilikuwa ni kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa sababu ya neema hii kubwa. Lakini kauli hii inapingana na dhahiri ya Aya wala haifikiani na kauli ya Yusuf katika Aya ya 4. "nimeota zikinisujudia, Yaani kumsujidia yeye sio mwengine.

Na akasema: "Ewe baba yangu! Hii ndio tafsiri ya ile ndoto yangu ya zamani. Mwenyezi Mungu ameijaalia iwe ya kweli.

Anaishiria kauli yake katika mwanzo wa Sura hii, Juz. 12 : “Ewe baba yangu! Hakika mimi nimeota nyota kumi na moja na jua na mwezi nimeota zikinisujudia.” Maelezo yake na ufafanuzi uko huko.
Katika tafsir ya Razi, imeelezwa: “Wametofautiana katika kiwango cha muda baina ya kuota ndoto na kukutana. Ikasemekana ni miaka 80, wengine miaka 70 na ikasemwa ni miaka 40, na hiyo ndio kauli ya wengi; na kwamba umri wake aliishi miaka 120”
Sisi hatujui kwa yakini umri wake ulikuwa miaka mingapi alipotiwa kisimani wala muda aliokaa katika nyumba aliyonunuliwa au muda wake gerezani na kutumikia serikali.
Kwa sababu hatukupata kauli yoyote ya kutegemea kutuongoza kwenye hilo na kauli za wafasiri zimegongana, lakini wengi wamesema kuwa aliishi miaka 120.

Na Mwenyezi Mungu alinifanyia wema kunitoa gerezani na kuwaleta nyinyi kutoka jangwani.

Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) humjaribu mtu kwa raha, kama anavyomjaribu kwa shida. “Akasema: Haya ni katika fadhila za Mola wangu, ili anijaribu nitashukuru au nitakufuru?” (27: 40). Imam Ali (a.s) anasema: **“Hazikuadhimishwa neema za Mwenyezi Mungu na yoyote ila huzidi haki ya Mwenyezi Mungu juu yake kwa cheo”**
Yusuf alipata majaribu ya tabu akavumilia, na ya raha akashukuru. Ndio hapa anazizungumza neema za Mwenyezi Mungu juu yake na kuzihesabu hisani alizofanyiwa: amenitoa gerezani, akanitukuza kwenye cheo na akawaleta watu wangu wa nyumbani, ambapo walikuwa jangwani wakifuga ngamia na mbuzi na kondoo ambao pia nao walimalizwa na ukame wakawa kwenye ardhi tupu isiyo na chochote, wakimwambia mheshimiwa: “Fanya kama unatupa sadaka. Hakika Mwenyezi Mungu huwalipa wanaotoa sadaka”
Wala hakutaka kutaja kutolewa kwake kisimani kwa kuchunga hisia za ndugu zake. Vile vile uadui wao aliuelekeza kwa shetani bila ya kuuelekeza kwao moja kwa moja kwakusema:

Baada ya shetani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu ni mpole kwa alitakalo.

Anawafanyia upole wema na kuwafikisha anapotaka kwenye enzi na utukufu.

Hakika yeye ni Mjuzi Mwenye hekima.

Tofauti baina ya ujuzi wake na hekima yake ni kwamba vitendo vyake vyote na hukumu zake zinakuja kulingana na hekima, “Ewe Mola wetu hukuviumba hivi bure” Juz.4 (3:919).
Ama elimu yake, haiepukani na kinachojulikana. Kwa maneno mengine ni kuwa elimu yake ni kukiambia kitu kuwa kikawa.

Ewe Mola Wangu! Hakika umenipa utawala na umenifunza tafsiri ya matukio. Ewe mvumbuzi wa mbingu na ardhi! Wewe ndiwe mtawala wangu katika dunia na akhera. Nifishe hali ya kuwa ni Mwislamu na unikutanishe na watu wema.

Maana ya mvumbuzi ni kuwa ameziumba bila ya mfano mwingine uliotangulia. Ametaja mbingu kwa tamko la wingi na ardhi kwa tamko la

umoja kwa vile mtu huona kwa macho yake mbingu nyingi, lakini haoni isipokuwa ardhi moja.

Maana ya wewe ni mtawala wangu ni kuwa wewe ndiye unayosimamia mambo yangu yote ya dunia na akhera. Baada ya Yusuf kutaja, neema za Mwenyezi Mungu kwake, alimwelekea Mwenyezi Mungu Mtukufu kumshukuru kwa utawala aliompa na kumuhusisha na utume, akiwa amewakilisha kwake mambo yake yote huku akimwomba afe kwenye utifu na radhi zake Mwenyezi Mungu na pia amjumuishe na watu wema waliopita miongoni mwa wazazi wake na amjalie ni kizazi chema kilichobakia baada ya wazazi wake.

Hayo ni katika habari za ghaibuu tulizokupa wahyi.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja kisa cha Yusuf, alimwelekea Mtume wake mtukufu Muhammad **(s.a.w.w)** kwa Aya hii. Lengo ni kutoa hoja kwa anayekanusha utume wake.

Ufupisho wake ni kuwa hayo tuliyoyasimulia kuhusu Yusuf, kwa ufafanuzi huu, hakuyashuhudia Muhammad **(s.a.w.w)** wala kuyasoma katika kitabu au kusikia kutoka kwa mtu yeyote, isipokuwa ni Wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu unaojulisha ukweli wake na utume wake.

Na hakuwa pamoja nao walipoazimia shauri lao wakipanga njama.

Walioazimia ni ndugu wa Yusuf. Anayeambiwa ni Muhammad **(s.a.w.w)**. Watu wote wanajua kuwa Muhammad **(s.a.w.w)** hakuwako wakati walipofanya shauri la kumtupa Yusuf shimoni na pia walipofanya njama kwa baba yake kusema kuwa ameliwa na mbwa mwitu.

Vilevile watu wanajua kuwa Muhammad **(s.a.w.w)** hakusoma kitabu wala kuwa mwanafunzi wa ustadh yeyote. Kwa hiyo basi hakuna njia iliyobaki ya kuyajua hayo isipokuwa wahyi wa mbinguni.

Mfano wa Aya hii ni ile isemayo: "Hizo ni habari za ghaibuu tunazokupa wahyi, Hukuwa ukizijua wewe wala watu wako kabla ya hii. Basi subiri! Hakika mwisho ni wa wacha Mungu." Juz.12 (11:49)

## JE, KISA CHA YUSUF NI CHA MAPENZI?

Kwa mtazamo wa juu juu, inaweza kudhaniwa kuwa sura ya Yusuf inafanana na kisa ambacho mhusika mkuu ni mwanamke aliyetawaliwa na tabia ya kike iliyompa ashiki kwa kijana mtanashati ambaye hajapatapo kumuwaza mwingine mfano wake kwa uzuri, na kwamba kijana huyo alijizuia kwa uchaji Mungu wake na kuhofia hisabu na malipo ya Mungu, sawa na kisa cha Sallam Mughniya pamoja na Abdurrahman Al-Qass[1].

Kuna baadhi ya watu wanasema kuwa ingelikuwa vizuri kama kisa hiki kisingetajwa katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, Baadhi ya waumini wanasema kuwa Mwenyezi Mungu ana hekima ya ndani katika Sura hii ambayo hatuijui.

Hawa wakawa wamejichunga sana; kama walivyokosea Khawarij Maymuniya walipoikana sura ya Yusuf kwa vile ni kisa cha mapenzi jambo ambalo liliwatoa nje ya madhehebu ya Kiislamu.

Hakika tuliyoishilia nayo, wakati tukifasiri Sura hii ni kwamba mwenye kuisoma kwa kuitilia manani na kuzingatia maana yake (Tadabbur) na akagundua siri zake na malengo yake ataamini kabisa kwamba Sura hii

1. Kinapatikana katika Aqdulfarid Juz 7.

inaeleza mfano ulio wazi zaidi kuwa mara nyingi kushikamana na msimao wa kiroho ni nyenzo ya kufaulu katika maisha haya yaliyojaa ufisadi.
Mwenye kuisoma kijujuu atasema kama walivyosema Maymuniya kuwa ni kisa cha mapenzi au walivyosema baadhi ya waumini kuwa Mungu ana hekima isiyojulikana katika kisa hiki. Ni kweli hawezi kuijua isipokuwa yule mwenye kuyazingatia vizuri (kuyafanyia tadabbur) maneno ya Mwenyezi Mungu na Aya zake.
Tutaonyesha baadhi ya uhakika ulioko kwenye sura hii unaojitokeza kwa kila mwenye kuutafuta, kama ifutatavyo:-
1. Mvutano baina ya haki na batili unaendelea daima katika maisha haya, wala haitapatikana suluhu baina yake. Natija ya kimaumbile ya hilo ni kwamba mwenye kufuata njia ya batili atapata upinzani kutoka kwa wenye haki, lakini kwa njia ya uadilifu na ukweli, sio kwa uwongo na hadaa. Kwa sababu wao hawaitaki silaha isiyokubaliwa na haki na uadilifu.
Vile vile naye mwenye kufuata njia ya haki atapigwa vita na wabatilifu, lakini kwa uzushi na kila aina ya vitimbi. Kwa sababu mwenye kung'ang'ania ubatilifu, hana silaha isipokuwa kupotoa na kuzulia. Ndio maana haki ikawa ni ghali na yenye takilifa nyingi kwa anayeifuata na kushikamana nayo.
Mwenyezi Mungu amepigia mfano wa hakika hii kwa Sura ya Yusuf. Mke wa mheshima alimtaka Yusuf, lakini akakafaa na akajihifadhi kwa sababu ya kumcha Mungu (takua).
Akamtishia kifungo kama hatafanya lakini akajizuia na wala asifanye huku akisema: "Ewe Mola wangu! Gereza linapendeza zaidi kwangu kuliko haya wanayoniitia"; Kwa hiyo akajitolea kwa thamni ghali kuliko nafsi yake kwa sababu dini ina thamani na ni ghali zaidi.
Hata hivyo wale wanaoipinga haki mwisho wanaangusha silaha chini kwa wenye haki, kama ilivyotokea kwa nduguze Yusuf na mke wa mheshimiwa.
2. Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Kama asingeona dalili ya Mola wake," inatupa udhibiti wa kiujumla na makisio sahihi ya mapambano baina ya mumin na asiyekuwa mumin. Mwenye kuitikia buruhani hii wakati wa mtihani, kama alivyofanya Yusuf, basi huyo ni katika wale ambao imani na yakini imetulizana katika nyoyo zao kwa haki na uadilifu. Na mwenye kusukumwa na matamanio na shahawa zake na akajitia hamnazo akaacha buruhani ya mola wake, basi huyo hana dini kitu.
3. Yanapotokea matatizo watu wema wanajulikana na kuwa ni tegemeo la watu, kama alivyo tegemea mfalme wa Misr kwa Yusuf akiwa yuko gerezani, ili aweze kuikinga nchi na balaa la miaka ya ukame. Hali ya ufisadi inawainua waovu na kuwaweka chini wema, lakini shida na matatizo yanadhihirisha hakika ya mambo.
4. Kuizowesha nafsi kutegemea njia ya haki kutaleta natija nzuri na bora. Yusuf alivumilia kisimani, gerezani, kuuzwa kama mtumwa na kutuhumiwa, lakini natija ikawa yeye ndiye bwana mkubwa mheshimiwa, anaambiwa na mfalme "Hakika wewe leo kwetu ni mwenye heshima mwenye kuaminika." Na nduguze Yusuf wanasimama wakiwa wamehemewa wakitaka kuhurumiwa huku wakisema: "basi tupimie kipimo na fanya kama unatupa sadaka; hakika Mwenyezi Mungu huwalipa

wanaotoa sadaka" Na mwisho wanakuja kumsujudia. "mvumilivu hula mbivu".

Huu ndio mtazamo wa haraka haraka wa baadhi ya mazingatio na mafundisho ya sura hii tukufu. Mwenye kutaka ufafanuzi na aisome kwa ukamilifu pamoja na tafsiri yake.

4

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

103. Na watu wengi si wenye kuamini ujapopupia.

وَمَا تَسْأَلُهُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۚ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٠٤﴾

14. Wala wewe huwaombi ujira kwa haya. Haikuwa hii ila ni mawaidha kwa wal- imwengu

وَكَأَيِّن مِّنْ آيَةٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ يَمُرُّونَ عَلَيْهَا وَهُمْ عَنْهَا مُعْرِضُونَ ﴿١٠٥﴾

105. Ni ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipitia na hali ya kuwa wanazipuuza.

وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُم بِاللَّهِ إِلَّا وَهُم مُّشْرِكُونَ ﴿١٠٦﴾

106. Na wengi wao hawamwamini Mwenyezi Mungu pasi na kuwa ni washirikina.

أَفَأَمِنُوا أَن تَأْتِيَهُمْ غَاشِيَةٌ مِّنْ عَذَابِ اللَّهِ أَوْ تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٠٧﴾

107. Je wanaaminisha kuwajia adhabu ya Mwenyezi Mungu ya kuwagubika au kuwafikia saa (Kiyama) kwa ghafla na hali hawatambui?

## NA WATU WENGI SI WENYE KUAMINI AYA

**Aya 103-107**

### MAANA

Na watu wengi si wenye kuamini ujapopupia.

Muhammad **(s.a.w.w)** ana ishara na miujiza inayojulisha juu ya utume wake, zikiwemo sharia na sera zake. Nyingine ni Qur'an na ufasaha wake, mafunzo yake, uhakika wake na kutolea habari mambo ya ghaibuu. Miongoni mwa ghaibuu hizo ni kisa cha Yusuf kwa ufafunuzi wake, kama tulivyotaja katika Aya 102 ya Sura hii.

Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** alikuwa akipupia sana watu waamini na waongoke, hasa kaumu yake ya kiquraish, lakini wengi wao hawakuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu, kwa sababu ya masilahi yao binafsi; kama vile viongozi na wenye nguvu, au kwa sababu ya ujahili na kuiga; kama vile wanyonge na wafuasi.

Katika Aya hii Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwambia mtume wake mtukufu kuwa wewe huwezi kumwongoza umpendaye pamoja na ikhlasi yako na miujiza yako na wewe huna haja nao wala imani yao.

Wala wewe huwaombi ujira kwa haya. Haikuwa hii ila ni mawaidha kwa walimwengu.

Neno 'hii' ni Qur'an ambayo inaongoza kwenye usawa ikizielekeza akili kwenye ishara za Mwenyezi Mungu na dalili za uadilifu na umoja wake. Inaongoza na kuelekeza kupitia mdomoni mwa Mtume Mtukufu Muhammad **(s.a.w.w)**

Ni ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipitia na hali ya kuwa wanazipuuza.

Kana kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anamwambia Mtume wake, wewe tulia moyo wako wasipokuamini wewe na dalili za utume wako, kwani wao wamenikufuru mimi nikiwa muumba wao na mwenye kuwaruzuku. Nimeujaza ulimwengu dalili za utukufu wangu na uwezo wangu, lakini bado wakazipinga. Basi hakuna ajabu wakikupinga wewe pamoja na miujiza iliyodhihiri mikononi mwako.

Na wengi wao hawamwamini Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni washirikina.

Hili ni jawabu la swali linalokadirika kutokana na Aya iliyotangulia, “Na watu wengi siwenye kuamini ujapopupia. Swali lenyewe linakuja hivi: Vipi Mwenyezi Mungu aseme watu wengi hawaamini na inajulikana kuwa waarabu na watu wa Kitabu wanakiri kuweko muumba na wao ndio waliokuwa watu wengi wakati huo? Bali Qur’an yenyewe inakubali hilo wazi wazi pale iliposema: “Na ukiwauliza ni nani aliyeumba mbingu na ardhi na akalitiisha jua na mwezi? Bila shaka watasema ni Mungu” (29:16).

Kwa hiyo ndio Mwenyezi Mungu (s.w.t) akajibu swali hili la kukadiriwa kwa kusema wengi wao kuamini kwao hakuachani na ushirikina, yaani wanamshiriksha Mungu, Wanakubali kuwa mumba yuko, lakini wengi wao wana mfanyia washirika.

Kwa mfano Mayahudi au kikundi katika wao wanasema Mungu ana mtoto anayeitwa Uzayr, Manaswara (wakirsto) nao wanasema mtoto wa Mungu ni Masih. Waarabu wanayashirikisha masanamu katika ibada wanamwambia Mwenyezi Mungu: labeka huna unayeshirikiana naye isipokuwa anayeshirikiana nawe. Kwa hiyo hakuna tofauti baina ya anayekanusha na anayeshirikisha.

Je wanaaminisha kuwajia adhabu ya Mwenyezi Mungu ya kuwagubika au kuwafikia saa (kiyama) kwa ghafla na hali hawatambui?

Katika aya 103 Mweyezi Mungu(s.w.t.) alimwambia mtume wake kuwa wao hawakuamini katika 105 alimwambia wao wamenikufuru mimi hali ya kuwa ni muumba na katika 106 akasema hata wale wanaonikubali wananifanyia washirika. Ikawa ni mazoweya ya kuyafuatishia haya kwa makemeo na kiaga cha adhabu kali.

**Unaweza kuuliza**: Kutaja ghafla hakuhitajii tena kutaja hawatambui, je, kuna lengo gani la kukaririka?

**Jibu**: Neno ghafla linaashiria kutokea adhabu wakiwa macho, lakini kutotambua inawezekana kuwa katika hali ya kuwa macho au kulala, kama alivyosema Mwenyezi Mungu (s.w.t):

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَتَاكُمْ عَذَابُهُ بَيَاتًا أَوْ نَهَارًا ﴿٥٠﴾

Sema: Mwaonaje ikiwafikia adhabu yake usiku au mchana” Juz.11 (10:50)

قُلْ هَـٰذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّـهِ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي وَسُبْحَانَ اللَّـهِ وَمَ ا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٨﴾

108. Sema: Hii ndiyo njia yangu ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa busara mimi na wanaonifuata. Na ametakasika Mwenyezi Mungu! Wala mimi si katika washirikina.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُّوحِي إِلَيْهِم مِّنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ ۗ أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنظُرُوا
كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۗ وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِّلَّذِينَ اتَّقَوْا ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٠٩﴾

109. Na hatukuwatuma Mitume kabla yako isipokuwa ni wanaume tuliowapa wahyi miongoni mwa watu wa mijini. Je, hawatembei katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Na hakika nyumba ya Akhera ni bora kwa wenye takua, Basi hamtii akili?

حَتَّىٰ إِذَا اسْتَيْأَسَ الرُّسُلُ وَظَنُّوا أَنَّهُمْ قَدْ كُذِبُوا جَاءَهُمْ نَصْرُنَا فَنُجِّيَ مَن نَّشَاءُ ۖ وَلَا يُرَدُّ بَأْسُنَا
عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١١٠﴾

110. Hata mitume walipokata tamaa na wakadhani kuwa wamekadhibishwa, hapo ikawajia nusra yetu, wakaokolewa tuwatakao, na adhabu yetu haiondolewi kwa kaumu ya wakosefu.

لَقَدْ كَانَ فِي قَصَصِهِمْ عِبْرَةٌ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ۗ مَا كَانَ حَدِيثًا يُفْتَرَىٰ وَلَٰكِن تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ
يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ كُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿١١١﴾

111. Kwa hakika katika simulizi zao mna mazingatio kwa wenye akili. Si hadithi za kuzuliwa, lakini ni kusadikisha yaliyo kabla yake na ufafanuzi wa kila kitu na ni uwongofu na rehema kwa kaumu yenye kuamini.

## SEMA HII NI NJIA YANGU

**Aya 108 -111**

### MAANA

Sema: Hii ndiyo njia yangu ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa busara mimi na wanaonifuata.

Mwenyezi Mungu alimwamrisha Muhammad awaambie washirikina kuwa hii ndiyo njia yangu na desturi yangu, hakika yake iko dhahiri na ni halisi, ni mwito wa Mwenyezi Mungu kutokana na elimu, hoja na mantiki.

Hakuna mwenye shaka kuwa mitume wote na wafuasi wao wenye ikhlasi wanalingania kwenye imani ya Mungu na siku ya mwisho, kusimamisha haki na uadilifu, kuwa wanafanya hayo kwa hekima na mawaidha mazuri, na kukabiliana na hoja kwa hoja na fikra kwa fikra, kwenye mantiki yaliyosalimika ambayo yanategemea risala ya mitume na mwito wa viongozi wema.

Na ametakasika Mwenyezi Mungu! Wala mimi si katika washirikina.

Huu ni ubainifu na tafsiri ya mwito wa Muhammad **(s.a.w.w)** kwamba umetakasika na kila aina ya shirki.

Na hatukuwatuma mitume kabla yako isipokuwa ni wanaume tuliowapa wahyi miongoni mwa watu wa mijini.

Makusudio ya miji ni yoyote ile iwe mikubwa au midogo sio mashambani. Wafasiri wamesema:

Inafahamisha aya kuwa Mwenyezi Mungu hakutuma mtume mwanamke kabisa wala mwanamume kutoka mashambani, kwa sababu wao ni wazito wasiokuwa na maana.

Wafasiri wamewataja watu wa mashambani kuwa hawana maana na wakasahau kuwa wao ndio wakweli zaidi wa lahaja wenye maumbile safi ya tabia kuliko watu wa mijini, na pia wamesahau wanawake wa mjini wanavyojishughulisha kupaka rangi za mdomo na kujikwatua nyuso.

Hali yoyote iwayo ni kuwa Mwenyezi Mungu ndiye anayejua zaidi pa kuweka ujumbe wake.

Ama lengo la Aya ni kutoa hoja kwa yule anayepinga risala ya Muhammad **(s.a.w.w)** kwamba yeye hakuwa peke yake katika ujumbe wake. Walikuweko watu wa kawaida mfano wake kabla yake, wakila chakula wakitembea masokoni mijini na mwito wao ulikuwa sawa na wake.

Sasa mnaona ajabu gani, enyi washirikina, kwenye risala ya Muhammad, na msione ajabu ya kutumwa mwenginewe?

Aya hii inafaa kuwa jawabu la wale aliowaashiria Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Aya:

وَإِذَا رَأَوْكَ إِن يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُوًا أَهَـٰذَا الَّذِي بَعَثَ اللَّـهُ رَسُولًا ﴿٤١﴾

Na wanapokuona hawakufanyii ila kejeli tu: je, huyo ndiye Mwenyezi Mungu amemtuma kuwa mtume? ( 25:41)

Je, hawatembei katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha?

Umetangulia mfano wake katika Juz 4 (3:137).

Na hakika nyumba ya Akhera ni bora kwa wenye takua, Basi hamtii akili?

Kusema kwake “kwa wenye takua” ni dalili wazi kuwa njia ya wema wa mtu katika akhera ni amali njema hapa duniani na amali bora zaidi humu duniani ni ile inayolenga heri ya mtu na kuongoka kwake, kuchunga haki yake na uhuru wake usichezewe na dhulma.

Hata mitume walipokata tamaa na wakadhani kuwa wamekadhibishwa, hapo ikawajia nusra yetu, wakaokolewa tuwatakao, na adhabu yetu haiondolewi kwa kaumu ya wakosefu.

Makusudio ya wakadhani, hapa ni kuwa na yakini, yaani wakaona. Mitume waliwalingania umma kwa Mungu na hawakuitikiwa, wakawaonya na adhabu kali ya dunia kabla ya akhera, lakini wakadharau
na kufanya maskhara. Mitume wakangoja adhabu iwashukie wenye dharau, lakini muda ukawa mrefu kiasi cha kukata tamaa na kudhani kuwa adhabu haitakuja na kiaga hakitakamilika. Lakini hatimaye adhabu ikwashukia wakosefu na wenye takua wakaokoka bila ya kuguswa na dhara yoyote au kuhuzunika.

Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu “walikata tamaa na wakadhani” ni fumbo tu la machungu ya kungoja sana. Mifano ya mfumo huu wa mafumbo ni mingi na imezoeleka katika lugha ya kiarabu na fasihi yake.

Hata hivyo wafasiri hapa wana kauli na rai zilizo mbali kabisa na ufahamisho wa matamko na mfumo mzima wa maneno, mbali ya kuwa unamzidisha msomaji kuduwaa na kupotea.

Kwa hakika katika simulizi zao mna mazingatio kwa wenye akili.

Neno akili hapa limefasiriwa kutoka na neno lub lenye maana ya kokwa au kiini. Akili imeitwa hivyo kwa vile ndio kitu muhimu kwa binadamu. Maana ya simulizi zao ni masimulizi ya Yusuf na nduguze pamoja na mke wa mheshimiwa na mfalme.

Tumekwisha bainisha kuwa katika kisa cha Yusuf kuna mafunzo aina kwa aina, yaliyomuhimu zaidi ni kuwa mwenye kuachana na watu na akamtegemea Mungu peke yake lazima mwisho wake utakuwa mwema.

Si hadithi za kuzuliwa, lakini ni kusadikisha yaliyo kabla yake na ufafanuzi wa kila kitu na ni uwogofu na rehema kwa kaumu yenye kuamini.
Kila kilichokuja katika Qur'ani ni haki na ukweli, kikiwemo kisa cha Yusuf. Na kimekuja kama alivyokieleza Mwenyezi Mungu kwa Mitume wake waliotangulia katika vitabu vya mbinguni. Na inajulikana kuwa Muhammad hakukisoma yeye mwenyewe wala kukisikia kwa mwinginewe.
Zaidi ya hayo ni kuwa katika Qur'an kuna ubainifu wa itikadi na sharia, na kwamba hiyo ni uwongofu kwa anayetaka uwongofu kwa njia yake na rehema kwa yule atakayetumia hukumu zake na kuwaidhika na mawaidha yake. Hakuna shaka kwamba wanaowaidhika na uwongofu wa Mwenyezi Mungu ni wale.

الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُم بِظُلْمٍ أُولَـٰئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُم مُّهْتَدُونَ ﴿٨٢﴾

"Ambao wameamini na hawa kuchanganya imani yao na dhullma, Hao ndio watakaopata amani na ndio waliongoka" Juz 7 (6:82).

## MWISHO WA SURA YA KUMI NA MBILI

5

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

Sura Ya Kumi Na Tatu: Surat Ar-Ra'd
Imeshuka Madina, ina Aya 43

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

المر تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ وَالَّذِي أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ الْحَقُّ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١﴾

1. Alif Laam Raa. Hizo ni Aya za Kitabu. Na uliyoteremshiwa kutoka Mola wako ni haki lakini watu wengi hawaamini.

## HIZO NI AYA ZA KITAB

**Aya 1**

### MAANA

Alif Laam Raa.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 1 mwanzo wa Sura Baqara.

Hizo ni Aya za Kitabu.

Yaani Aya za Sura hii ni katika Qur'an Tukufu. Lengo la kutoa habari hii ni kubainisha kuwa sura hii ni haki kwa sababu ni katika Qur'an. Kwa vile Qur'an ni haki basi nayo ni haki. Haya ndiyo makusudio ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Na uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako ni haki.

**Hapa linakuja swali**: Kuna dalili gani kuwa Qur'an ni haki?
**Jibu**: utalipata Juz. 1 (2:23-25) Imam Ali (a.s) anasema: **"Hakika Qur'an dhahiri yake ni safi na undani wake ni wa kina, maajabu yake hayaishi wala giza haliondoki ila kwayo."**

Lakini watu wengi hawaamini Qur'an wala kauli nyingine ya haki na uadilifu ila yule anayeona heri yake ni heri ya watu na shari yake ni shari yao pia.

Mtu mmoja katika watu wa Mungu aliambiwa kuwa soko limeungua lakini duka lako halikuungua, akasema: Alhamdullilah. Kisha akatanabahi kuwa ameasi kwa kujitakia yeye binafsi heri kuliko watu wengine, akatubia dhambi yake na akaomba msamaha.

Mfano wa watu hawa ni wachache ambao wanawafikiria wengine, ndio aliowakudia Mwenyezi Mungu kwa kusema: 'Lakini watu wengi hawaamini".

اللَّـهُ الَّذِي رَفَعَ السَّمَاوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلٌّ يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَمًّى يُدَبِّرُ الْأَمْرَ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُم بِلِقَاءِ رَبِّكُمْ تُوقِنُونَ ﴿٢﴾

2. Mwenyezi Mungu ndiye aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona; kisha akatawala kwenye Arshi na amelitiisha Jua na Mwezi, kila kimoja kinaendelea mpaka muda uliotajwa. Anayapanga mambo Anazipambanua ishara, ili mpate kuwa na yakini ya kukutana na Mola wenu.

وَهُوَ الَّذِي مَدَّ الْأَرْضَ وَجَعَلَ فِيهَا رَوَاسِيَ وَأَنْهَارًا ۖ وَمِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ جَعَلَ فِيهَا زَوْجَيْنِ اثْنَيْنِ ۖ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٣﴾

3. Na yeye ndiye aliyeitandaza ardhi. Na akaweka humo milima na mito. Na katika kila matunda akafanya humo viwili viwilidume na jike. Huufunika usiku kwa mchana. Hakika katika hayo zimo ishara kwa watu wanaofikiri.

وَفِي الْأَرْضِ قِطَعٌ مُّتَجَاوِرَاتٌ وَجَنَّاتٌ مِّنْ أَعْنَابٍ وَزَرْعٌ وَنَخِيلٌ صِنْوَانٌ وَغَيْرُ صِنْوَانٍ يُسْقَىٰ بِمَاءٍ وَاحِدٍ وَنُفَضِّلُ بَعْضَهَا عَلَىٰ بَعْضٍ فِي الْأُكُلِ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٤﴾

4. Na katika ardhi mna vipande vilivyokaribiana. na zipo bustani za mizabibu na mimea mingine na mitende ichipuayo kwenye shina na isiyochipua kwenye shina moja inayonyweshwelezwa maji yale yale Na tunaifanya bora baadhi yake kuliko mingine katika kula. Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanotia akilini (mambo).

## AMEINUA MBINGU BILA YA NGUZO

**Aya 2-4**

### MAANA

Mwenyezi Mungu ndiye aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona.

Yaani mnaziona hizo mbingu, Maana ni kuwa hakika Mwenyezi Mungu ameziinua mbingu kwa amri yake nazo zimeinuliwa hasa kama mnavyoziona bila ya nguzo.

Katika Mustadrak Nahjul-balagha imeelezwa kuwa Imam Ali (a.s) alizisifu mbingu kwa kusema: **"Ameinua mbingu bila ya nguzo – yaani kihalisi na kidhahiri – na akaitandika ardhi hewani bila ya nguzo".**

Kisha akatawala kwenye arshi.

Hili ni fumbo kuwa yeye anamiliki ulimwengu na kupangilia mambo yake kwa elimu yake na hekima yake, kama alivyosema: 'Anayepanga mambo.' Jumla hii imekwishapita katika Juz. 8 (7:54) na katika Juz. 11 (10:3).

Na amelitiisha Jua na Mwezi, kila kimoja kinaendelea mpaka muda uliotajwa.

Kwa nidhamu, kama yaonavyo macho yetu na kwa lengo maalum kama zinavyotambua akili zetu.

Jua linapita kwenye falaki yake katika mwaka, na mwezi nao unapita kwenye falaki yake kwa muda wa mwezi mmoja. Vilikuwa hivyo tangu mamilioni ya miaka iliyopita na vitaendelea hivyo mpaka atakapotaka Mwenyezi Mungu.

Hakuna mwaka unaotofautiana na mwingine wala muda unaotofautiana na muda mwingine. Hii ni dalili mkataa ya kuweko mjuzi mwenye hekima. Ama sadfa inabatilishwa na nidhamu na kukaririka mambo.

Anayapanga mambo yote bila ya kubakisha, yakiwemo kulitiisha jua na mwezi, kutuma mitume kuteremsha vitabu n.k.

Anazipambanua ishara, Anabainisha dalili za kupatikana kwake, Kwa nini anafanya hivyo?

Ili mpate kuwa na yakini ya kukutana na Mola wenu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameumba ulimwengu na akaupanga kwa ukamilifu katika njia zote. Akili iliyosalama inatambua mipangilio hii na

kupata dalili kwayo ya kupatikana mzingatiaji mwenye hekima na uweza wake wa kurudisha viumbe.
Kwa sababu mwenye kuweza kuuleta ulimwengu uliokuwa hauko na akaupangilia pamoja na vilivyomo ndani yake, zikiwemo nyota na sayari nk, kwa mpangilio wa kiuhakika, basi bila shaka atakuwa na uwezo zaidi wa kuukusanya pamoja baada ya kutawanyika.
Ukithibiti kwa akili uwezo wa kuurudisha, na mkweli mwaminifu akautolea habari kwa wahyi, basi kutokea kwake ni kwa lazima.
Baada Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja mbingu ametaja ardhi na lengo ni moja - kuwatanabaisha walioghafilika kwenye dalili za kiulimwengu za kupatikana Mwenyezi Mungu na utukufu wake.
Na kwamba mwenye kuumba ulimwengu huu mkubwa pamoja na ardhi yake na mbingu yake anaweza kutuma mitume na kuteremsha vitabu, kufufua wafu.
Dalili hizo miongoni mwake ziko za mbinguni; kama vile kuinua mbingu bila ya nguzo, kulitiisha jua na mwezi n.k. Na nyingine ni za ardhini; kama zile alizoziashiria Mwenyezi Mungu kwa kauli zifuatazo:
1. Na yeye ndiye aliyeitandaza ardhi yaani aliyeitandika.
Mahali pengine Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَاللَّـهُ جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ بِسَاطًا ﴿١٩﴾

“Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye wafanyia ardhi kuwa busati” (71:19)

وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَٰلِكَ دَحَاهَا ﴿٣٠﴾

“Na ardhi baada ya hayo akaitandika” (79:30)
Inavyoonyesha ni kwamba kutandazwa ardhi na kutandikwa pamoja na upana wake, hakuna uhusiano wowote na kuwa ardhi ni mviringo au ni bapa. Kwa sababu kitu kikiwa kikubwa sana, kama ardhi, kila upande wake unakuwa umeenea kwa upana na urefu, hata kama kiko mviringo.
Kwa hiyo basi Aya haizuii kuwa ardhi ni mviringo, jambo ambalo halina shaka. Razi anasema katika kufasiri Aya hii: “Hakika imethibiti, kwa dalili kwamba, ardhi ni tufe na ardhi ni kitu kikubwa na tufe likiwa ni kubwa sana basi kila sehemu yake inaonekana kama bapa.”
Wataalamu wa Kiyunani (kigiriki) katika enzi za Aristatle, waliafikiana kuwa ardhi ni mduara, lakini wakasema kuwa imetulia.
2. Na akaweka humo milima.
Neno milima limefasiriwa kutoka na neno Rawasi lenye maana ya kila kitu kilichothibiti mahali, lakini neno hili limetumika zaidi kwa milima, kiasi ambacho likitajwa tu bila ya nyongeza, inafahamika kuwa ni milima.
Hekima ya kupatikana hiyo milima ni utulivu wa ardhi na uthabiti wake, Mwenyezi Mungu anasema: “Je, hatukuifanya ardhi kuwa ni tandiko na milima kuwa ni vigingi?” (78:7).
3. Na mito.
Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekutanisha kutaja milima na mito kwa sababu mito inachimbuka kutoka humo milimani. Anasema:

وَجَعَلْنَا فِيهَا رَوَاسِيَ شَامِخَاتٍ وَأَسْقَيْنَاكُم مَّاءً فُرَاتًا ﴿٢٧﴾

“Na tukaweka humo milima mirefu na tukawanywesha maji tamu” (77:27)
4. Na katika kila matunda akafanya humo viwili viwili–dume na jike.

Kila aina ya matunda ina dume na jike katika aina zake kwa dhahiri, kama vile mtende dume mtende jike, au kwa undani, kama mimea mingine.
Sheikh Al-Maraghi, katika tafsiri yake, anasema: "Imethibitisha elimu hivi sasa kwamba mti na mmea wowote hauzai matunda isipokuwa kwa ushirikiano baina ya wa kike na wa kiume. Aghlabu mbegu zinakuwa katika mti mmoja kama ilivyo miti mingi, au katika miti miwili tofauti, kama ilivyo kwa mtende."
Katika jarida la Al-ulum la Lebanon toleo la Juni 1967 kwenye kichwa cha maneno "Vipi uhai unakuwa katika vitu", imeelezwa kuwa vidudu vinachukua mbegu za uzazi kwenye mwili wake kupeleka kwenye makole ya maua bila ya kukosea, na kwamba ndege wanachukua mbegu za uzazi za yungi yungi kwenye midomo yao. Hakika ni muujiza.
Katika vita kuu vya ulimwengu vya pili walifika wapiganaji huko Corse, zaituni ikapata magonjwa na matunda yakapungua. Amerika ikataka kusaidia kutatua tatizo hilo, Kwa hiyo wakanyunyizia miti dawa ya DDT. Vidudu vya maradhi vikafa, lakini vikafa na vidudu vingine. Katika mwaka uliofuatia natija ikawa ni kutopatikana chochote! Si zaituni si limao wala lozi.
Kwa hiyo inatubainikia kuwa mimea haiwezi kuzaa matunda isipokuwa kwa kukutana mbengu za kike na za kiume.
5. Huufunika usiku kwa mchana.
Imepita tafsiri yake katika Juz. 8 (7:54).
Hakika katika hayo zimo ishara kwa watu wanaofikiri.
Katika ulimwengu huu ambao unakwenda kulingana na kanuni thabiti zisizotetereka kwa hali yoyote ile. Lau si uthabiti wake, isingeliwezekana kwa wataalamu kuuchunguza na kuuelewa. Ilivyo ni kwamba linalodumu linapinga sadfa. Na kwa ajili hii wataalamu wengi wa maumbile wameamini kuweko Mungu.
Na katika ardhi mna vipande vilivyokaribiana.
Ardhi imeungana, lakini kuna sehemu kadhaa zinazotofautiana, kuna tambarare, milima na mabonde. Pia kuna udongo mgumu na mchangatifu, changarawe na utelezi, weusi na weupe n.k. Siri ya hilo ni amri ya Mwenyezi Mungu na upangiliaji wake katika kuumba.
Na zipo bustani za mizabibu na mimea mingine na mitende ichipuayo kwenye shina, Ni mitende ya aina moja.
Na isiyochipua kwenye shina moja ni ile mitende inayotokana na mashina tofauti. Amehusisha kutaja mizabibu na mitende kwa sababu ndiyo matunda yanayopatikana sehemu nyingi au ndio yenye chumo na pengine ndiyo iliyokuwa muhimu wakati huo. Hilo linafahamika kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَاضْرِبْ لَهُم مَّثَلًا رَّجُلَيْنِ جَعَلْنَا لِأَحَدِهِمَا جَنَّتَيْنِ مِنْ أَعْنَابٍ وَحَفَفْنَاهُمَا بِنَخْلٍ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمَا زَرْعًا ﴿٣٢﴾

"Na wapigie mfano wa watu wawili: Mmoja wao tulimjalia vitalu viwili vya mizabibu na tukavizungushia mitende na kati yake tukatia mimea ya nafaka" (18:32)
Inanyweshwelezwa maji yale yale; kama vile mvua, kisima au mto. Pia sehemu ni moja kwa kukarubiana, lakini matunda yanatofautiana kirangi,

ukubwa, harufu na hata ladhaa. Siri ya hilo ni upangiliaji wake Mwenyezi Mungu na hekima yake.

Na tunaifanya bora baadhi yake kuliko mingine katika kula pamoja na kuwa nyezo za kumea kwake ni aina moja.

Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanaotia akilini (mambo).

Yaani tofauti hii inayopatikana katika nyezo za aina moja, yakiwemo maji na hewa, ni dalili wazi ya kuweko mpangiliaji mambo vizuri, kwa yule ambaye haamini kitu ila baada ya kufikiri na kutia akilini.

Miongoni mwa kauli ya Imam Ali (a.s): **"Hakuna elimu kama kufikiri wala hakuna fahari kuliko kunyeyekea"**.

## SAYYID AFGHANI NA WANAOMKANA MUNGU

Ufafanuzi mzuri wa Aya hii kwa ujumla ni majibu ya Sayyid, Jamaluddin Al-Afghani, kwa wale wanaokana kuweko Mwenyezi Mungu anasema: "Akiulizwa Darwin kuhusu miti iliyoko katika misitu wa India na mimea inayozaliana humo tangu zama za kale sana ambazo historia haijui muda wake, isipokuwa kudhania tu.

Mashina yake yote yako katika uwanja mmoja matawi yake yote yanakwenda kwenye anga moja, Sasa ni kitu gani kinachofanyika mpaka mmoja ukatofautiana na mwingine katika umbile lake, majani yake, kimo chake na ukubwa.

Vile vile maua yake, matunda yake na hata ladha yake? Ni, kitu gani cha nje kilichoathiri mpaka ikapatikana tofauti katika makuzi ya aina moja, maji na hewa ya aina moja? Nadhani hawezi kupata jibu la hayo

Akiulizwa kuhusu hawa samaki wa mto Oural na wa bahari ya Qazwini (Caspian sea) wanashirikiana katika vyakula, lakini wanatofautiana kabisa kimaumbile, je kuna sababu gani ya kutofautiana huku? Sioni kama ataweza kuwa na majibu isipokuwa kushindwa"

**Unaweza kuuliza kuwa**: Darwin anaweza kumjibu Sayyid Afghani kwamba wataalamu wa mimea wanajua sababu ya kutofautiana huku na wanaweza kuifichua kwa kila anayetaka na kupendelea; Kwa hiyo basi, hakuna dharura, katika hali hii, kulazimika kuweko mpangiliaji?

**Jibu**: Tuchukulie kuwa wataalamu wa mimea wanajua sababu ya hilo, lakini ujuzi wao utakuwa na kiwango cha kujua sababu ya karibu ya hilo.

Na kama wakiulizwa sababu ya mbali iliyosababisha hii ya karibu hawatapata isipokuwa moja ya sababu mbili: Ama sadfa au kuweko mpangiliaji mwenye hekima. Sababu ya kwanza itakuwa batili kwa sababuu sadfa haikaririki wala kudumu, Kwa hiyo itabaki sababu ya pili.

Mara kadhaa tumebainisha kuwa ni desturi ya Qur'an kutegemeza matukio yote ya kimaumbile kwenye sababu yake ya kilimwengu.

Hilo ni katika kukitegemeza kitu kwa mtendaji wake wa kwanza, kwa lengo la kukumbusha kuweko Mwenyezi Mungu na kwamba yeye ndiye muumba wa ulimwengu wote pamoja na ardhi yote na mbingu yake.

**Unaweza kusema tena**: Wakana Mungu nao wanaweza kuuliza: Kuna sababu gani ya kuweko mpangiliaji mambo?

**Jibu**: Hakika swali hili sio la msingi kwa sababu kuweko mpangiliaji hakuna sababu na kwamba yeye ndiye msabibishaji sababu. Kuuliza sababu ya kuweko msababishaji ni sawa na kuuliza: Nina ni aliye muumba Mungu baada ya kufaradhia kuwa yeye ni muumba sio muumbwa.

Au kuuliza sababu ya kusadikisha jicho lilichokiona na sikio lilichokisikia na huku tunaamini kuwa hiyo ni hoja mkataa ya kila shaka na kila shubha.

وَإِن تَعْجَبْ فَعَجَبٌ قَوْلُهُمْ أَإِذَا كُنَّا تُرَابًا أَإِنَّا لَفِي خَلْقٍ جَدِيدٍ أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ
وَأُولَـٰئِكَ الْأَغْلَالُ فِي أَعْنَاقِهِمْ وَأُولَـٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٥﴾

5. Na kama ukistaajabu basi cha ajabu ni usemi wao: ‘Ati tutakapokuwa mchanga, kweli tutakuwa katika umbo jipya?’ Hao ndio waliomkufuru Mola wao na hao ndio watakokuwa na minyororo shingoni mwao na hao ndio watu wa motoni, Humo watadumu.

وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ وَقَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِمُ الْمَثُلَاتُ وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ
لِّلنَّاسِ عَلَىٰ ظُلْمِهِمْ وَإِنَّ رَبَّكَ لَشَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٦﴾

6. Wanakuhimiza ulete maovu kabla ya mema, hali ya kuwa imepita kabla yao mifano. Na hakika Mola wako ni mwenye maghufira kwa watu juu ya udhalimu wao. Na hakika Mola wako ni mkali wa kuadhibu.

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِّن رَّبِّهِ إِنَّمَا أَنتَ مُنذِرٌ وَلِكُلِّ قَوْمٍ هَادٍ ﴿٧﴾

7. Na husema wale ambao wamekufuru: ‘Mbona hakuteremshiwa ishara kutoka kwa Mola wake.’ Hakika wewe ni mwunyaji tu. Na kila kaumu ina wa kuwaongoza.

## KWELI TUTAKUA KATIKA UMBO JIPYA?

**Aya 5-7**

### MAANA

Na kama ukistaajabu basi cha ajabu ni usemi wao: ‘Ati tutakapokuwa mchanga, kweli tutakuwa katika umbo jipya?’

Maneno yanaelekezwa kwa Muhammad **(s.a.w.w)** wasemaji ni washirikina waliokana utume wake. Maana ni kuwa ikiwa ewe Muhammad utashangazwa na ibada ya masanamu ya washirikina na kukanusha kwao utume wako, basi la kushangaza zaidi ni kukadhibisha kwao ufufuo.

Kwa sababu wao wanakubali kuwa yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Muumba wa ulimwengu, na mwenye kuweza hilo si anakuwa na uwezo zaidi wa kumrudisha mtu baada ya kufa kwake?

Hao ndio waliomkufuru Mola wao na hao ndio watakokuwa na minyororo shingoni mwao na hao ndio watu wa motoni, Humo watadumu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja neo ‘hao’ mara tatu kuelezea kwa ufasaha zaidi hasira zake na kuchukia kwake. Kauli yake: Hao ndio waliomkufuru Mola wao, inafahamisha kuwa Mwenye kuamini kuwa Mwenyezi Mungu ni muumba wa ulimwengu inamlazimu yeye, kwa hali yoyote, kuamini kuwa yeye ni muweza wa kuwafufua walio makaburini. Atakayepinga hilo atakuwa moja kwa moja amemkufuru Mwenyezi Mungu atake asitake.

Mwenye kuchanganya imani ya Mungu na kushindwa kufufua watu, atakuwa amechanganya mambo mawili yanayopingana. Washirikina wamepinga ufufuo, kwa vile, kulingana na madai yao, Mwenyezi Mungu hawezi; kama inavyojulisha kauli yao “Ati tutakapokuwa…” Kwa hiyo, ilivyo hasa, ni kuwa wao wanampinga Mwenyezi Mungu kwa ndimi zao.

## WANAOAMINI MAADA NA MAISHA BAADA YA MAUTI

Wanaoamini maada wanakana kuweko Mwenyezi Mungu, sana sana wanapinga maisha baada ya mauti. Dalili yao ni moja tu haibadiliki wala haigeuki. Nayo ni kuwa kila linaloweza kuhisiwa na kushuhudiwa inapasa kuliamini na kila lisiloweza kuhisiwa inapasa kulikana na kulipinga.

Kwa hiyo, kwao, hisia ya dhahiri peke yake ndiyo dhahiri na ndiyo batini, ndiyo ya mwanzo na ya mwisho; kama wanavyosema. Vipi wataamini Bustani (Pepo) nao hawajala matunda yake, vipi wakubali kuwa kuna Jahannam na moto wake haujawafikia?

Sisi nasi, kwa upande wetu, tunauliza hivi: Mmepata wapi elimu au imani ya kuwa hisia za dhahiri pekee ndiyo njia ya haki na hali halisi, na kwamba mengineyo ni upuuzi? Mkisema hayo mmeyajua kupitia hisia, tutasema:

Sisi pia tunazo hisia na hatujamuona mwingine zaidi yenu akisema kuwa msiamini isipokuwa hisia. Ikiwa mtasema mmejua hilo kwa njia nyingine isiyokuwa hisia, basi mtakuwa mmejipinga wenye kwa kuamini kisichoshuhudiwa na hisia.

Mnamo mwaka 1962 nilitunga kitabu kuwajibu wanaoamini maada, kwa jina Falsafatul-Mabda' (falsafa ya misingi), Kisha baadae nikasoma mambo mengi kuhusu wanavyoamini wa maada na majibu yao; miongoni mwayo ni:

1. Kwa mujibu wa wanaoamini maada ni lazima kutokuweko tofauti yoyote baina ya mtu aliye na miujiza na vidudu duni vinavyotokana na uchafu kwa vile wote hao ni watoto wa sharia ya sadfa na maumbile pofu yasiyokuwa na mipangilio yoyote .

2. Wataalamu wamepata katika ubongo wa binadamu nyuzi milioni elfu 14 zimefumwa na kupangiliwa vizuri sana kwa namna ambayo wahandisi wakuu wote hawawezi; kiasi ambacho unyuzi mmoja tu ukienda kombo basi mtu hatakuwa na utambuzi au atachanganyikiwa, sawa na umeme ukiharibika moja ya nyaya zake. Hakuna tafsiri ya hayo, kwa mwenye akili, isipokuwa kuweko mpangiliaji mwenye hekima asiyeweza kuonwa kwa jicho, kusikiwa na sikio, kuguswa kwa mkono, kunuswa na pua au kuonjwa kwa ulimi.

Kwa namna yoyote itakavyokuwa sadfa na muujiza, lakini haiwezi kufanya umeme; sikwambii kuunganisha nyuzi milioni elfu 14 zilizopangiliwa, kiufundi na kuwekwa kwenye chombo kimoja kwa idadi ya vichwa na bongo za binadamu wote; tena waweze kuhisi na kutambua.

3. Waamini maada wanasema kuwa ubongo wa binadamu ni sawa na akili ya mashine. Zote mbili zimetokana na vitu vilivyosukwa na kupangwa kuweza kuleta athari.

Mtaalamu wa kifaransa, aitwaye Caussine, aliwajibu kwa kusema: Iwapo gari yangu ya zamani ikianza kutoa sauti mbovu kama mtu aliyepatwa na ugonjwa wa baridi yabisi, inawezekana niseme kuwa gari yangu ina baridi yabisi? Na kabureta inapotatarika wakati ninapokanyaga mafuta, je, itafaa niseme kuwa gari yangu imepatwa na pumu?

Nasi tunaongezea juu ya kauli ya mtaalamu huyu kwa kusema: mpangilio na utaratibu kwenye akili ya mashine umetokana na kitendo cha mtu, hilo halina shaka. Lakini ni nani aliyepangilia na akaweka mfumo kwenye ubongo wa binadamu?

Ikiwa binadamu amevumbua akili ya mashine, je akili hii ya mashine inaweza kuvumbua akili nyingine mfano wake au kitu duni kama pini? Katika kitabu Al-amal wal – Mukh (kazi na ubongo), kilichofasiriwa na Shakri Azir cha Mtaalamu wa Kirusi Yuri Bakhlov, anasema: Wale wanaodhani kuwa kuna uwezekano wa mashine kuchukua nafasi ya akili ya binadamu wamekosea kosa kubwa sana… ubongo wa binadamu unatofautiana kabisa na chombo chochote katika utendaji kazi wake, uwelekevu na ustadi wake usio na kikomo. Ama akili ya mashine ina kikomo - kile alicho kiweka binadamu.
4. Kuna ugunduzi mkubwa wa nyuki kuhusu vifaa vya kupunguza joto (viyoyozi), Kwamba nyuki aligundua kifaa hiki kabla ya binadamu. Joto linapozidi kwenye Masega ya nyuki kundi moja linaondoka kuleta maji kwa kutumia visiku vyao na kuyaweka kwenye tanki. Kikipatikana kiasi cha kutosha husimama kundi jengine kunyunyiza maji na kundi jingine la tatu linatengeneza tiyara ya hewa na maji yanayayuka kwa haraka; kwa myeyuko huo kiwango cha joto kinashuka.
Ni nani aliyempa nyuki akili hii? Ni sadfa? Au kuna nguvu ya hakika inayojitokeza kwenye maumbile na nidhamu yake? Nyuki na sisimizi wana masimulizi ambayo hayana tafsiri wala picha yoyote isipokuwa kuweko mpangiliaji mwenye hekima.
Turudie kauli ya Voltare ambaye huko nyuma tumewahi kumdokeza mara kwa mara, anasema: Mbele ya fikra ya kuweko Mwenyezi Mungu kuna vikwazo lakini katika fikra ya kupinga kuna upumbavu …Namna hii binadamu anahama kutoka kwenye shaka hadi shaka nyingine mpaka anafikia kusadikisha kuwa kuweko Mwenyezi Mungu ndio jambo la karibu zaidi na kwaye zinafungamana kanuni za dharura ya ulimwengu.

Wanakuhimiza ulete maovu kabla ya mema, hali ya kuwa imepita kabla yao mifano.

Makusudio ya maovu hapa ni adhabu na mema ni thawabu na mifano ni mifano ya adhabu.
Mtume **(s.a.w.w)** aliwalingania washirikina kwenye Tawhid, na akawaahidi thawabu wakiitikia mwito na kuwapa kiaga cha adhabu wakitoitikia.
Wao badala ya kuitikia mwito na kutubia shirk, waliendelea kuasi na wakajifanya jeuri, huku wakisema: Harakisha unayotuahidi ukiwa ni mkweli waliyasema haya bila ya kuzingatia umma zilizopita ziliyoyapata baada ya kuwaasi Mitume wao.
Kwa hakika mghafala huu wa kutopata funzo, hauhusiki na washirikina peke yao, Watu wengi hawazingatii yaliyowapata wenzao wala hawapati funzo; hata wenyewe wanaotoa mawaidha. Siri ya hilo ni kuwa wengi wanashindwa na tamaa na masilahi sio kwa akili wala dini.
Kuna mfano maarufu wa kimagharibi unaosema: Mwanamke kumwongoza mwana- mume kwa tumbo si kwa akili.

Na hakika Mola wako ni mwenye maghufira kwa watu juu ya udhalimu wao. Na hakika Mola wako ni mkali wa kuadhibu.

Makusudio ya maghufira hapa ni kupuuza na kutoharakisha adhabu kwa dhambi. Hilo linafahamika kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu: "Na hakika Mola wako ni mkali wa kuadhibu. Kwa sababu maghufira hayawi pamoja na adhabu ya akhera sikwambii iliyo kali.

Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) hamwadhibu mja mara tu anapofanya dhambi isipokuwa anamngojea na kumfungulia mlango wa toba ili aweze kurejea kutokana na upotevu wake, aweze kupata thawabu kwenye uwongofu wake.

Kuna tafsiri nyingine isemayo kuwa Mwenyezi Mungu husamehe dhambi za walioasi katika waislamu na anakuwa mkali wa kuadhibu kwa makafiri. Lakini tafsiri hii iko kinyume na dhahiri, tena inahimiza uasi. Usawa hasa ni yale tuliyoyasema kuongezea Aya nyingine isemayo:

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّـهُ النَّاسَ بِظُلْمِهِم مَّا تَرَكَ عَلَيْهَا مِن دَابَّةٍ ﴿٦١﴾

"Lau Mwenyezi Mungu angeliwachukulia watu kwa sababu ya dhulma yao, asingelimwacha hata mnyama mmoja juu yake" (16:61).

Na husema wale ambao wamekufuru: 'Mbona hakuteremshiwa ishara kutoka kwa Mola wake?' Hakika wewe ni mwonyaji tu. Na kila kaumu ina wa kuwaongoza.

Imepita mifano yake katika Juz.7 (6:37), Na tumefafanua kuhusu muujiza wa Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** na matakwa ya wenye kiburi katika Juz 1 (2:118).

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

اللَّـهُ يَعْلَمُ مَا تَحْمِلُ كُلُّ أُنثَىٰ وَمَا تَغِيضُ الْأَرْحَامُ وَمَا تَزْدَادُ وَكُلُّ شَيْءٍ عِندَهُ بِمِقْدَارٍ ﴿٨﴾

8. Mwenyezi Mungu anajua mimba aibebayo kila mwanamke na kinachopungua na kuzidi matumboni. Na kila kitu kwake ni kwa kipimo.

عَالِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْكَبِيرُ الْمُتَعَالِ ﴿٩﴾

9. Ni mjuzi wa ghaibu na yanayoshuhudiwa, mkubwa aliyetukuka.

سَوَاءٌ مِّنكُم مَّنْ أَسَرَّ الْقَوْلَ وَمَن جَهَرَ بِهِ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ ﴿١٠﴾

10. Ni sawa anayeficha kauli kati yenu na anayeidhihirisha na anayejibanza usiku na anayetembea mchana.

لَهُ مُعَقِّبَاتٌ مِّن بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ يَحْفَظُونَهُ مِنْ أَمْرِ اللَّـهِ إِنَّ اللَّـهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ
يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ وَإِذَا أَرَادَ اللَّـهُ بِقَوْمٍ سُوءًا فَلَا مَرَدَّ لَهُ وَمَا لَهُم مِّن دُونِهِ مِن وَالٍ ﴿١١﴾

11. Ana yanayomfuatilia mbele yake na nyuma yake yanamhifadhi kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu habadilishi yaliyoko kwa watu mpaka wabadilishe yaliyo katika nafsi zao, Mwenyezi Mungu akiwatakia watu uovu hakuna cha kumzuia wala hawana mlinzi yeyote badala yake.

## MWENYEZI MUNGU ALIJUA

**Aya 8-11**

### MAANA

Mwenyezi Mungu anajua mimba aibebayo kila mwanamke na kinachopungua na kuzidi matumboni.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Aya iliyotangulia ametaja kuwa washirikina walimtaka Muhammad **(s.a.w.w)** muujiza zaidi unao fahamisha kuhusu utume wake.

Katika Aya hii anasema kuwa Yeye anajua kilicho katika matumbo ya uzazi awe ni mtoto wa kiume au wa kike mmoja au zaidi upungufu au ukamilifu. Basi mwenye kujua yote hayo, anajua kwamba kutaka muujiza zaidi ni inadi na kiburi tu, si kutaka kuongoka.

Wameafikiana Waislamu wote kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu anajua viumbe vyote vikubwa kwa vidogo; Kwa sababu kila kiumbe kinajulikana mbele yake. Kwa ibara ya Muhyiddin bin Al-arabi:

"Hakika hakuna chochote kilichopo ulimwenguni ila kina wajihi maalum kwa yule aliyekifanya kiweko"

Kisha wanafalsafa wakatofautiana na ulamaa wa elimu ya Mwenyezi Mungu ambao wanasema kuwa Mwenyezi Mungu anajua mafungu yote; kama vile aina ya wanyama, mimea na vitu vingine kwa ujuzi wa moja kwa moja bila ya kuweko kitu chochote kati yake. Wanafalsafa nao wanasema anajua kupitia sababu zake na kinachozalikana nacho.

Sisi hatuoni faida yoyote ya tofauti hii; Kwa sababu ni juu ya Mwislamu kuamini kuwa elimu ya Mwenyezi Mungu imeenea kwenye kila kitu,

kiujumla na kimafungu; hata mapigo ya moyo na pepesi za akilini. Ama kuamini elimu yake kwa namna hii au ile si chochote katika dini.

Kuna hadithi zinazokataa kuifikiria dhati ya Mwenyezi Mungu na kuamuru kufikiria kuumba kwake na utengenezaji wake.

Na kila kitu kwake ni kwa kipimo haumbi kimchezomchezo na bila ya misingi; bali kila kitu kina kiwango chake na nidhamu yake katika kipimo cha mafungu, mihimili athari na mahusiano yake. Vile vile kinamna kitakavyokuwa na sura, mahali, wakati, sababu na desturi yake. Yote hayo ni kulingana hekima na masilaha.

Analoweza binadamu ni kuona, kuchunguza, kupima na kukisia; Kwa hivyo anaweza akapatia au kukosea. Kwa sababu elimu ya mtu inatokana na kutafuta, kwa hiyo inahitaji msababishaji.

Mara nyingi sana kuna yanayodhaniwa kuwa ni sababu ya jambo fulani, kumbe sivyo kabisa. Ama elimu Yake Mwenyezi Mungu Mtukufu ni ya kidhati na hali halisi.

Ni mjuzi wa ghaibu na yanayoshuhudiwa, Mkubwa aliyetukuka.

Makusudio ya ukubwa sio ukubwa wa umbo na utukufu sio mahali panapohisiwa, bali hayo ni mafumbo ya utukufu wa dhati Yake na sifa Zake. Mjuzi wa ghaibuu ni kujua yale tusiyoyajua, yaliyo ughaibuuni kutokana na elimu yetu na yanayoshuhudiwa ni yale tunayoyaona na kuyashuhudia.

Hakika ulimwengu umejaa viumbe jinsi na aina mbali mbali za hali ya juu na za chini. Kuanzia vidudu hadi binadamu na Malaika, madini hadi mimea na wanyama, mpaka kufikia maji na hewa na mengineyo yasiyokuwa na ukomo.

Mtume anaweza kujua upande moja tu wa baadhi ya vitu vya ulimwengu lakini ujuzi wake, kadiri utakavyokuwa si chochote kulinganisha na asiyoyajua, Mengi yanayofichuka yanaficha siri nyingi.

Wala hajui yaliyoko ulimwenguni isipokuwa muumba wa ulimwengu huo tu. Yeye peke yake ndiye ambaye, kwake, siri na dhahiri ni sawa tu.

وَمَا أُوتِيتُم مِّنَ الْعِلْمِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٨٥﴾

“Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu.” (17:85)

Ni sawa anayeficha kauli kati yenu na anayeidhihirisha na anayejibanza usiku na anayetembea mchana.

Umepita mfano wake katika Juz. 7(6:3) na Juz.10 (9:78).

Ana yanayomfuatilia mbele yake na nyuma yake yanamhifadhi kwa amri ya Mwenyezi Mungu.

Anayefuatiliwa ni binadamu na yanayomfuatilia ni fumbo la hisia na silika zake ambazo zina athari katika kuwa kwake na kuhifadhi utu wake. Hayo yametokana na riwaya iliyopokewa kutoka kwa Imam Jafar As-Sadiq (a.s.).

Wafasiri wamesema kuwa makusudio ya yanayomfuatilia ni Malaika, na tafsiri nyingine zinasema kuwa Mwenyezi Mungu hupeleka Malaika kumi mchana kumlinda binadamu na jua linapozama wanaondoka hao na kuja wengine kumi wa zamu ya usiku; na kwamba kila mtu anakuwa hivyo. Iblisi naye zamu yake ya kuwapoteza watu ni mchana na usiku ni zamu ya watoto wake.

Mbali ya kuwa maelezo hayo yako mbali na tamko linavyofahamisha, lakini akili pia inayakataa. Tuonavyo sisi ni kuwa makusudio ya yanayofuatilia ni

hisia zinazomhifadhi mtu; kama tulivyotangulia kueleza. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemuumba mtu, akampa masikio, macho, utambuzi na mengineyo, ili yamlinde na kumchunga.

Maana haya, ingawaje yako mbali na tamko la Aya, lakini yanaafikiana na hali halisi wala hayapingani na mfumo wa Aya. Ni kwa utambuzi, mtu ana mapambano kati ya manufaa na madhara, ni kwa macho anaweza kufuata njia iliyosalama na ni kwa kupenda dhati ndio atajihifadhi na maangamizi.

## HABADILISHI MPAKA WAJIBADILISHE

Hakika Mwenyezi Mungu habadilishi yaliyoko kwa watu mpaka wabadilishe yaliyo katika nafsi zao.

Wafasiri wamesema: Aya hii inafahamisha kuwa watu wanaoishi katika neema ya mali, amani na jaha, Mwenyezi Mungu hawezi kuwaondolea madamu wanaswali na kutoa Zaka, lakini wakiasi basi anawaondolea neema hii.

Ama sisi tutafasiri Aya hii katika mwelekeo wa mafunzo ya kiislamu na maana yanayochukuliwa na tamko la Aya.

Katika mafunzo ya Uislamu, yaliyo muhimu ni wajibu wa jihadi ya nafsi ikiwa inapondokea kwenye haramu na maangamizi au kuridhia udhalili na ufukara. Vile vile jihadi ya nafsi na mali katika njia ya uadilifu na kujikomboa kutokana na dhulma na utumwa.

Hakuna mwenye shaka kwamba mwenye kupinga udhalili, akapuuza uhai na kukataa kila kitu isipokuwa heshima yake au mauti, basi Mwenyezi Mungu atamshika mkono kumpeleka kwenye matakwa na malengo anayoyakusudia.

Na mwenye kubweteka kwenye raha na uvivu, vyovyote itakavyokuwa Mwenyezi Mungu atamdhalilisha na kumwachia udhaifu wake wala hatamwangalia au kumsikiliza; hata kama ataijaza dunia kwa unyenyekevu, vilio, na dua.

Kwa hivyo basi inatufunukia kuwa maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: “ Hakika Mwenyezi Mungu habadilishi yaliyoko kwa watu mpaka wabadilishe yaliyo katika nafsi zao,” ni kuwa Yeye ambaye imetukuka heshima yake, atambakisha mtu kwenye udhalili ikiwa amekaa tu bila ya kujikwamua na kuipinga batili.

Ndio! Mwenyezi Mungu hawezi kutuondolea ufukara mpaka tuamini kuwa ufukara umetoka ardhini sio mbinguni, na mpaka tupigane jihadi dhidi ya ukandamizaji na unyonyaji na mpaka tujenge viwanda na tulime mashamba.

Mwenyezi Mungu hatubadilishii ujinga mpaka tujenge mashule na vyuo vikuu, Mwenyezi Mungu hatubadilishii utumwa mpaka tulete mapinduzi dhidi ya dhulma. Na Mwenyezi Mungu hatatubadilishia matatizo mbalimbali mpaka tuzisafishe nyoyo zetu na tuondoe pingamizi na vikwazo vilivyo baina yetu.

Mwenyezi Mungu akiwatakia watu uovu hakuna cha kumzuia wala hawana mlinzi yeyote badala yake.

Makusudio ya uovu hapa ni adhabu. Wakati wowote Mwenyezi Mungu anapomtakia mtu au kundi jambo lolote, basi hakuna wa kuzuwiya, na Yeye ni mwadilifu, hamtakii isipokuwa analostahiki. Ulinzi ni katika sifa za Mwenyezi Mungu kwa sababu yeye analinda mambo na huyasimamia kwa mipangilio iliyo kamili.

هُوَ الَّذِي يُرِيكُمُ الْبَرْقَ خَوْفًا وَطَمَعًا وَيُنشِئُ السَّحَابَ الثِّقَالَ ﴿١٢﴾

12. Yeye ndiye anayewaonyesha umeme kwa hofu na tamaa, na huyaleta mawingu mazito.

وَيُسَبِّحُ الرَّعْدُ بِحَمْدِهِ وَالْمَلَائِكَةُ مِنْ خِيفَتِهِ وَيُرْسِلُ الصَّوَاعِقَ فَيُصِيبُ بِهَا مَن يَشَاءُ وَهُمْ يُجَادِلُونَ فِي اللَّـهِ وَهُوَ شَدِيدُ الْمِحَالِ ﴿١٣﴾

13. Na radi inamtakasa kwa kumsifu na Malaika pia kwa kumhofia. Naye hupeleka mapigo ya radi yakampata amtakaye, Nao wanabishana juu ya Mwenyezi Mungu; na yeye ni mkali wa hila.

لَهُ دَعْوَةُ الْحَقِّ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِهِ لَا يَسْتَجِيبُونَ لَهُم بِشَيْءٍ إِلَّا كَبَاسِطِ كَفَّيْهِ إِلَى الْمَاءِ لِيَبْلُغَ فَاهُ وَمَا هُوَ بِبَالِغِهِ وَمَا دُعَاءُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ﴿١٤﴾

14. Kwake ndio maombi ya haki, Na hao wanaoomba badala yake hawajibiwi chochote isipokuwa kama yule anyooshaye viganja vyake kwenye maji ili yafikie kinywani mwake, lakini hayafiki. Na maombi ya makafiri hayako ila kwenye upotevu.

وَلِلَّـهِ يَسْجُدُ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَظِلَالُهُم بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿١٥﴾

15. Na vilivyomo mbinguni na ardhini vinamsujudia Mwenyezi Mungu vitake visitake na vivuli vyao asubuhi na jioni.

## ANAYEWAONYESHA UMEME

**Aya 12-15**

### MAANA

Yeye ndiye anayewaonyesha umeme kwa hofu na tamaa na huyaleta mawingu mazito.

Umeme unaokusudiwa hapa ni ule wa radi.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameumba ulimengu; ulimwengu nao una mambo yake na desturi zenye athari; ukiwemo umeme radi mawingu, vimondo na mengineyo anayoweza kuyashuhudia mtaalamu na mtu wa kawaida na pia muumin na mlahidi. Wala hajui hakika yake na umbile lake isipokuwa wataalamu wahusika.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameyategemeza kwake moja kwa moja, wala hakuyategemeza kwenye sababu za ulimwengu, kwa upande wa kutegemeza kitu kwenye sababu yake ya kwanza.

Lengo ni kukumbusha kwamba Yeye ndiye sababu ya sababu zote, na kwake Yeye pekee yanarejea mambo yote.

Kauli yake kwa hofu na tamaa ni kuashiria umeme, mara nyingine unakua ni kutoa onyo la kupiga radi ya kimondo na mara nyingine ni dalili njema ya mvua. Kwa hiyo mtu anapata hofu na furaha kwenye kitu hicho hicho kimoja.

Na radi inamtakasa kwa kumsifu na Malaika pia kwa kumhofia.

Makusudio ya kumtakasa (tasbih) ya radi ni kufahamisha uweza na cheo chake Mwenyezi Mungu; sawa na maandishi yanavyomfahamisha mwandishi na jengo na mjengaji wake.

Hapa ndio tunapata tafsiri ya kauli yake Mwenyezi Mungu:

وَإِن مِّن شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ ﴿٤٤﴾

Na hapana kitu chochote ila kinamtakasa Mwenyezi Mungu kwa kumsifu" (17:44).
Yaani kinamfahamisha, Kwa maneno mengine kila kitendo kizuri kilichofanywa kwa mpangilio mzuri kinamfahamisha aliyekifanya jinsi alivyo na kumsifia, kwa lugha ya hali.
Hakuna mwenye shaka kwamba kila kilichomo ulimwenguni kimefanywa kwa mpangilio mzuri usio na kikomo. Kwa hivyo kinafahamisha jinsi alivyo muumba wake na kumsifia.
Kauli ya kushangaza ni ile ya baadhi ya masufi wanaosema kuwa radi ni kukoroma kwa Malaika na umeme ni mapigo ya nyoyo zao.

Naye hupeleka mapigo ya radi yakampata amtakaye.

**Unaweza kuuliza**: mapigo ya radi mitetemeko ni mambo ya kidhahiri ya kimaumbile na desturi yake. Ni wazi kwamba maumbile ni pofu hayachagui baina ya mwema na muovu, shari yake na heri yake inawaenea wote bila kutofautisha, lakini kauli Yake Mwenyezi Mungu Mtukufu 'yakampata amtakaye' inatambulisha kutofautisha?
**Jibu**: Makusudio ya mapigo ya radi hapa ni adhabu ya radi aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa wale waliong'ang'ania shirki wakawafanyia inadi Mitume wao; kama vile kaumu ya A'd na Thamud, kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿فَإِنْ أَعْرَضُوا فَقُلْ أَنذَرْتُكُمْ صَاعِقَةً مِّثْلَ صَاعِقَةِ عَادٍ وَثَمُودَ ﴿١٣﴾

"Kama wakikataa waambie nawahadharisha na pigo la radi mfano wa pigo la radi la A'd na Thamud." (41:13).

﴿فَقَالُوا أَرِنَا اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْهُمُ الصَّاعِقَةُ بِظُلْمِهِمْ ﴿١٥٣﴾

"Walisema: 'Tuonyeshe Mwenyezi Mungu wazi wazi.'Wakapigwa na radi kwa sababu ya dhulma yao." Juz.6 (4:153).
Imetangulia mara nyingi kuelezwa kwamba Qur'an inajitamkia yenyewe kwa yenyewe na baadhi yake ina shuhudia baadhi nyingine.

Nao wanabishana juu ya Mwenyezi Mungu.

Wanaobishana ni washirikina. Maana ni kuwa hawa wanabishana katika uweza wa Mwenyezi Mungu na utukufu wake, Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** na Utume wake na pia ufufuo na uwezekano wake, pamoja na kudhihiri dalili za uweza wa Mwenyezi Mungu, Muujiza wazi wa Utume wa Muhammad **(s.a.w.w)** na kushuka adhabu kwa wapinzani wa ufufuo na hisabu.

Na yeye ni mkali wa hila.

Yaani ni mwenye nguvu sana za kuwakamata maadui zake na maadui wa mawalii wake. Kwa ufupi ni kuwa washirikina wanabishana kwa maneno na Mwenyezi Mungu anakamata kwa vitendo.

﴿إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١٢﴾

"Hakika mashiko ya Mola wako ni makali." (85:12).

Kwake ndio maombi ya haki, Na hao wanaoomba badala yake hawajibiwi chochote isipokuwa kama yule anyooshaye viganja vyake kwenye maji ili yafikie kinywani mwake, lakini hayafiki. Na maombi ya makafiri hayako ila kwenye upotevu.

Mwenyezi Mungu ndiye haki, Mwenye kutenda kwa ajili yake na akamtegemea yeye, basi atamlipa thawabu na mwenye kuasi na akafanya jeuri atastahiki adhabu; mwenye kuomba mwenginewe, kama masanamu ,atakuwa ameomba batili isiyodhuru wala kunufaisha.

Na maombi ya makafiri hayako ila kwenye upotovu.

Sawa na mwenye kiu akidhani moshi ni mawingu na mangati kuwa ni maji. Ananyoosha viganja vyake ili avijaze maji na anafungua kinywa chake ili aburudike, mara hamna kitu.

Na vilivyomo mbingu ni na ardhini vinamsujudia Mwenyezi Mungu vitake visitake.

Umepita mfano wake katika Juz.3(3:83).

Na vivuli vyao asubuhi na jioni.

Kivuli ni akisi ya mwili ambao unakuwa nacho, ukitingishika nacho hutingishika; sawa na sura ya kitu kwenye kioo. Mwenyezi Mungu amehusisha kutaja asubuhi na jioni, kwa sababu kivuli kinarefuka katika nyakati mbili hizi.

Maana ni kuwa vilivyomo mbinguni na ardhini na pia vivuli vyao vinamsujudia. Unaweza kuuliza: Kivuli si chochote isipokuwa kinafuata na kinapigiwa mfano wa kutokuwepo kitu. Vipi Mwenyezi Mungu amejaalia ni kitu na akaunganisha na mwenye kivuli hicho?

Sufi wamejibu kuwa vilivyomo mbinguni na ardhini ni viwiliwili na vivuli ni roho.

Tunavyofahamu ni kuwa kivuli ni fumbo la kuenea kwenye kila kitu na kwamba kila kilichoko ulimwenguni kinamsujudia Mwenyezi Mungu; yaani kinakubali kuweko kwake, hata kivuli kingelimsujudia kama kingelikuwa ni kitu.

قُلْ مَن رَّبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ قُلِ اللَّـهُ قُلْ أَفَاتَّخَذْتُم مِّن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ لَا يَمْلِكُونَ لِأَنفُسِهِ مْ
نَفْعًا وَلَا ضَرًّا قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ أَمْ هَلْ تَسْتَوِي الظُّلُمَاتُ وَالنُّورُ أَمْ جَعَلُ وا لِلَّـهِ
شُرَكَاءَ خَلَقُوا كَخَلْقِهِ فَتَشَابَهَ الْخَلْقُ عَلَيْهِمْ قُلِ اللَّـهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿١٦﴾

16. Sema: Ni nani Mola wa mbingu na ardhi? Sema, ni Mwenyezi Mungu. Sema: Je, mnawafanya wengine badala yake kuwa ni walinzi na hawajifai wenyewe kwa nafuu wala dhara? Sema: Je, anaweza kuwa sawa kipofu na aonaye? Au je, huwa sawa giza na nuru? Au wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika, walioumba kama kuumba kwake kwa hiyo kuumba kukashabihiana kwao? Sema: Mwenyezi Mungu ndiye muumba wa kila kitu na yeye ni mmoja, Mwenye kushinda.

## KIPOFU NA MWENYE KUONA

**Aya 16**

### MAANA

Sema: Ni nani Mola wa mbingu na ardhi?

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja kuwa kila kilichomo ulimwenguni kinanyenyekea uweza wake, anawarudia washirikina na kuwauliza kupitia mdomoni mwa Mtume wake Mtukufu, kuwa ni nani aliyeumba ulimwengu ikiwemo ardhi yake na mbingu yake?

Kwa kuwa swali liko pamoja na jawabu lake; na wala aliyeulizwa hawezi kupinga, alimwamrisha Mtume wake awajibu: Sema: ni Mwenyezi Mungu.

Sema: Je, mnawafanya wengine badala yake kuwa ni walinzi na hawajifai wenyewe kwa nafuu wala dhara?

Mara nyingine, tena kwa kusisitiza hoja, Mwenyezi Mungu anamwamrisha Muhammad awaambie washirikina kuwa nyinyi mnaabudu mawe ambayo yenyewe hayajiwezi kujikinga na madhara wala kuleta manufaaa, je yataweza kumfaa mwingine?

Aya hii si majibu ya washirikina pekee, bali pia ni majibu ya wale wasemao kuwa akili za watu zinajitosha, hazihitajii kupelekewa mitume na kuteremshwa vitabu kutoka mbinguni. Waabudu mawe walikuwa na wanaendelea kuwa wanajiona ni wenye akili na pia watu wangine wanawaona hivyo.

Sema: Je, anaweza kuwa sawa kipofu na aonaye?

Makusudio ya kipofu ni kafiri. Kwa sababu hakuweza kutofautisha baina ya yule asiyejiweza, na mwenye kumiliki dhara na manufaa? Makusudio ya mwenye kuona ni mumin ambaye anatofautisha kati ya wawili hao (asiyejiweza na mwenye uwezo).

Au je, huwa sawa giza na nuru?

Giza ni fumbo la kufuru na nuru ni fumbo la imani. Mwenyezi Mungu anasema:

الر ۚ كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ﴿١﴾

“Hiki ni Kitabu tulichokiteremsha kwako ili uwatoe watu gizani uwapeleke kwenye nuru” (14:1).

Au wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika, walioumba kama kuumba kwake kwa hiyo kuumba kukashabihiana kwao?

Hii ni kuwarudi washirikina. Ufupisho wake ni kuwa mawe ambayo wanayaabudu hayaumbi chochote; kama aumbavyo Mwenyezi Mungu. Sasa wamethubutu vipi kusema kuwa Mungu anaumba na masanamu yanaumba.

Ikiwa Mwenyezi Mungu anastahiki Uumbaji, basi vile vile atastahiki Uungu na ibada. Ufafanuzi ni kama ifuatavyo:

## AKILI ZA WATU HAZIWATOSHELEZI

Maarifa ya mtu yanagawanyika kwenye mafungu mawili: Maarifa ya kiumbile ya kidhati na maarifa ya kinadharia ya kutafuta. Ya kimaumbile hayahitaji bidii wala juhudi, bali yanapatikana kiasi cha kuleta picha tu kichwani; kama kujua kwamba nuru sio giza, kuona si upofu, urefu sio ufupi, jiwe limeumbwa na haliwezi kuumba. Katika maarifa haya anashiri kimjuzi na asiyekuwa mjuzi, na mwenye kukosea hana udhuru wowote[1].

Ama maarifa ya kinadharia ya kutafuta hayapatikani kwa kuleta picha, bali inahitajika kuyafanyia kazi, juhudi na bidii; kama vile kujua kuwa maji yameshikana au yameachana? Na kujua mardhi haya yanaambukiza au la.

1. Baadhi wametofautisha baina ya elimu na maarifa, kwamba elimu inafunga- mana na mambo yote ya kijumla na maarifa yanafungamana na mafungu fulani. Lakini sisi hatuoni tofauti yoyote kati yake, Mwenyezi (s.w.t) anasema: "Kila kabila ikajua mahali pake pa kunywea." Juz.1 (2:60). Ametumia neno elimu - ikajua, na wawala hakusema ikapata maarifa. Na inajulikana kuwa kunywa kwa kila kabila kulikua mahsus sio kiujumla.

Kadhia hii huitwa 'nadharia' ambayo inatofautiana kulingana na maarifa na vipawa vya wenye nadharia hizo. kukosea katika nadharia kunasame- hewa kukiwa kumetokea baada ya bidii na juhudi. Kwa sababu kupatia katika kila kitu ni jambo zito.

Masanamu waliyoyaabudu washirikina hayana mshabaha wowote na uungu kwa njia yoyote ile ya mbali au ya karibu, kuweza kumfanya mtu aingie shaka au aone uwezekano wa kuwa ni mshirika wa Mwenyezi Mungu katika kuumba kwake.

Itakuwaje yakiwa hayo yenyewe yanakojolewa na mbwa na vicheche? Kuyaabudu ni upumbavu zaidi kuliko kusema kuwa giza ni nuru au kipofu anaona.

**Unaweza kuuliza**: Ni kweli kwamba kuna aina ya maarifa ambayo ni maumbile na kwamba kuukana uungu wa mawe ni mambo ya kimsingi yaliyo wazi yasiyohitaji nadharia, lakini washirikina pamoja na akili yao ya kimaumbile wameweza kuyaabudu, wakiwa ni wenye akili timamu. Je, ni kwa nini?

**Jibu**: Baadhi yao waliabudu kijujuu tu kwa sababu ya chumo na masilahi fulani, wengine waliabudu kwa kuiga na kurithi. Ilivyo ni kuwa akili inadhoofika na kurudi nyuma katika kuigiza au mazoweya, hasa muda ukiwa mrefu na kurithiwa na vizazi baada ya vizazi vingine.

Ndio maana ikawa dini iliyo salimika ni dharura na lazima kwa binadamu kadiri atakavyokuwa na akili na elimu. Kuna wengi sana waliozowea mifu- mo ya elimu na njia zake za undani, hivi sasa, wanaamini mambo mengi ya upotevu. Gustave Labon, anasema katika kitabu Al-arau wal-mutaqada (Rai na itikadi).

"Hakika wataalamu wanatokewa na mambo ya kijinga sawa na wanavyotokewa wasiojua chochote. Ni mara chache sana mtaalamu kusalimika na ujinga katika mambo yasiyokuwa fani yake.

Kwa maelezo haya ndio tunapata sababu ya wataalamu bora zaidi kuaamini mambo ya kipumbavu sana!! Kisha akatoa mifano mingi sana ya hilo; miongoni mwa mifano hiyo ni: kulikuwa na mtaalamu mmoja mkubwa katika zama zake alikuwa hawezi kutoka nyumbani kwake mpaka afunge kamba shingoni ya kumkinga na dege na uchawi.

Sema: Mwenyezi Mungu ndiye muumba wa kila kitu na yeye ni mmoja, Mwenye kushinda.

Ni mmoja katika dhati yake, sifa zake, na kuumba kwake. Mwenye kumshinda kila mwenye inadi na mwenye kuasi hukumu miongoni mwa hukumu zake.

Katika Juz.5 (4:48) Tumetaja dalili za umoja wa muumba. Hapa tutaunganisha na maelezo yaliyo katika Kitab Difau anil- Islam (kuutetea uislam) kilichoandikwa na Laura Fisheva Gallery na kutarjumiwa na Ustadh Munir Baalbaki.

Anasema: Mtume mwarabu alitoa mwito wa itikadi ya umoja wa Mungu (Tawhid) akapata upinzani wa wasio na mtazamo ambao ulimuongoza mtu kwenye shirk. Muhammad alitoa mwito wa kusoma kitabu cha maisha na kufikiria kwenye ulimwengu na desturi yake akiwa anaamini kuwa kila mwenye akili hana budi mwisho kuamini Mungu mmoja.

7

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

أَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَسَالَتْ أَوْدِيَةٌ بِقَدَرِهَا فَاحْتَمَلَ السَّيْلُ زَبَدًا رَّابِيًا وَمِمَّا يُوقِدُونَ عَلَيْهِ فِي
النَّارِ ابْتِغَاءَ حِلْيَةٍ أَوْ مَتَاعٍ زَبَدٌ مِّثْلُهُ كَذَٰلِكَ يَضْرِبُ اللَّـهُ الْحَقَّ وَالْبَاطِلَ فَأَمَّا الزَّبَدُ فَيَذْهَبُ جُفَاءً
وَأَمَّا مَا يَنفَعُ النَّاسَ فَيَمْكُثُ فِي الْأَرْضِ كَذَٰلِكَ يَضْرِبُ اللَّـهُ الْأَمْثَالَ ﴿١٧﴾

17. Ameteremsha maji kutoka mbinguni na mabonde yakamiminika maji kwa kadiri yake na mvo ukachukua mapovu yaliyokusanyika juu yake. Na katika vile wanavyoyeyusha katika moto kwa kutaka mapambo au vyombo vingine hutokea povu mfano wake. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyopiga mfano wa haki na batili, Ama povu linakwenda bure; ama kinachowafaa watu hukaa kwenye ardhi, Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyopiga mifano.

لِلَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمُ الْحُسْنَىٰ وَالَّذِينَ لَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُ لَوْ أَنَّ لَهُم مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ
مَعَهُ لَافْتَدَوْا بِهِ أُولَـٰئِكَ لَهُمْ سُوءُ الْحِسَابِ وَمَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿١٨﴾

18. Waliomwitikia Mola wao watapata wema na wasiomwitikia, hata wange-likuwa na vilivyomo ardhini vyote na mfano wake, hakika wangelivitoa kujikombolea. Hao wana hisabu mbaya kabisa na makao yao ni Jahannam, na hapo ni mahali pabaya mno.

## POVU HALIDUMU

**Aya 17-18**

### MAANA

Katika Aya iliyotangulia Mwenyezi Mungu (s.w.t) amefananisha baina ya mumin na kafir, akapiga mifano miwili: Kwanza, baina ya kipofu na mwenye kuona - kumfananisha kafiri na upofu na mumin na kuona. Pili, baina ya giza na nuru - kumfananisha kafiri na giza na mumin na nuru.

Katika Aya tuliyo nayo hivi sasa, amefananisha haki na batili akaleta mifano miwili vile vile: Kwanza, baina ya maji yanayokaa ardhini na kuwapatia watu heri na uhai. Pili, mapovu ambayo yanashuka kwenye maji kisha yanachukuliwa na mumbu na kwenda na upepo. Amefananisha haki na maji yenye kunufaisha, na batili akifananisha na mapovu yasiyokaa. Haya ndiyo aliyoyakusudia Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliposema:

Ameteremsha maji kutoka mbinguni na mabonde yakamiminika maji kwa kadiri yake na mvo ukachukua mapovu yaliyokusanyika juu yake.

Makusudio ya kadiri yake ni kwamba kila bonde linachukua maji ya mvua kwa kiasi chake cha upana na kina yanayozidi yanaminika kwengine.

Ama mfano mwingine wa haki na batili alioufananisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) ni madini yanayoyeyushwa motoni ili yatengenezwe vipambo kama dhahabu na fedha au vifaa kama chuma risasi na shaba na povu linazimika kwenye madini yaliyoyeshwa ambayo yanapotea; kama yanavy- opotea mapovu yanayochukuliwa na mvo. Kwa hiyo haki ni kama myeyuko wa madini ulio na manufaa na batili ni povu linalotokana na myeyuko ambalo halina manufaa. Hiyo ndiyo maana ya kauli yake:

Na katika vile wanavyoyeyusha katika moto kwa kutaka mapambo au vyombo vingine hutokea povu mfano wake.

Yaani kwenye madini pia hutokea povu lisilokuwa na manufaa sawa na povu la mvo.

Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyopiga mfano wa haki na batili.

Yaani Mwenyezi Mungu analeta mfano na picha ya haki kwa ubainifu katika picha ya maji na madini ambayo hupatiwa manufaa na batili katika picha ya povu lisilokuwa na manufaa.

Ama povu ambalo linachukuliwa na mvo au kuzimika kwenye madini yanapoyeyeshwa linakwenda bure bila ya manufaa.

Ama kinachowafaa watu hukaa kwenye ardhi nayo ni maji na madini hukaa ardhini kwa ajili ya heri na uhai

Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyopiga mifano ya haki na batili na mingineyo.

Mara nyingi maana yanakuwa magumu kufahamika na watu wengi. Mifano ni nyenzo nzuri ya kufafanua na kuweka wazi, mbali ya kuwa mfano unaongezea uzuri wa ubainifu.

Mwenyezi Mungu amepiga mifano mingi katika Aya nyingi za ubainifu; kama vile ukafiri na imani kuupigia mfano wa giza na nuru au upofu na uoni. Vile vile mfano wa haki, katika Aya hii, kwa maji na madini, na wa batili kuwa povu.

Aya hii inaleta picha halisi ya Uislamu, Au kwa ufasaha zaidi, inaleta picha ya Mwislamu wa kweli, kuwa ni yule ambye watu wananufaika naye kwa manufaa yenye kudumu; sawa na yule aliyeihuisha ardhi baada ya kufa; na kama madini magumu yanayojengewa viwanda na viwanda vinazalisha zana na vifaa mbali mbali na kuleta maendeleo, vya mbali vikaletwa karibu. Kukawa na majeshi, wakatembea angani, ardhi ikalimwa na dunia ikajaa heri, amani na raha.

Natija ya hayo ni kwamba kila mwenye kunufaisha, akaleta utengeneo na katenda kwa ajili ya maisha ya binadamu mwenzake awe na uhuru, amani na raha, hakika mtu huyo atakuwa kwenye malengo ya Uislam, hata kama si Mwislamu. Kwa sababu yeye ni sawa na madini aliyoyatolea mfano wa haki Mwenyezi Mungu. Na kwamba kila mwenye kutenda kwa ajili ya uovu wa mtu. Yeye hana uislamu kitu, hata kama atafunga maisha na kuunganisha swala za usiku na alfajiri.

Waliomwitikia Mola wao watapata wema.

Yaani watapata wema kwa sababu ya kumwitikia Mola wao kwenye mwito wa kutenda kwa ajili ya manufaa ya watu na kwa ajili ya maisha bora. Ama makusudio ya wema ni ujira na thawabu na kwamba watu wa haki watanufaisha, kama maji yanavyonufaisha ardhi.

Na wasiomwitikia - nao ni wale wasiokuwa na maana, kama mapovu- hata wangelikuwa na vilivyomo ardhini vyote na mfano wake, hakika wangelivitoa kujikombolea. Hao wana hisabu mbaya kabisa na makao yao ni Jahannam, na hapo ni mahali pabaya mno.

Umetangulia mfano wake katika Juz.3 (3:91) na Juz,11(10:54).

أَفَمَن يَعْلَمُ أَنَّمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ أَعْمَىٰ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿١٩﴾

19. Je, anayejua kwamba yaliyoteremshwa kutoka kwa Mola wako ni haki, ni sawa na aliye kipofu? Wanaozingatia ni wenye akili tu.

الَّذِينَ يُوفُونَ بِعَهْدِ اللَّـهِ وَلَا يَنقُضُونَ الْمِيثَاقَ ﴿٢٠﴾

20. Wale ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu wala hawavunji maagano.

وَالَّذِينَ يَصِلُونَ مَا أَمَرَ اللَّـهُ بِهِ أَن يُوصَلَ وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ وَيَخَافُونَ سُوءَ الْحِسَابِ ﴿٢١﴾

21. Na wale ambao huyaunga aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe na humwogopa Mola wao na huihofu hisabu mbaya.

وَالَّذِينَ صَبَرُوا ابْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَنفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً وَيَدْرَءُونَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ أُولَـٰئِكَ لَهُمْ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢٢﴾

22. Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao na wakasimamisha Swala na wakatoa kwa siri na kwa uwazi katika vile tulivyowaruzuku na wakayaondoa maovu kwa wema, Hao ndio watakaopata malipo ya nyumba.

جَنَّاتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا وَمَن صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ وَالْمَلَائِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِم مِّن كُلِّ بَابٍ ﴿٢٣﴾

23. Nayo ni Bustani (Pepo) za Milele wataziingia wao na walio wema miongoni mwa baba zao wake zao na vizazi vyao, Na Malaika wanawaingilia kila mlango.

سَلَامٌ عَلَيْكُم بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢٤﴾

24. (wakisema): Assalaam alaykum kwa sababu ya mlivyosubiri. Basi ni mema mno malipo ya nyumba.

وَالَّذِينَ يَنقُضُونَ عَهْدَ اللَّـهِ مِن بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّـهُ بِهِ أَن يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ أُولَـٰئِكَ لَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٢٥﴾

25. Na wale wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuifunga na wanakata aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe na wanafanya ufisadi katika nchi. Hao ndio walio na laana na wana nyumba mbaya.

## YALIYOTEREMSHWA KUTOKA KWA MOLA WAKO NI HAKI

**Aya 19-25**

### MAANA

Je, anayejua kwamba yaliyoteremshwa kutoka kwa Mola wako ni haki, ni sawa na aliye kipofu? wanaozingatia ni wenye akili tu.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kufananisha ukafiri na upofu, tena akafananisha haki kwa maji na batili kwa povu, sasa anafananisha mwenye kumwamini Muhammad na kuona na mwenye kumkana kwa upofu.

Mwenyezi Mungu ameeleza uhakika huu kwa njia ya swali ili kumsuta na kumtahayariza.

Wanaozingatia ni wenye akili tu wanasikiliza sauti kwa akili na yule asiyetia akilini isipokuwa yanayoafiki hawaa yake, ni sawa na asiye na akili.

Kisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja sifa za wenye akili ambazo zinafahamisha makusudio ya wenye akili kuwa ni waumini wenye takua; kama ifuatavyo:

1. Wale ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu.

Kila lililo na dalili basi hilo ni ahadi ya Mwenyezi Mungu na ni juu ya binadamu kutekeleza, lakini maibilisi wanapotosha uhakika kwa mapenzi yao kisha wananasibisha hawa zao hizi za kishetani kwa Mwenyezi Mungu na haki. Mwenyezi Mungu ametakata na yale wanayomzushia.

Wala hawavunji maagano, Hii ni kutilia mkazo kauli yake 'wanatimiza' ambapo wanalazimiana na utekelezaji ahadi bila ya kuvunja.

2. Na wale ambao huyaunga aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe.

Wafasiri wametaja kauli kadhaa katika kufasiri aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe, Kauli iliyo karibu zaidi ya roho ya Uislamu na misingi yake, ni ile ya yule aliyesema: Makusudio ya aliyoamrisha yaungwe, ni msaada wa mtu kwa nduguye mtu, kusaidiana naye kuondoa madhara na kuleta manufaa kwa karibu au mbali.

3. Na humwogopa Mola wao na huihofu hisabu mbaya kimatendo sio kinadharia na kimaneno. Imam Ali anasema: "Mambo mema yanafahamika kwa imani na imani inafahamika kwa mambo mema."

4. Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao. Wanapigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, wanavumilia majeraha na maumivu; hawataki malipo wala shukrani isipokuwa radhi ya Mwenyezi Mungu peke yake.

5. Na wakasimamisha Swala ambayo mwanzo wake ni Takbira ihram: Mungu ni mkubwa zaidi (Allahu akbar) hakuna mkubwa zaidi yake vyovyote atakavyo kuwa. Na Mwisho wake swala ni Tahlil na Salaam: Hakuna Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu (lailalaha illallah) Hakuna anayeabudiwa isipokuwa Yeye; hakuna mali wala jaha au hisabu zinazoweza kuabudiwa wala hakuna nguvu inayonyenyekewa isipokuwa nguvu yake Mwenyezi Mungu pekee yake bila ya kuwa na mshirika.

6. Na wakatoa kwa siri na kwa uwazi katika vile tulivyowaruzuku, Mali ndiyo ugomvi. Angalia tulivyoielezea katika mwanzo wa Juz.4 (3:92).

7. Na wakayaondoa maovu kwa wema, Hao ndio watakaopata malipo ya nyumba.

Makusudio ya wema hapa ni msamaha na uovu ni haki maalum inayokuwa baina ya wawili; kama kisasi. Mwenyezi Mungu anasema: "Mmeandikiwa kisasi katika waliouawa; muungwana kwa muungwana na mtumwa kwa mtumwa na mwanamke kwa mwanamke, Na anayesamehewa na ndugu yake chochote, basi ni kufuatana kwa wema na kulipa kwa ihsani." Juz.2 (2:178)

Ama haki ya Mwenyezi Haina kusameheana,

وَلَا تَأْخُذْكُم بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّـهِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّـهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ﴿٢﴾

"Wala isiwashike kwa ajili yao huruma katika hukumu ya Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho." (24:2).

Nayo ni Bustani (Pepo) za Milele wataziingia wao na walio wema miongoni mwa baba zao wake zao na vizazi vyao.

Wema wote wataingia peponi, Iwapo duniani walikuwa na udugu na upenzi basi furaha itazidi kwa kuunganishwa tena na kukumbuka enzi zao walipokuwa duniani. Iwapo matendo yao yatatofautiana, basi udugu na urafiki utakatika siku hiyo:

فَرِيقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ ﴿٧﴾

Kundi moja litakuwa Peponi na kundi jingine litakuwa Motoni. (42:7).

Na Malaika wanawaingilia kila mlango (wakisema): Assalaam alaykum kwa sababu ya mlivyosubiri. Basi ni mema mno malipo ya nyumba.

Maana ya Assalaamu alykum! Ni: Amani iwe juu yenu. Kauli yake Mwenyezi Mungu kwa sababu ya mlivyosubiri, inaashiria kwamba Pepo ni haramu isipokuwa kwa mwenye kufanya jihadi akasubiri, akavumilia tabu na mashaka ya jihadi, Imam Ali (a.s) anasema: **"Pepo imezungukwa na machukivu na moto umezungukwa na matamanio. Na jueni kuwa hakuna yeyote anayemtii Mwenyezi Mungu ila hujiwa na machukivu,Na hakuna yeyote aliyemwasi Mwenyezi mungu ila hujiwa na matamanio."**

Na wale wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuifunga.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwataja wema na sifa zao na malipo mema aliyowaandalia, sasa anawataja wafisadi. Kwa ibara ya kuunganisha ni kuwa baada ya kutaja wanamapinduzi dhidi ya ufisadi anataja wapinzani wao.

Ni kawaida makundi mawili hayo kupingana, Watenda mema hutekeleza ahadi ya Mwenyezi Mungu, wakatenda kulingana na akili na dhamiri na kila linalofahamishwa na dalili. Wafisadi wanavunja ahadi yake Mwenyezi Mungu na hutenda kulingana na mawazo ya kishetani wakiichanganya haki na batili na wakiificha haki na hali wanajua

Na wanakata aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe.

Wanawatawalisha mataghuti wakosaji na kuwasaidia kuwakandamiza watu wema kinyume na aliyoamrisha Mwenyezi Mungu na kuyakataza.

Na wanafanya ufisadi katika nchi kwa kuidhihirisha dhulma na kuleta fitina vurugu, kuwapoteza wasio na hatia, kuleta utengano, kuleta maangamizi na kila aina ya ufisadi na upotevu.

Hao ndio walio na laana na wana nyumba mbaya.

Ikiwa matendo yao ni kinyume cha watendao mema, basi vile vile ni kawaida malipo yao yawe tofauti. Wema watapata pepo na nyumba yenye neema na waovu watapata Jahannam na mahali pabaya.

اللَّـهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۚ وَفَرِحُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا مَتَاعٌ ﴿٢٦﴾

26. Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye na humkunjia. Wamefurahia maisha ya dunia na maisha ya dunia kwa kulingana na Akhera si kitu ila ni starehe.

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِّن رَّبِّهِ ۗ قُلْ إِنَّ اللَّـهَ يُضِلُّ مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ أَنَابَ ﴿٢٧﴾

27. Na husema wale ambao wamekufuru: "Kwa nini hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake?" Sema: Mwenyezi Mungu humpoteza amtakaye na humuongoza anayeelekea kwake.

الَّذِينَ آمَنُوا وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُم بِذِكْرِ اللَّـهِ ۗ أَلَا بِذِكْرِ اللَّـهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ ﴿٢٨﴾

28. Wale ambao wameamini na zikatua nyoyo zao kwa kumdhukuru Mwenyezi Mungu. Ehe! Kwa kumdhukuru Mwenyezi Mungu nyoyo zinatua.

الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ طُوبَىٰ لَهُمْ وَحُسْنُ مَآبٍ ﴿٢٩﴾

29. Wale ambao wameamini na wakafanya matendo mema, raha ni yao na marejeo mazuri.

## HUKUNJUA RIZIKI

**Aya 26-29**

### MTU NA RIZIKI

Katika Juz.6 (5:66) Tumelielezea suala hili. Pia katika Juz, 7 (5:100), tumefafanua zaidi katika kifungu 'Je riziki ni bahati au majaliwa' Hivi sasa tunarudia maudhui haya kwa mfumo mwingine kwa kuangalia umuhimu wake.

Mtu ana sifa nyingi, zikiwemo za kidhati na ulazima anazokuwa nazo bila ya kubanduka; kwa mfano kuwa mrefu au mfupi kuwa ni mtoto wa tajiri au fukara. Nyingine, sio za dhati ni za kutafuta; mfano kuwa mkulima, mfanyabiashara, tabibu au mwajiriwa n.k.

Utajiri nao una sababu zake; zikiwemo nasabu; yaani urithi, Huo unatambuliwa na kukubaliwa na dini, hata kama haukupatikana kwa jasho. Sababu nyingine ni ulanguzi na unyang'anyi; kama vile riba, ghushi, wizi, biashara ya haramu n.k. Huu ni haramu, hilo halina shaka. Sababu nyingine ya utajiri ni jasho la mtu na bidii; kama vile ukulima, viwanda n.k. Sababu hii ndio bora zaidi kiakili na kisharia.

Kwa hiyo basi, inatubainikia kuwa ufukara na utajiri unatokana na sanaa ya ardhini sio ya mbinguni. Lakini wako wanaotoka nje ya hayo na kuziita sababu za hayo kuwa ni tawfiki ya Mungu, wengine wakaita bahati, lakini hakuna hata mmoja wao anayethubutu kusema kuwa kadhaa na kadari inaingilia juhudi za mtu na kazi yake na kwamba inawaunga mkono wengine kwa kuwasaidia na kuwaacha wengine. Hakuna anayeweza kuthibitisha hilo. Vinginevyo ingelikuwa sababu zote ni bure tu, na kufanya kazi kungelikuwa ni maneno tu yasiyokuwa na maana.

**Unaweza kuuliza**: Kauli yako hii si inapingana na kauli ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye na humkunjia.

**Jibu**: Maisha ya watu yako makundi mawili: kuna wale walio na riziki pana na wale walio na riziki finyu. Kila moja kati ya utajiri na ufukara unatokana na sababu zake maalum ambazo tumekwisha zidokeza. Kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye na humkunjia' ni wasifu na kuelezea hali halisi ya watu; kana kwamba anasema watu ni makundi mawili mafukara na matajiri. Mwenyezi Mungu ameutegemeza ufukara na utajiri kwake ili kutanabahisha kuwa Yeye mtukufu ndiye muumba wa ulimwengu ambao una tabu na raha.

Ikiwa mtu atasema kwa nini basi Mwenyezi Mungu asingeumba ulimwengu usiokuwa na dhiki?

Majibu yake yako kwenye Juz, 5 (4:78), 'Kifungu cha Haiwezekani kuongeza zaidi ya ilivyo'

Wamefurahia maisha ya dunia na maisha ya dunia kwa kulingana na Akhera si kitu ila ni starehe.

Mfano wa Aya hii umekwishapita mara nyingi, ikiwemo ile ya Juz.4 (3:185). Kuongezea na tuliyoyazungumza huko, ni kwamba kuna aina ya watu wanafurahia mali kwa sababu inasitiri aibu yao na uovu wao. Wengi katika wao hawaoni kitu isipokuwa kwenye mali na utajiri. Ni maarufu kwa wamarekani kwamba wao hawaangalii kitu chochote ila kupitia dola (pesa). Hicho ndicho kipimo cha hadhi ya mtu, hata wataalamu na wenye vipaji, thamani yao ni vile vilivyo katika mifuko yao sio vilivyo vichwani mwao.

Na husema wale ambao wamekufuru: Kwa nini hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake?.

Umepita mfano wake katika Juz,1 (2: 118), Juz. 7 (6:37), Juz,11 (10:20) na kwa herufi zake hizihizi katika Juzu na sura hii tunayoendela nayo Aya 7.

Sema: Mwenyezi Mungu humpoteza amtakaye na humuongoa anayeelekea kwake.

Angalia kifungu cha ‘Uongofu na upotevu’ kwenye Juz,1 (2: 26) na kifungu ‘Upotevu’ katika Juz.5 (4:88).

Wale ambao wameamini na zikatua nyoyo zao kwa kumdhukuru Mwenyezi Mungu. Ehe! Kwa kumdhukuru Mwenyezi Mungu nyoyo zinatua.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) alipotaja watu wa mali na furaha yao inayotokana na kutulizana kwao kwenye maisha yao, anawataja waumini kwamba ni wale wanaotulizana kwa dhikri ya Mwenyezi Mungu. Kutua au kutulizana moyo maana yake ni kuzidi asili ya imani; yaani uthabiti wa imani na utulivu wake. Kuna Aya inayosema:

قَالَ أَوَلَمْ تُؤْمِن قَالَ بَلَىٰ وَلَـٰكِن لِّيَطْمَئِنَّ قَلْبِي ﴿٢٦٠﴾

“(Mwenyezi Mungu) akasema: Huamini? Akasema: Kwa nini! (naami-ni) Lakini upate kutulia moyo wangu.” Juz. 3 (2:260)

وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالْإِيمَانِ ﴿١٠٦﴾

Na hali ya kuwa moyo wake umetulia juu ya imani (16:106).

Makusudio ya Dhikr sio kutamka maneno tu; isipokuwa ni dhikri ambayo inamzidisha yakini ya Mwenyezi Mungu yule mwenye kudhukuru na akawa ana mategemeo ya ahadi na miadi yake Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo dhikri ya matamshi tu na tasbihi sio dhikr ya kiuhakika. Dhikri inayozidisha yakini ni ile aliyoisema Mwenyezi Mungu:

فَاذْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ ﴿١٥٢﴾

Basi nidhukuruni nitawadhukuru Juz 2 (2:152).

Wale ambao wameamini na wakafanya matendo mema, raha ni yao na marejeo mazuri.

Makusudio ya raha ni Pepo. Aya hii inaoana na ile isemayo:

وَبَشِّرِ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ﴿٢٥﴾

Wabashirie wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri, kwamba watapata mabustani yapitayo mito chini yake Juz.1 (2:25).

8

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

كَذَٰلِكَ أَرْسَلْنَاكَ فِي أُمَّةٍ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهَا أُمَمٌ لِّتَتْلُوَ عَلَيْهِمُ الَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَهُمْ يَكْفُرُونَ
بِالرَّحْمَٰنِ ۚ قُلْ هُوَ رَبِّي لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ مَتَابِ ﴿٣٠﴾

30. Ndio kama hivi tumekutuma kwa umma ambao zimekwishapita kabla yao umma nyingine, ili uwasomee tunayokupa wahyi na wao wamemkufuru Mwingi wa rehema. Sema, Yeye ni Mola wangu hakuna Mola mwengine isipokuwa yeye. Juu yake nimetegemea na kwake Yeye ndio marejeo yangu.

وَلَوْ أَنَّ قُرْآنًا سُيِّرَتْ بِهِ الْجِبَالُ أَوْ قُطِّعَتْ بِهِ الْأَرْضُ أَوْ كُلِّمَ بِهِ الْمَوْتَىٰ ۗ بَل لِّلَّهِ الْأَمْرُ جَمِيعًا ۗ أَفَلَمْ
يَيْأَسِ الَّذِينَ آمَنُوا أَن لَّوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَهَدَى النَّاسَ جَمِيعًا ۗ وَلَا يَزَالُ الَّذِينَ كَفَرُوا تُصِيبُهُم بِمَا
صَنَعُوا قَارِعَةٌ أَوْ تَحُلُّ قَرِيبًا مِّن دَارِهِمْ حَتَّىٰ يَأْتِيَ وَعْدُ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَا يُخْلِفُ الْمِيعَادَ ﴿٣١﴾

31. Na lau kwamba Qura'n ndiyo inayoendeshewa milima au kupasuliwa ardhi au kusemeshewa wafu (wasingeliamini). Bali amri zote ni za Mwenyezi Mungu. Je, hawajajua wale ambao wameamini kwamba lau Mwenyezi Mungu angelipenda bila shaka angeliwaongoa watu wote,Wala wale ambao wamekufuru hawaachi kusibiwa na balaa kwa waliyoyatenda au ikawateremkia karibu na nyumbani kwao mpaka iwafikie ahadi ya Mwenyezi Mungu, Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi.

## TUMEKUTUMA KATIKA UMMA

**Aya 30-31**

## MAANA

Ndio kama hivi tumekutuma kwa umma ambao zimekwishapita kabla yao umma nyingine, ili uwasomee tunayokupa wahyi na wao wamemkufuru Mwingi wa rehema.

Maneno yanelekezwa kwa Muhammad **(s.a.w.w)**. Mwenyezi Mungu amepeleka mitume kabla yao kwenye umma zilizopita kwa lengo hilo hilo, sasa basi kuna kioja gani? Wao si watu wa kwanza kupelekewa mtume na yeye si mtume wa kwanza kuwasomea watu wahyi wa Mwenyezi Mungu.

Sema: Yeye ni Mola wangu hakuna Mola mwengine isipokuwa yeye. Juu yake nimetegemea na kwake yeye ndio marejeo yangu.

Hii ndio imani ya Muhammad **(s.a.w.w)** na huu ndio mwito wake, Anamwamini Mwenyezi Mungu peke yake na anamwelekea Yeye kwenye mamabo yake wala haoni mwenye uwezo mwingine zaidi yake, Anawalingania watu kwenye imani hii, Ni mwito ambao unajifahamisha wenyewe.

### FIKRA YA MATAGHUTI

Na lau kwamba Qur'an ndiyo inayoendeshewa milima au kupasuliwa ardhi au kusemeshewa wafu (wasingeliamini) Bali amri zote ni za Mwenyezi Mungu.

Umepita mafano wa Aya hii mwanzo wa Juz. 8, na tumefafanua huko kwa anuani ya 'Aina ya watu.' Pia utakuja mfano wake katika Juz. 15. (17:90).

Tukiunganisha tuliyoyatanguliza ni kwamba Aya hii inaleta picha ya njia wanayoifikiria mataghuti ambao maisha yao yanasimama kwa kuwanyonya wanyonge na kuwafanya watumwa wao. Si maumbile wala akili, hisia, yanayoshuhudiwa, miujiza au chochote kile kitakachoweza kubadilisha ukaidi wa mataghuti na ulafi wao. Dawa pekee ni kuwaondoa na kuondoa misingi yao ya uporaji na unyang'anyi. Pamoja na yote hayo Muhammad anawataka wamkubali yeye na Qura'n.

Lakini wapi? Ni mpaka majabali yaendeshwe na Qur'an? Au mpaka wasemeshwe wafu? Kisha ndio iweje! Watapata faida gani katika hayo? Au kumuona Mungu ana kwa ana kutaongeza faida kwenye mali zao?

Hii ndio fikra yao na hii ndiyo lugha wanayoifahamu na kuisikiliza; wala hawasikilizi lugha nyingine isiyokuwa hiyo – lugha ya uchumi na faida ya paundi na dola. Lakini haki, uadilifu, mantiki na akili ni mazungumzo ya kipumbavu, yanayosadikiwa na watoto na wajinga.

Je, baada ya hayo, mtu anaweza kuuliza kwanini mataghuti hawakumwamini Muhammad pamoja na wito wake wa uadilifu na wema?

Mwito huu unaotaka kung'oa mizizi ya dhulma na ufisadi wanauona ni kosa kubwa. Hii ndio fikra pekee wanyoifikiria wale wanaoishi kwa uny- onyaji na unyang'anyi. Alikuwa nayo fikra hii Abu Jahl na Abu Sufyan wakati wa Muhammad **(s.a.w.w)**, katika zama zetu wamekuwa nayo Hitler na Musolini na leo hii fikra hii iko kwenye dola za kiukandamizaji zikion- gozwa na Marekani.

Dalili wazi ya hilo ni Marekani. Leo inaushinikiza Umoja wa Mataifa, kwa nguvu zake zote, ijitie hamnazo kwa sula lolote la usawa na uadilifu, ikishindwa inajitokeza waziwazi kupiga vita kila taifa litakalotaka haki na uadilifu na kuisaida dhulma na utaghuti popote ulipo; ni sawa uje kwa njia ya Israil au Ureno au hata kwa serkali ya kibaguzi ya Rhodesia[1] na Afrika kusini au kwengineko.

Siri ya yote hayo ni kuifagilia Marekani, kama kiongozi wa ukoloni. Lakini mwisho wa ubabe huu utakuwa kama wa Hitler, Dalili zimejionyesha wazi katika Vietnam. Ama masononeko yanayosababishwa na siyasa ya ukoloni yameena mashariki na magharibi, na masononeko haya hayatapita bure bila ya kuacha athari.

Mwanzo nilikuwa nikistaajbu kutokana na baadhi ya watu jinsi wanavyowadharau watu wema wenye ikhlasi na wasiwaheshimu, tena wanawaona ni kama watu wa kawaida; hata kama wakifanya maajabu gani na wakajitolea mhanga kuithibitisha haki!

Niliendelea kushangaa hivyo mpaka nilipofikia kufasiri Aya hii tuliyo nayo nikagundua kuwa fikra hii haiko kwa mataghuti na wafisadi tu; isipokuwa watu wengi wameondoa akilini ubora na msimamo na kuupima kwa chumo na faida tu; sawa na wale waliompiga vita Muhammad na waliosimama upande wa Israil katika Umoja wa mataifa na Baraza la usalama; isipokuwa tofauti yao hawa ni kuwa waliifuata njia ya ufisadi na utaghuti, lakini waliposhindwa basi wakabakia kwenye upinzani.

Je, hawajajua wale ambao wameamini kwamba lau Mwenyezi Mungu angelipenda bila shaka angeliwaongoa watu wote.

1. Nchi hiyo hivi sasa inaitwa Zimbabwe.- Mtarjumu.

Neno hawajajua limefasiriwa kutoka neno Yay'as, Tabari anasema: "wametofautiana wafasiri kuhusu neno 'yay'as' … Usawa hasa ni kubainikiwa na wamenukuu tafsiri hii wengi akiwemo Imam Ali (a.s). Na sisi ni miongoni mwa wale wanaoamini kuwa watu wa nyumba ndio wanojua zaidi kilichomo humo nyumbani."
Vyovyote iwavyo ni kuwa makusudio ya wale ambao wameamini ni maswahaba wa Mtume **(s.a.w.w)** pale walipotamaani kuwa washirikina wamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Ndipo Mwenyezi Mungu aliyetukuka akwaambia, mpaka lini mtakuwa na tamaa ya kuamini washirikina?
Je, hajajua na kubainikiwa kuwa wao kivyovyote hawataamini hata kama wafu watazungumza nao au majabali yatembee. Achaneni nao na utaghuti wao! Lau Mwenyezi Mungu angelitaka kuwaingiza kwenye imani angelifanya, lakini hekima yake Mtukufu imepitisha kumwachia mtu na hiyari yake ili kuweza kumpa uhuru na ubinadamu wake.
Lau angelimnyang'anya uhuru huu na hiyari, basi asingelikuwa ni chochote, na wala asingelistahiki kusifiwa au kushutumiwa wala thawabu au adhabu, Angalia tafsir yetu Juz. 12 (11: 118).

Wala wale ambao wamekufuru hawaachi kusibiwa na balaa kwa waliyoyatenda au ikawateremkia karibu na nyumbani kwao mpaka iwafikie ahadi ya Mwenyezi Mungu.

Makusudio ya wale ambao wamekufuru ni wale waliomkadhibisha Muhammad **(s.a.w.w)**. Maana ni kuwa Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu hawachi duniani hawa waliokadhibisha bila ya kuwatia adabu; bali anawateremshia balaa kila baada ya muda.
Hayo ni kwa sababu ya msimamo wao kwa Muhammad **(s.a.w.w)**. Au anawateremshia balaa karibu yao iwatie hofu na fazaa nyoyoni mwao. Analifuatilia hilo Mwenyezi Mungu mpaka itimie ahadi yake ya ushindi kwa Mtume wake.

Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi.

Vipi avunje miadi naye ndie mkweli zaidi wa ahadi. Maswahaba na kila mumin ana imani kuwa Mwenyezi Mungu atatekeleza ahadi na atalinusuru jeshi lake tu.

وَلَقَدِ اسْتُهْزِئَ بِرُسُلٍ مِّن قَبْلِكَ فَأَمْلَيْتُ لِلَّذِينَ كَفَرُوا ثُمَّ أَخَذْتُهُمْ ۖ فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ ﴿٣٢﴾

32. Na hakika walifanyiwa stihizai Mitume waliokuwa kabla yako, lakini nikawapa muda wale ambao wamekufuru, kisha nikawashika! Basi ilikuwaje adhabu!

أَفَمَنْ هُوَ قَائِمٌ عَلَىٰ كُلِّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ ۗ وَجَعَلُوا لِلَّـهِ شُرَكَاءَ قُلْ سَمُّوهُمْ ۚ أَمْ تُنَبِّئُونَهُ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي الْأَرْضِ أَم بِظَاهِرٍ مِّنَ الْقَوْلِ ۗ بَلْ زُيِّنَ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مَكْرُهُمْ وَصُدُّوا عَنِ السَّبِيلِ ۗ وَمَن يُضْلِلِ اللَّـهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ﴿٣٣﴾

33. Je anayesimamia kila nafsi kwa yale iliyoyachuma na wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika! Sema watajeni, Au ndio mnampa habari ya yale asiyoyajua katika ardhi? Au ni maneno matupu? Bali wale ambao wamekufuru wamepambiwa vitimbi vyao na wamezuiliwa njia. Na anayepotezwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumuongoza.

﴿لَّهُمْ عَذَابٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۖ وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَشَقُّ ۖ وَمَا لَهُم مِّنَ اللَّـهِ مِن وَاقٍ ﴿٣٤﴾

34. Wanayo adhabu katika maisha ya dunia. Na hakika adhabu ya Akhera ina mashaka zaidi. Na wala hawana wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu.

## MITUME WALIFANYIWA STIHZAI

**Aya 32-34**

### MAANA

Na hakika walifanyiwa stihizai Mitume waliokuwa kabla yako, lakini nikawapa muda wale ambao wamekufuru, kisha nikawashika! Basi ilikuwaje adhabu!

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anamwambia Mtume wake, vumilia na uendele na mwito wako na achana nao wale wanokukejeli na jiweke mbali na maoni yao kwako, Walikwishafanya waliokuwa kabla yako, nikawaacha kisha nikawaadhibu adhabu isiyowezekana. Huu kwa hakika ndio mwisho wa wakadhibishaji.

Mwenyezi Mungu hakumtuma mtume ila anampa mambo mawili: Ujuzi wa dalili za kilimwengu na za kiakili juu ya kuweko Muumba na umoja wake, Na muujiza unaojitokeza mikononi mwake utakaojulisha utume wake. Jambo hilo la kwanza ni kwa ajili ya kuwakinahisha watu na Tawhidi (umoja wa Mungu) na la pili ni kwa jili ya kuwakinaisha watu kuwa yeye ni mtume wa Mwenyezi Mungu.

Wale wasioamini isipokuwa manufaa yao na chumo lao tu walikuwa wakiwakejeli Mitume na kuwafanyia maskhara pamoja na dalili zao na miujiza yao. Mwenyezi Mungu naye huwapa muda ili warudi kwenye uongofu na awaonye kwa kuwapa muda, kama alivyowaonya kwa hoja.

Je anayesimamia kila nafsi kwa yale iliyoyachuma.

Anaichunga nafsi na kuilinda na kudhibiti kila kitu, kisha kuilipa thawabu ikifanya mema na adhabu ikifanya uovu. Mwenye sifa zote hizi anafanywa kuwa wenzake ni mawe? Na wawemfanyia Mwenyezi Mungu washirika! Mwenyezi Mungu anasema:

﴿أَفَمَن يَخْلُقُ كَمَن لَّا يَخْلُقُ ۗ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿١٧﴾

Ati anayeumba ni kama asiyeumba? Basi hivi hamkumbuki? (16:17).

Sema watajeni.

Yaani enyi washirikina tajeni angalau sifa moja tu inayostahiki kuabudiwa masanamu yenu, Hii ni dharau na dhihaka, sawa na mwoga kusema: Mimi ni shujaa, kisha aambiwe: tutajie ushahidi mmoja wa ushujaa wako.

Au ndio mnampa habari ya yale asiyoyajua katika ardhi?

Mwenyezi Mungu anasema hana mshirika na nyinyi manasema ana washirika wengi. Maana yake ni kuwa wao wanajua zaidi na Mwenyezi Mungu hajui.

Ametakaka Mwenyezi Mungu na hayo kabisa; kama wase- mavyo watu wa mantiki: kikipatikana chenye kulazimiwa ndio umepatikana ulazima na kikikosekana chenye kulazimiwa ndio umekosekana ulazima – likipatikana jua ndio umeptikana mchana na likikosekana jua ndio umekosekana mchana na ukikosekana mchana ndio hakuna jua.

Kwa hiyo ikiwa kuna mshrika, kwa vyovyote Mwenyezi Mungu atamjua. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu hamjui mshirika huyo basi hayupo; vinginevyo Mungu atakuwa halijui hilo, jambo ambalo haliwezekani.

Mwenyezi Mungu amehusisha kutaja ardhi pamoja nakuwa Yeye hana mshirika ardhini na mbinguni, kwa vile mazungumzo yanahusiana na masanamu yaliyoko ardhini.

Au ni maneno matupu.

Hilo ni tamko la kufahamisha maana ya kupatikana. Maneno yoyote yasiyofahamisha kitu halisi basi ni maneno matupu. Na neno washirika hapa ni majina yasiyokuwa na wenyewe:

إِنْ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمَّيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَآبَاؤُكُم مَّا أَنزَلَ اللَّـهُ بِهَا مِن سُلْطَانٍ ﴿٢٣﴾

"Hayo hayakuwa ila ni majina mliyoyaita nyinyi na baba zenu ambayo Mwenyezi Mungu hakuyateremshia dalili yoyote" (53:23).

Umepita mfano wa Aya hii katika Juz. 8 (7:710) na katika Juz, 12 (12:40).

Bali wale ambao wamekufuru wamepambiwa vitimbi vyao.

Maana ya vitimbi ni hadaa. Washirikina walihadaliwa na masanamu, wakayadhania ni washirika wa Mwenyezi Mungu katika viumbe vyake na wakajipambia wenyewe hadaa hii.

Na wamezuiliwa njia kwa kuchukulia lisilojulikana.

Yaani lile walilojipambia limewazuilia wao na haki na imani ya Mwenyezi Mungu na umoja wake.

Na anayepotezwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumuongoza. Tazama Juz. 5 (4:88).

Wanayo adhabu katika maisha ya dunia kwa kupata hizaya na utwevu.

Na hakika adhabu ya Akhera ina mashaka zaidi, kwa sababu kila kitu duniani kusikiwa kwake ni kukubwa kuliko kuonekana kwake na kila kitu katika Akhera kuonekana kwake ni kukubwa kuliko kusikiwa kwake; kama asemavyo Imam Ali (a.s).

Na wala hawana wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu na adhabu yake.

9

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

مَّثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وُعِدَ الْمُتَّقُونَ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ أُكُلُهَا دَائِمٌ وَظِلُّهَا تِلْكَ عُقْبَى الَّذِينَ
اتَّقَوا وَّعُقْبَى الْكَافِرِينَ النَّارُ ﴿٣٥﴾

35. Mfano wa Bustani (Pepo) waliyoahidiwa wenye takua inapita mito chini yake, matunda yake ni ya daima na pia kivuli chake. Hiyo ndio mwisho wa wale wenye takua. Na mwisho wa makafiri ni moto.

وَالَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَفْرَحُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمِنَ الْأَحْزَابِ مَن يُنكِرُ بَعْضَهُ قُلْ إِنَّمَا
أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّـهَ وَلَا أُشْرِكَ بِهِ إِلَيْهِ أَدْعُو وَإِلَيْهِ مَآبِ ﴿٣٦﴾

36. Na wale ambao tumewapa Kitabu wanafurahia uliyoteremshiwa, Na katika makundi mengine wapo wanayoyakataa baadhi yake. Sema: Nimeamrishwa nimwabudu Mwenyezi Mungu wala nisimshirikishe. Ninalingania kwake Yeye, na marejeo ni kwake.

وَكَذَٰلِكَ أَنزَلْنَاهُ حُكْمًا عَرَبِيًّا وَلَئِنِ اتَّبَعْتَ أَهْوَاءَهُم بَعْدَ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ مَا لَكَ مِنَ اللَّـهِ
مِن وَلِيٍّ وَلَا وَاقٍ ﴿٣٧﴾

Na ndio kama hivyo tumeiteremsha Qur'an kuwa ni hukumu kwa Kiarabu. Na kama ukifuata hawaa zao baada ya kukujia ilimu hii, hutakuwa na msimamizi wala mlinzi mbele ya Mwenyezi Mungu.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّن قَبْلِكَ وَجَعَلْنَا لَهُمْ أَزْوَاجًا وَذُرِّيَّةً وَمَا كَانَ لِرَسُولٍ أَن يَأْتِيَ بِآيَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ
اللَّـهِ لِكُلِّ أَجَلٍ كِتَابٌ ﴿٣٨﴾

38. Na hakika tulikwishawatumma mitume kabla yako na tukawajalia wawe na wake na kizazi. Na haiwi kwa Mtume kuleta muujiza isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, Kila muda una kitabu.

## MFANO WA BUSTANI

**Aya 35-38**

### MAANA

Mfano wa Bustani (Pepo) waliyoahidiwa wenye takua inapita mito chini yake, matunda yake ni ya daima na pia kivuli chake.

Mwenyezi Mungu alipomaliza kutaja malipo ya makafiri, sasa anataja malipo za wenye takua, kama kawaida yake ya kutaja kitu na kinyume chake. Malipo ya wenye takua ni Bustani (Pepo) pamoja na nema yake ya kudumu – mito, matunda na vivuli.

Hiyo ndio mwisho wa wale wenye takua.

Hiyo ni ishara ya Pepo. Wenye kumcha Mungu ni wale wanoilinda haki na watu wake na kupambana na batili na watu wake. Kuna Hadith isemayo: "Hakika imani iko juu ya Uislamu na kumcha Mungu kuko juu ya Imani na yakini iko juu ya kumcha Mungu" Makusudio ya yakini ni kuwa na imani na Mwenyezi Mungu na kumtegemea Yeye.

Na mwisho wa makafiri ni moto.

Makusudio ya makafiri hapa sio tu wale wanaomkana Mwenyezi Mungu au kumshirikisha; isipokuwa makusudio ni kila anayeipinga haki, huku akiwa anajua. Zimeleza Hadith nyingi kuwa unafiki ni ukafiri n ria ni shirk. Mwenyezi Mungu amewasifu na ukafiri madhalimu, aliposema:

فَأَبَى الظَّالِمُونَ إِلَّا كُفُورًا ﴿٩٩﴾

"Lakini madhalimu hawataki ila ukafiri" (17:99);
kama ambavyo amewasifu makafiri na washirikiana kwa dhulma katika Aya kadhaa.

## SHIA IMAMIYA NA SWAHABA

Wamezowea baadhi ya wanaolipwa walio wajinga kuleta fitna na ghasia baina ya Waislamu ili kuuchafua umoja wao na kuwagombanisha. Wamezoya sana hilo kwa njia ya kutia doa na kuleta uzushi kwa Shia kwa kuwazulia kuwatukana maswahaba; kumfanya Mungu Ali, kuwa Qur'an imepotolewa, jambo ambalo linaitingisha Arsh, na mengineyo miongoni mwa uwongo na uzushi.

Nimeandika makala ndefu katika kuwajibu vibaraka na wafanya propaganda hizi. Kisha nikayaweka kwenye vitabu: Ma'shia al-imamiyya, Ashia wal-hakimun, Al-ithnaashariya wa Ahlulbayt, na Ashia wat tashayyu' ambacho ni kikubwa kuliko vyote.

Lengo langu la kwanza la makala na tungo hizi ni kuuweka wazi uhakika kwa yule anayetaka kuujua na kuubatilisha uongo na uzushi uliosemwa na unaosemwa juu ya taifa hili.

Hapa nimedokeza niliyoyaandika na kuyatunga kuhusiana na maudhui haya kwa mnasaba wa Aya hii tuliyo nayo, kama ifuatavyo:

Na wale ambao tumewapa Kitabu wanafurahia uliyotermshiwa.

Amesema Abu Hayan Al-andalusi, Zamakhshari, Sheikh Al-maraghi, Al-baydhawi na wengineo katika maulama wa kisunni kuwa makusudio ya wale ambao wamepewa Kitabu ni Myahudi na Manaswara wale waliomwamini Muhammad **(s.a.w.w)**.

Na akasema Tabrasiy, katika Tafsir Majmau'lbayan, ninamnukuu: "Mwenyezi Mungu (s.w.t) anawakusudia maswahaba wa mtume **(s.a.w.w)** ambao walimwamini na kumsadikisha, wakapewa Qur'an na kuifurahia kushuka kwake" Tabrasiy ni miongoni mwa maulama wakubwa wa kishia (alikufa mwaka 548 AH).

Kwa hiyo basi wanchuoni wengi wa kisunni wamefasiri Aya hii kuwa ni waliosilimu katika Mayahudi na manaswara; na wa kishia wamefasiri kuwa ni Mswahaba wa Mtume mtukufu **(s.a.w.w)**. Ikiwa wao wanawatukana maswahaba angelielekea Sheikh wao Tabrasiy, katika kufasiri Aya hii kwenye njia ya maswahaba, Hapa unatubainikia uzushi uliowekwa kwenye kundi hili.

Aban bin Taghlab ni mmoja katika wanafunzi wakubwa wa Imam Jafar As-Sadiq (a.s), kiasi ambacho Imam alikuwa akiwaamuru Shia kuchukua dini kutoka kwake. Siku moja aliulizwa na mtu mmoja anayeitwa Abul-bilad kuhusu Shia, akamwambia: ni wale ambao wakitofautiana watu kuhusu riwaya iliyopokewa kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** basi huchukua riwaya ya Ali aliyoipokea kutoka kwa Mtume na wanapotofautiana watu katika riwaya ya Ali huchukua kauli ya Jafar As-Sadiq aliyoipokea kutoka kwa Ali.

Kwa hiyo basi, kwa Shia, kadhia ni mategemezi ya riwaya kutoka kwa Muhammad **(s.a.w.w)** sio kadhia ya kutukana na kushutumu maswahaba wa Muhammad. Siri ya mategemezi yao Shia kwa Ahlu bayt (watu wa nyumba ya Mtume) ni Hadith kadhaa zilizothibiti, zinazohimiza hilo. Miongoni mwazo ni ile allyoipokea Muslim katika Sahihi yake kutoka kwa Mtume, kwenye mlango wa Fadhail Ali bin Abi Twalib (Ubora wa Ali bin Abi Twalib), kwamba mtume amesema:

Mimi ni mtu, mjumbe wa Mwenyezi Mungu anakurubia kunijia nimwitikie; nami ninacha kwenu vizito viwili, cha kwanza ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu ndani yake mna uongofu na nuru, basi kichukueni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na shikamaneni nacho.

Akahimiza kuhusu Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kukipen- dekeza, kisha akasema: Na Ahl bayt yangu (watu wa nyumba yangu) ninawakumbusha kwa Mwenyezi Mungu kuhusu Ahl bayt wangu, Alilikariri hilo mara tatu.

Na katika makundi mengine wapo wanayoyakataa baadhi yake.

Makusudio ya makundi mengine ni watu wa mila na dini nyingine; kama vile mayahudi, manaswara na wengineo wanaoyakataa yale yanayokhalifiana na mapenzi yao na wakayakubali yanayoafikiana na mapenzi yao katika Qur'an.

Ilivyo ni kuwa kupinga kwao hawa na kukubali kwao ni sawa tu, kwa sababu kukubali ni kwa kuafikiana na hawaa zao sio kwa sababu ya Qur'an.

Sema: Nimeamrishwa nimwabudu Mwenyezi Mungu wala nisimshirikishe. Ninalingania kwake Yeye, na marejeo ni kwake.

Huu ndio Uislamu: Hakuna Mola mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu ni wake ufalme na mwito wa kuabudiwa ni kwake Yeye tu, na mwisho marejeo ni kwake yeye.

Na ndio kama hivyo tumeiteremsha Qur'an kuwa ni hukumu kwa Kiarabu.

Makusudio ya hukumu ni Qur'an, kwa sababu ndio hukumu ya Mwenyezi Mungu, isiyokuwa hiyo ni hukumu ya kijahili; kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

أَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّـهِ حُكْمًا لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٥٠﴾

"Je wanataka hukumu za Kijahiliya, Na ni nani aliye mwema zaidi kwa hukumu kuliko Mwenyezi Mungu, kwa watu wenye yakini" Juz, 6 (5:50)

Kama ambavyo Mwenyezi Mungu, alimtuma kila mtume kwa lugha ya watu wake, vilevile alimtuma Muhammad. Mwenyezi Mungu anasema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن رَّسُولٍ إِلَّا بِلِسَانِ قَوْمِهِ لِيُبَيِّنَ لَهُمْ ﴿٤﴾

"Na hatukumtuma Mtume ila kwa ulimi wa watu wake ili apate kuwabainishia (14:4)

Tumefafanua sababu za kushuka Qur'an kwa kiarabu, pamoja na kuwa Muhammad ametumwa kwa watu wote, katika Juz. 12 (12:2).

Na kama ukifuata hawaa zao baada ya kukujia ilimu hii, hutakuwa na msimamizi wala mlinzi mbele ya Mwenyezi Mungu.

Wanaokusudiwa katika neno hawaa zao ni watu wa mila nyingine isiyokuwa Uislamu. Mwenyezi Mungu anajua kuwa Nabii hafuati wala hatafuata hawaa na matamanio yao. Lengo la ukatazo huu ni uthabiti na kuendelea kuilingania haki, wala asiogope lawama ya mwenye kulaumu.

Tumeelza mara kwa mara kuwa amri ikitoka kwa mkubwa hakiangaliwi cheo cha mdogo vyovyote kilivyo

Na hakika tulikwishawatuma mitume kabla yako na tukawajalia wawe na wake na kizazi.

Asiye na haki akishindwa huanza kuzungusha maneno na kupima mambo kwa mawazo na njozi zake. Na hivyo hasa ndivyo ilivyokuwa kwa washirikina na Muhammad **(s.a.w.w)**. Aliwaletea hoja na dalili, waliposhindwa kuzijibu wakanza kusema: itakuwaje ni nabii naye ana mke na watoto.

Mantiki hii inafanana kabisa na mantiki ya wanaoamini utawa. Mwenyezi Mungu amewajibu kwa kuwambia kuwa Muhammad ni kama Nuh, Ibrahim, Ismail na wengineo katika mitume ambao wana wake na watoto, sasa kuna ajabu gani katika hilo?

Kuna hadith iliyopokewa kutoka kwa mtume, amesema: Ama mimi ninafunga, ninafungua, ninalala, ninaamka, ninakula nyama na ninaoa. Mwenye kujiepusha na desturi yangu basi yeye si katika mimi.

Na haiwi kwa Mtume kuleta muujiza isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

Haya vilevile ni majibu kwa washirikina ambao walimpendekezea mtume miujiza ile waitakayo. Njia ya majibu ni kuwa Yeye Mwenyezi Mungu swt) amemsheheneza mtume wake kwa dalili zinazotosheleza kujulisha juu ya utume wake, kwa yule mwenye kuzingatia na kuitafuta haki kwa njia ya haki. Ama kuitikia mapenzi ya mwenye inadi na kiburi hakukubaliwi na akili wala desturi. Anaachiwa Mwenyezi Mungu na hekima yake.

Kila muda una kitabu.

Yaani kila kitu kina muda wake, kiwe ni muujiza, adhabu, au chochote kile, Na muda umeandikwa hautangulizwi wala kucheleweshwa nao umefichwa, haujui isipokuwa Mwenyezi Mungu

يَمْحُو اللَّـهُ مَا يَشَاءُ وَيُثْبِتُ ۖ وَعِندَهُ أُمُّ الْكِتَابِ ﴿٣٩﴾

39. Mwenyezi Mungu hufuta na huthibitisha ayatakayo na kwake kuna mama wa Kitab.

وَإِن مَّا نُرِيَنَّكَ بَعْضَ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ نَتَوَفَّيَنَّكَ فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَاغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿٤٠﴾

40. Na ikiwa tutakuonyesha baadhi ya tuliyowaahidi au tukakufisha, basi ni juu yako kufikisha na juu yetu ni hisabu.

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا ۚ وَاللَّـهُ يَحْكُمُ لَا مُعَقِّبَ لِحُكْمِهِ ۚ وَهُوَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٤١﴾

41. Je hawakuona kwamba tunaifikia ardhi tukiipunguza janibu zake. Na Mwenyezi Mungu huhukumu, hapana wa kupinga hukumu yake; na Yeye ni mwepesi wa kuhisabu.

قَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ فَلِلَّـهِ الْمَكْرُ جَمِيعًا ۖ يَعْلَمُ مَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ ۗ وَسَيَعْلَمُ الْكُفَّارُ لِمَنْ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٤٢﴾

42. Na wamekwisha fanya vitimbi waliokuwa kabla yao na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye vitimbi vyote, Anajua inayoyachumma kila nafsi. Na makafiri watajua ni ya nani nyumba ya mwisho.

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَسْتَ مُرْسَلًا ۚ قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ وَمَنْ عِندَهُ عِلْمُ الْكِتَابِ ﴿٤٣﴾

43. Na wale ambao wamekufuru wanasema wewe hukutumwa. Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi na yule mwenye elimu ya Kitabu.

## MWENYEZI MUNGU HUFUTA NA HUTHIBITISHA AYATAKAYO

**Aya 39-43**

### MAANA

Mwenyezi Mungu hufuta na huthibitisha ayatakayo na kwake kuna mama wa Kitab.

Mama wa kitabu ni fumbo la ujuzi wake Mwenyezi Mungu wa yaliyokuwa na yatakayokuwa.

Lau ingekuwa inafaa kufasiri matamshi kwa muonjo na kupendeza, basi tungelifasiri kitabu ni ulimwengu na mama ni siri zake; kwa sababu Mwenyezi Mungu ana vitabu viwili: kimoja kinatamka kwa lugha ya hali nacho ni ulimwengu na kingine kinatamka kwa lugha ya maneno nacho ni Qur'an.

Ama kufuta na kuthibitisha, Tabrasi amenukuu katika maana yake kauli nane, iliyokaribu zaidi na maana ni kuwa makusudio ya kufuta ni kufuta sharia za zamani au kufuta baadhi ya hukumu zake; kama vile kufuta hukumu ya kuelekea Baytil-maqds. Ama kuthibitisha, makusudio yake ni kuthibitisha hukumu mpaka siku ya Kiyama.

Kwa hiyo maana ni kuwa Yeye Mwenyezi Mungu (s.w.t) anafuta au kuthibitisha sharia zote au baadhi, vile masilahi na hekima yake inavyotaka. Na Yeye ambaye umetukuka utufu wake anajua yaliyo na maslahi kwa waja na yaliyo na uharibifu. Kwa hiyo anawamrisha hili na kuwakataza lile, daima au kwa muda, kulingana na vile elimu yake inavyojua muda wa madhara na manufaa, Tumezungumzia kuhusu kufuta hukumu katika Juz.1 (2:106).

Na ikiwa tutakuonyesha baadhi ya tuliyowaahidi au tukakufisha, basi ni juu yako kufikisha na juu yetu ni hisabu.

Aya hii ianungana na Aya 31 ya Sura hii. Njia ya kuungana ni dhahiri: Kule amemwambia mtume wake kuwa Yeye kwa vyovyote atamteremshia adhabu yule anayemkadhibisha; hapa anasema kama tutakuonyesha adhabu yao au tutakufisha kabla ya hiyo adhabu, basi umuhimu wako wa kwanza na wa mwisho ni kufikisha tu, mengine tuachie sisi.

Je hawakuona kwamba tunaifikia ardhi tukiipunguza janibu zake.

Ardhi ni tufe, lisilokuwa na ncha, lakini ni pana linaloweza kukaliwa na mamilioni ya aina mbali mbali ya viumbe, Nayo hubadilika daima. Binadamu anaweza kuona au kusikia kuwa ardhi hii ni nzuri kukaliwa na watu itakuwa na maendeleo na ardhi ile haifai ni njangwa. Mara ile iliyoonekana inafaa inakuwa haifai na ile iliyokuwa jangwa isiyofaa inakuwa bustani yenye mito.

Watu wa ardhi pia ni hivyo hivyo, maendeleo yanakuwa hai na mengine yanakufa; ufalme unasimama na mwingine unaanguka, Hivi ndivyo ilivyo

dunia ‘kigeugeu’ Hakuna ubaya wala neema inayoweza kudumu hapa ardhini.
Imam Ali (a.s) anasema: **“Tahadharini na dunia ina ghururi na inahadaa, inatoa na kuzuia, inavika na kuvua. Haidumu raha yake wala tabu yake haiishi.”** Kauli yake Mwenyezi Mungu: Tukiipunguza janibu zake, inaashiria maana hii na kwamba mwenye akili anapata funzo kwa mageuko haya:

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ﴿١٠٩﴾

“Je, hawatembei katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? (12:109).

Na Mwenyezi Mungu huhukumu, hapana wa kupinga hukumu yake.

Na amekwisha hukumu kuwaangamiza wenye makosa na amekwishaipitisha hukumu hiyo.

Na wamekwisha fanya vitimbi waliokuwa kabla yao na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye vitimbi vyote.

Makusudio ya vitimbi vya Mwenyezi Mungu ni kupangua vitimbi, Angalia Juz.3 (3:53).

Anajua inayoyachuma kila nafsi; Kwa sababu yeye ni mwenye wasaa aliye mjuzi.

Na makafiri watajua ni ya nani nyumba ya mwisho. Siku ile watakaporudi kwa Mola wao na kusema leo ni siku nzito.

Na wale ambao wamekufuru wanasema wewe hukutumwa.

Waliukana utume wa Muhammad pamoja na dalili zote, kwa vile huo ni vita dhidi ya dhulma na utaghuti na jambo lolote linalozuia uhuru wa mtu, amani yake na wema wake

## RAHA YA DHAMIRI NA MAWAZO

Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi na yule mwenye elimu ya Kitabu.

Katika Aya hii Mwenyezi Mungu anamwamrisha mtume wake awaambie: ikiwa mnakanusha utume wangu, basi Mwenyezi Mungu anshuhudia kuwa mimi ni mtume kutoka kwake, vile vile wenye kuchunga haki katika maulama wa Tawrat na Injil wanashuhudia hilo.

Haya ndio maana ya dhahiri na ndio makusudio yake na ndiyo waliyoeleza wafasiri na sisi tuko pamoja nao, lakini zaidi ya hiyo tunagusia maana kubwa zaidi inayofungamana na kila mwenye kuiamini haki akaitumia na akapingwa na wenye kufanya ufisadi katika ardhi na yakampata yaliyowapata.

Muhtasari wa maana haya makubwa na matukufu ambayo yanaashiriwa na Aya ni kuwa kila ambaye dhamiri yake inalionea raha jambo na kushuhudiwa na mawazo yaliyo salama, basi Mwenyezi Mungu, Malaika wake na wenye kuchunga haki pia wanalishuhudia kuwa ni haki, awe ni Mtume au sio Mtume.

**Unaweza kuuliza**: Ni wakati gani mtu anakuwa na raha ya dhamiri na kushuhudiwa na mawazo salama?

**Jibu**: Hakika binadamu hawezi kuwa ni katika mwenye dhamiri hai na mawazo salama ila ikiwa anaamini msimamo wa kibinadamu; kama vile uadilifu, uhuru, ukweli, uaminifu na mengineyo ambayo heri yake

inawarudia wote. Pale tu, mtu atakapoamini msimamo huu na ukaoana na vitendo vyake, basi atakuwa amestarehe dhamiri, na kushudiwa na mawazo yake.
Na wakati wowote, vitendo vyake na imani yake vitakapotengana, atakuwa ameitia utumwani dhamiri yake na itamsuta yeye mwenyewe.
Watu wa dhamiri na mawazo hawatilii umuhimu isipokuwa misimamo yao mbele ya dhamiri zao na mbele ya watu wema mfano wao ambao wanashirikiana nao kwa kuonyesha mfano na msimamo wa kibinadamu.
Lakini msimamo wao unakuwa hauna thamani mbele ya asiyekuwa na dhamiri ambaye haoni isipokuwa nafsi yake na masilahi yake tu.
Mimi nina yakini kwamba watu wema zaidi ni wale wenye misimsmo ya haki ambao hawajui starehe yoyote isipokuwa ile inayotuliza dhamiri zao.
**Unaweza kuuliza**: kuwa watu wengi wanaona raha wanapo pata yale wanayoyataka, ingawaje wao hawamini misingi wala misimamo yoyote; je, hiyo si inamaana wema na raha ni kupata mtu atakacho na ubaya ni kukosa atakacho?
**Jibu**: **kwanza**: mazungumzo yetu tangu mwanzo ni juu ya watu wenye dhamiri, na hawa unaowasema hawana dhamiri yoyote.
**Pili**: watu wengi wanaojionyesha kuwa wanapinga misimamo, huwa kiundani, wanaikubali ndani ya nafsi yao; lakini uovu ulipowashinda walijaribu kuficha kwa kukana yale wanayoyaamini, huku wakijidanganya kwa kusema:
Lau kungelikuwa na msimamo wowote tungelilazimiana nao; sawa na mwenye makosa kukana makosa yake, huku anajua kuwa yeye ni mwenye hatia.

## MWISHO WA SURA YA KUMI NA TATU

10

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

Sura Ya Kumi Na Nne: Surat Ibrahim

Imeshuka Makka. Ina Aya 52, Imesemekana kuwa Aya mbili katika hizo zimeshuka Madina.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

الر كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِ رَبِّهِمْ إِلَىٰ صِرَاطِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿١﴾

1. Hiki ni Kitabu tulichokiteremsha kwako ili uwatoe watu gizani uwapeleke kwenye nuru, kwa idhini ya Mola wao, uwafikishe kwenye njia ya Mwenye nguvu, Mwenye kusifiwa.

اللَّـهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَوَيْلٌ لِّلْكَافِرِينَ مِنْ عَذَابٍ شَدِيدٍ ﴿٢﴾

2. Ni Mwenyezi Mungu ambaye ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na ole wao makafiri kwa adhabu kali.

الَّذِينَ يَسْتَحِبُّونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا عَلَى الْآخِرَةِ وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّـهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا أُولَـٰئِكَ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿٣﴾

3. Wale ambao wamestahabu maisha ya dunia kuliko Akhera na wakawazuilia watu na njia ya Menyezi Mungu na wanataka kuipotosha, hao wamepotelea mbali.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن رَّسُولٍ إِلَّا بِلِسَانِ قَوْمِهِ لِيُبَيِّنَ لَهُمْ فَيُضِلُّ اللَّـهُ مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٤﴾

4. Na hatukumtuma Mtume ila kwa ulimi wa watu wake ili apate kuwabainishia. Basi humpoteza amtakaye na humwongoza amtakaye na Yeye ni Mwenye nguvu mwenye hekima.

## DINI NI NURU

**Aya 1-4**

### MAANA

Alif Laam Raa

Umetangulia mfano wake katika Juz.1 (2:1).

Hiki ni Kitabu tulichokiteremsha kwako ili uwatoe watu gizani uwapeleke kwenye nuru, kwa idhini ya Mola wao, uwafikishe kwenye njia ya Mwenye nguvu Mwenye kusifiwa.

Makusudo ya Kitabu hapa ni Qur'an. Msemo wa tumekuteremshia unaelekezwa kwa Muhammad **(s.a.w.w)**. Na makusudio ya idhini ni amri.

Aya inafahamisha kwa uwazi kuwa lengo la msingi la kutumwa Muhammad **(s.a.w.w)** na kuteremshwa Qura'n ni kuziweka pamoja nguvu zote za watu na kuwa na mshikamano kwa ajili ya ubinadamu na heri yake na utulivu wake. Kwa sababu kuwatoa watu kwenye giza hakuwezi kukamilika kwa

miito na Swala; isipokuwa ni kwa juhudi za pamoja, sio za mtu pekee, dhidi ya ukandamizaji, ujinga, ufisadi na uigizaji wa kipumbavu.
Na kweli Muhammad aliunganisha udugu baina ya maswahaba zake, na akawaingiza roho ya kusafiana nia, mahaba na kujitolea na akawafanya miongoni mwao - wakiwa ni washamba na wajinga-wajumbe wa heri wenye kuelimika na maendeleo.
Kwa mnasaba huu tunagundua kuwa wale matapeli wanaohimiza upotofu kwa kuupa jina la dini, kuwa ni maadui wakubwa wa Mwenyezi Mungu na mtume wake. Kwa sabu dini ni nuru na upotofu ni giza, dini ni njia ya Mwenyezi Mungu mwenye kusifiwa na giza ni njia ya shetani mwenye kulaaniwa. Unaweza kuuliza, kuna Aya isemayo:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na dini ya haki ili ipate kushinda dini zote, ijapokwa washirikina wamechukia. Juz. 10 (9:33)
**Unaweza kuuliza**: Dahiri ya Aya hii ni kuwa Mwenyezi Mungu amemtuma Muhammad kwa lengo la kuwa dini yake iwe juu ya dini zote. Sasa kuna wajihi gani wa kuunganisha baina ya Aya hizi mbili (kushinda dini na kutoa gizani)?.
**Jibu**: **kwanza**: makusudio ya dini katika kauli yake Mwenyezi Mungu: 'ili ipate kushinda dini zote,' ni ushirikina. Hilo linafahamika kutokana na kauli yake: ijapokuwa washirikina wamechukia.
**Pili**: kwamba dini zote katika zama za Muhammad zilikuwa ni giza, hata zile dini za mbinguni zilikuwa zimechezewa na mikono ya wapotofu.
**Tatu**: Kuwa juu dini ya Muhammad ndio kuwa juu haki ambayo, siku zote iko juu wala haikaliwi. Vyovyote iwavyo ni kwamba misingi yoyote wanayonufaika nayo watu kwa namna yoyote ile, inakutana katika upande huu na dini ya Mwenyezi Mungu na mwito wa Muhammad, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**.
Ni Mwenyezi Mungu ambaye ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini
Kauli hii imekaririka katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu mara kumi, Na lengo ni kukumbusha kuwa Mwenyezi Mungu ndiye muumba wa ulimwengu na ni mtawala wa vilivyo humo.
Kisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) anataja malipo ya makafiri na sifa zao:
1. Na ole wao makafiri kwa adhabu kali.
Hiki ni kiaga cha Mwenyezi Mungu kwa makafiri kutokana na ukafiri wao, kwamba malipo yao ni maangamizi na adhabu. Razi anasema: "Hakika amewahusu kwa ole wao, kwa sababu watakuwa katika adhabu kali wakisema ole wetu."
2. Wale ambao wamestahabu maisha ya dunia kuliko Akhera.
Huu ndio wasifu wa kwanza wa makafiri; kwamba wao wameathirika na batili kuliko haki, dhulma kuliko uadilifu na ufisadi kuliko wema. Kila anayekuwa hivyo basi yeye ni kafiri au anakutanishwa na makafiri katika vitendo vyake, naye anastahiki laana na adhabu, kama wanavyostahiki makafiri; ajapo swali, akufunga na akahiji.
3. Na wakawazulia watu na njia ya Mwenyezi Mungu.
Wanawazulia watu na njia ya haki na uongofu, wakawa kwa hilo ni wenye kupotea na wenye kupoteza, wafisadi na wenye kufisidisha.

4. Na wanataka kuipotosha, hao wamepotelea mbali.

Neno upotofu linaashiria kuwa wao wanafikia malengo yao kwa njia kombokombo na za haramu; kama vile uwongo, utapeli, njama na kusaidiana na mataghuti. Wasifu huu hauhusiki na washirikina na makafiri peke yao; kwani Waislamu wengi wanasema uwongo, wanafanya hiyana na kupanga njama pamoja na maadui wa Mwenyezi Mungu na wa wananchi dhidi ya viumbe wa Mwenyezi Mungu na nyenzo zao. Hawa ni wapotevu zaidi na waliopotea njia.

Makusudio ya upotevu uliombali, ni kuwa wao wamezama kwenye upotevu mpaka wakafikia mwisho wake.

Na hatukumtuma Mtume ila kwa ulimi wa watu wake ili apate kuwabainishia waweze kumfahamu na litimie lengo la risala yake.

Lau kungelikuwa na Lugha inayoweza kufahamika na watu wote, basi angelitumwa nayo Muhammad **(s.a.w.w)**, kwa sababu yeye ni Mtume wa watu wote sehemu zote na wakati wote.

Hata hivyo ni lazima ifahamike kuwa kuna tofauti baina ya kusema Tumemtuma kwa lugha ya watu na kusema Tumemtuma kwa watu wa lugha yake. Tamko la kwanza halizuiwii kuwa mjumbe wa wote na tamko la pili linahusika na watu wake tu. Angalia Juz. 12 (12:2).

Mwenyezi Mungu aliwatuma wajumbe wake kwa waja wake ili awaokoe kutokana na ujinga na upotevu. Basi mwenye kuwasikiliza na akatii, ameongoka na mwenye kuachana nao akaasi basi ni mpotevu. Kwa hiyo uon- gofu unapimwa kwa kumtii Mwenyezi Mungu na upotevu kwa kumwasi.

Na lau kama Mwenyezi Mungu hakuweka sharia wala kuwatuma mitume basi kusingelikuwa na twaa na maasi wala uongofu na upotevu, Lakini Yeye Mwenyezi Mungu ameweka sharia akatuma mitume. Kwa hiyo natija ya hayo ni twaa na maasi, uongovu na upotevu.

Kwa kuzingatia hivi ndipo ikafaa kunasibisha upotevu na uongofu kwake Yeye Mwenyezi Mungu ambaye umetukuka utukufu wake Angalia Juz.1 (2:26) na Juz. 5 (4: 88).

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا أَنْ أَخْرِجْ قَوْمَكَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَذَكِّرْهُم بِأَيَّامِ اللَّـهِ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿٥﴾

5. Hakika tulimtuma Musa pamoja na miujiza yetu kuwa watoe watu wako kutoka gizani kwenda kwenye nuru, Na uwakumbushe siku za Mwenyezi Mungu. Hakika katika hayo kuna ishara kwa kila mwenye kusubiri, mwenye kushukuru.

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ اذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّـهِ عَلَيْكُمْ إِذْ أَنجَاكُم مِّنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ وَيُذَبِّحُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ ۚ وَفِي ذَٰلِكُم بَلَاءٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَظِيمٌ ﴿٦﴾

6. Na Musa alipowaambia watu wake: “Kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, alipowaokoa na watu wa Firauni walipowapa adhabu mbaya na wakiwachinja watoto wenu wa kiume na wakiacha hai watoto wenu wa kike, Na katika hayo ulikuwa mtihani mkubwa kutoka kwa Mola wenu.”

وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ ۖ وَلَئِن كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ ﴿٧﴾

7. Na alipotangaza Mola wenu: Mkishukuru nitawazidishia na mkikufuru basi adhabu yangu ni kali.

وَقَالَ مُوسَىٰ إِن تَكْفُرُوا أَنتُمْ وَمَن فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا فَإِنَّ اللَّـهَ لَغَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٨﴾

8. Na alisema Musa: mkikufuru nyinyi na waliomo duniani wote, hakika Mwenyezi Mungu ni mkwasi mwenye kusifiwa.

## TULIMTUMA MUSA

**Aya 5-8**

### MAANA

Hakika tulimtuma Musa pamoja na miujiza yetu kuwa watoe watu wako kutoka gizani kwenda kwenye nuru.

Maneno yamerudi tena kwa Musa (a.s) na Waisrail ambao walimtoa roho. Mazungumzo yamewarudia wao na yamekaririka mara kadhaa. Mimi sijui siri ya kukaririka mazungumzo yanayowahusu wao kuliko wengine isipokuwa ni kwamba wao wamevuka mipaka ya kiutu kitabia na kivitendo; kama nilivyodokeza mwanzoni. Mimi sifichi kuwa ninaona uzito sana nikifasiri Aya zilizo na jina la Waisrail.

Na uwakumbushe siku za Mwenyezi Mungu.

Siku zilizo dhahiri zaidi na zenye neema juu yao ni zile walizookolewa na adhabu ya Firauni na kukombolewa kutoka utumwani.

Hakika katika hayo kuna ishara kwa kila mwenye kusubiri mwenye kushukuru.

"Vumilia mitihani yako kwa kutumaini nusura yako"

Makusudio ya hayo ni hayo ya ukumbusho. Na makusudio ya ishara hapa ni mazingatio na mawaidha. Ilivyo ni kuwa mwenye kuzingatia na akawaidhika ndiye mumin wa kweli anayeshukuru wakati wa raha na kuvumilia wakati wa balaa pamoja na kujitahidi kufanya ikhlas.

Na Musa alipowaambia watu wake: "Kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, alipowaokoa na watu wa Firauni, walipowapa adhabu mbaya na wakiwachinja watoto wenu wa kiume na wakiacha hai watoto wenu wa kike. Na katika hayo ulikuwa mtihani mkubwa kutoka kwa Mola wenu.

Musa (a.s) aliwakumbusha wana wa Israil aliyowafanyia Firauni-kuwachinja watoto wao wa kiume na utumwa. Na akawakumbusha neema ya kuepukana na hayo na akawaamrisha wamkumbuke Mwenyezi Mungu na wamshukuru. Lakini wao hawakumshukuru wala kumkumbuka; bali walimkufuru Mwenyezi Mungu na wakaikana neema yake wakamuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wao Musa kwa kumwambia: Tuonyeshe Mungu waziwazi, Nenda wewe na Mola wako mkapigane.

Walipowapitia watu wakiabudu masanamu wakamwambia Musa tufanyie Mungu kama huyu wao; kisha wakaabudu ndama.

Hayo ndiyo malipo ya kumlipa Mungu aliyewaokoa na adhabu ya Firauni. Musa alipokata tamaa nao na kuona dhiki kubwa alimwelekea Mwenyezi Mungu na kusema:

قَالَ رَبِّ إِنِّي لَا أَمْلِكُ إِلَّا نَفْسِي وَأَخِي فَافْرُقْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٥﴾

Ewe Mola wangu! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu; basi tutenge na watu hawa mafasiki Juz.6 (5:25)

Kuna maajabu gani baada ya hayo ikiwa Mayahudi wataikana neema ya waislamu kwao siku walipokataliwa na ulimwengu, ambapo hakukuwa na Amerika wala Uingereza au Ujerummani ya magharibi kuwafanya wao ni madalali na mbwa wa kulinda ukoloni na u-Nazi, Umepita mfano wake katika Juz.1 (2:49).

Na alipotangaza Mola wenu: Mkishukuru nitawazidishia na mkikufuru basi adhabu yangu ni kali.

Makusudio ya kukufuru hapa ni kumuudhi yule mneemeshaji na kuzikana neema zake, kwa sababu mazungumzo yanahusiana na waisrail kukana neema za Mwnyezi Mungu. Wamesema wafasiri wengi kuwa Mwenyezi Mungu akimneemesha mja wake na akashukuru na akamkiri Mwenyezi Mungu kwazo, basi Mwenyezi Mungu atamdumisha nayo na kumzidishia. Wamesema hivi kwa kuchukulia kauli mashuhuri: “Shukrani zinadumisha neema.”

Tuonavyo sisi ni kwamba makusudio ya kuzidi neema ni kuzidi hiyo neema Akhera si duniani, kwa sabubu ni uhakika kuwa makusudio ya adhabu kali ya kukufuru neema ni adhabu ya Akhera, kwa hiyo malipo ya kushukuru vilevile yatakuwa ni Akhera. Imethibiti kutoka kwa Mtume kwamba yeye alifanya sawa kumpa mwema na muovu. Imam Ali amesema: “Mali ingelikuwa yangu ningelifanya sawa; vipi isiwe hivyo na mali yote ni ya Mwenyezi Mungu”

Zaidi ya hayo tunashuhudia mali nyingi inarundikana kwa mataghuti kadiri wanvyozidi uasi na kupetuka mipaka. Ndio! Kama ingelikuwa makusudio ya kushukuru ni kuichunga mali, kuipangia vizuri na kuizalisha, basi wafasiri wangelikuwa na njia ya kusemea, lakini hiyo ni kinyume na dhahiri ya Aya ilivyo na wala hakuna aliyewahi kusema hivyo, hata hao wafasiri wenyewe.

Na alisema Musa: “Mkikufuru nyinyi na waliomo duniani wote, hakika wenyezi Mungu ni mkwasi mwenye kusifiwa.”

Na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu si mwingine, na kujitosheleza ni kwake Yeye si mwingine. Musa alisema kauli hii kutokana na kukata kwake tamaa ya kuongoka Waisrail.

أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَبَأُ الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ قَوْمِ نُوحٍ وَعَادٍ وَثَمُودَ وَالَّذِينَ مِن بَعْدِهِمْ لَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا
اللَّـهُ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَرَدُّوا أَيْدِيَهُمْ فِي أَفْوَاهِهِمْ وَقَالُوا إِنَّا كَفَرْنَا بِمَا أُرْسِلْتُم بِهِ وَإِنَّا لَفِي
شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُونَنَا إِلَيْهِ مُرِيبٍ ﴿٩﴾

9. Je haziukuwafikia habari za walio kabla yenu: Kaumu ya Nuh na A’d na Thamud na walio baada yao? Hakuna awajuaye illa Mwenyezi Mungu, Waliwajia mitume wao kwa hoja zilizo wazi. Wakarudisha mikono yao kwenye vinywa vyao. Na wakasema: Hakika sisi tumeyakataa hayo mliyotumwa na hakika sisi tuna shaka kubwa ya mnayotuitia.

قَالَتْ رُسُلُهُمْ أَفِي اللَّـهِ شَكٌّ فَاطِرِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ يَدْعُوكُمْ لِيَغْفِرَ لَكُم مِّن ذُنُوبِكُمْ
وَيُؤَخِّرَكُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى قَالُوا إِنْ أَنتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا تُرِيدُونَ أَن تَصُدُّونَا عَمَّا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا
فَأْتُونَا بِسُلْطَانٍ مُّبِينٍ ﴿١٠﴾

10. Mitume wao wakasema: “Je kuna shaka na Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi? Anawaita ili apate kuwaghufiria dhambi zenu na

anawapa muhula mpaka muda uliowekwa. Wakasema: Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi. Mnataka kutuzuwia na waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu, Basi tuleteeni hoja iliyo wazi.

قَالَتْ لَهُمْ رُسُلُهُمْ إِن نَّحْنُ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ وَلَـٰكِنَّ اللَّـهَ يَمُنُّ عَلَىٰ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۖ وَمَا كَانَ لَنَا أَن نَّأْتِيَكُم بِسُلْطَانٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّـهِ ۚ وَعَلَى اللَّـهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾

11. Mitume wao wakawaambia: "Sisi si chochote ila ni wanadamu kama nyinyi, lakini Mwenyezi Mungu humneemesha amtakaye katika waja wake. Wala sisi hatuwezi kuwaletea dalili isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu.

وَمَا لَنَا أَلَّا نَتَوَكَّلَ عَلَى اللَّـهِ وَقَدْ هَدَانَا سُبُلَنَا ۚ وَلَنَصْبِرَنَّ عَلَىٰ مَا آذَيْتُمُونَا ۚ وَعَلَى اللَّـهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿١٢﴾

12. Na tuna nini hata tusimtegemee Mwenyezi Mungu na hali yeye ametuongoza kwenye njia yetu na hakika sisi tutavumilia mnayotuudhi, na kwa Mwenyezi Mungu nawategemee wenye kutegemea.

## JE HAZIKUWAFIKIA HABARI

**Aya 9-12**

### MAANA

Je haziukuwafikia habari za walio kabla yenu: Kaumu ya Nuh na A'd na Thamud na walio baada yao? Hakuna awajuaye illa Mwenyezi Mungu.

Mfumo wa maneno unaonyesha kuwa haya ni maneno kutoka kwa Nabii Musa (a.s) kwenda kwa wana wa Israil, sio kutoka kwa Muhammad **(s.a.w.w)** kwenda kwa washirikina wa kiarabu au wengineo, kama ilivyosemekana.

Maana ni kuwa Nabii Musa anawaambia Waisrail kuwapa mawaidha na kuwahadharisha kuwa mumesikia tufani ya Nuh na majanga yaliyowapitia watu wa A'd na Thamud na mengineyo zaidi ya hayo ambayo hajui idadi yake isipokuwa Mwenyezi Mungu? Aliwafanyia hayo Mwenyezi Mungu kwa sababu wao waliasi Mitume na wakafanya ukaidi. Je, hamzingatii na kupata mawaidha kwa umma zilizotangulia? Musa aliwaambia haya na zaidi watu wake, lakini Israil ni ileile ya mwanzo na ya mwisho.

Waliwajia mitume wao kwa hoja zilizo wazi.

Kila mtume anayetoka kwa Mwenyezi Mungu kwenda kwa waja wake hana budi kuwa amepewa hoja mkataa zinazofahamisha utume wake; kama vile balozi anavyoleta makaratasi ya kumjulisha kutoka kwenye serikali yake iliyomchagua kuwa balozi wake. Kwa hiyo basi inafahamisha kuwa makusudio ya hoja zilizowazi ni miujiza inayofahamisha juu ya unabii na utume wao.

Wakarudisha mikono yao kwenye vinywa vyao.

Waliorudisha ni watu wa Nuh na waliokuwa baada yao. Kurudisha mikono vinywani mwao ni fumbo la kukataa sana; mfano wa kauli yake Mwenyezi Mungu:

عَضُّوا عَلَيْكُمُ الْأَنَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ ﴿١١٩﴾

"Huwaumia vidole kwa hasira" Juz.4 (3:119)

Na wakasema: "Hakika sisi tumeyakataa hayo mliyotumwa na hakika sisi tuna shaka kubwa ya mnayotuitia.

Washirikina walitia shaka au walidhihirisha shaka katika ukweli wa mitume wao na hapo mwanzo walikuwa wakiwakubali kuwa ni wakweli na wenye ikhlasi. Kwanini? Si kwa lolote ila ni kuwa manabii waliwataka walazimiane na haki na uadilifu na kuacha dhulma na batili. Haya hasa ndio mantiki ya wale wanaoangalia masilahi yao tu; leo wanayakana yale waliyoyakubali jana na kinyume chake. Siri ya hilo inakuwa katika faida na chumo; wao wako pamoja nayo popote ilipo na itakapokuwa.

Mitume wao wakasema: "Je kuna shaka na Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi?

Ni ajabu ya maajabu kutia shaka mahali pa imani na kuamini mahali pa shaka. Walimpinga Muumba wao wakaamini mawe, yanayokojolewa na mambwa, na kuyaabudu.

Anawaita ili apate kuwaghufiria dhambi zenu.

Mwenyezi Mungu ametukuka! Angalia ukarimu wake na upole wake, anawaita waja wake kwenye msamaha wake na rehema yake na anawatakia yale yanayowanufaisha.

Na anawapa muhula mpaka muda uliowekwa, wala hana haraka ya kuwaadhibu, bali anawapa muda ili warejee kwenye uongofu.

Wakasema: "Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi.

Kauli hii inafahamisha fikra yao kwamba watu wa kawaida hawafai kushika uongozi wa juu, hata kama watakuwa na ikhlasi, ukweli, na kujitolea kwa kiwango cha juu.

Mnataka kutuzuwia na waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu.

Kwa hiyo baba zao ni watukufu zaidi ya Mwenyezi Mungu na kufuata kwao upotevu ni haki zaidi ya twaa ya Mwenyezi Mungu; hata kama baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawaongoki.

Basi tuleteeni hoja iliyo wazi.

Mitume waliwajia na hoja wazi na muujiza unaofahamisha kuhusu ukweli, lakini washirikina walitaka miujiza maalum ambayo Mwenyezi Mungu aliashiria kwa kusema:

لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ كَنزٌ أَوْ جَاءَ مَعَهُ مَلَكٌ ﴿١٢﴾

Mbona hakuteremshiwa hazina au wakaja naye Malaika? Juz, 12 (11:12)

وَقَالُوا لَن نُّؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَنبُوعًا ﴿٩٠﴾

Na wakasema: hatutakuamuini mpaka utuchimbulie chemchem katika ardhi hii au uwe na kitalu cha mitende na mizabibu na utupitishie mito kati yake ikimiminika (17:90)

wao wanataka miujiza, lakini kupitia tumboni sio akilini.

Mitume wao wakawaambia: "Sisi si chochote ila ni wanadamu kama nyinyi, lakini Mwenyezi Mungu humneemesha amatakaye katika waja wake.

Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye hekima na kwa vile yeye ni mwenye hekima na mjuzi, basi hamneemeshi kwa risala yake ila yule aliye kufu nayo mwenye sifa za kuichukua na kutekeleza:

اللَّـهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ﴿١٢٤﴾

Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi wa kujua mahali anapoweka ujumbe wake" Juz.8 (6:124)

Wala sisi hatuwezi kuwaletea dalili isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu.

Angalia katika Juzuu hii (13: 38), Juz.7 (6:37) na Juz.1 (2:118).

Na tuna nini hata tusimtegemee Mwenyezi Mungu na hali yeye ametuongoa kwenye njia yetu na hakika sisi tutavumlia mnayotuudhi; na kwa Mwenyezi Mungu nawategemee wenye kutegemea.

Tunayafupiliza maana, ingawaje yako wazi, kuwa Mitume waliwaambia washirikina: sisi tunafikisha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na tunamlingania Yeye; hatujali yule atakayekataa wala maudhi yatakayotupata katika njia hii. Kwa sababu sisi tunamtegemea Mola wetu na ubainifu wa jambo letu. Swali hili la: 'Tuna nini hata tusimtegemee Mwenyezi Mungu.' linafahamisha kwamba mitume hawaoni kitu isipokuwa Mwenyezi Mungu.

11

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِرُسُلِهِمْ لَنُخْرِجَنَّكُم مِّنْ أَرْضِنَا أَوْ لَتَعُودُنَّ فِي مِلَّتِنَا فَأَوْحَىٰ إِلَيْهِمْ رَبُّهُمْ لَنُهْلِكَنَّ الظَّالِمِينَ ﴿١٣﴾

13. Na wale ambao wamekufuru waliwaambia mitume wao: “Tutawatoa katika ardhi yetu au mrudi kwenye mila yetu. Mola wao akawapa wahyi: hakika tutawangamiza madhalimu.”

وَلَنُسْكِنَنَّكُمُ الْأَرْضَ مِن بَعْدِهِمْ ذَٰلِكَ لِمَنْ خَافَ مَقَامِي وَخَافَ وَعِيدِ ﴿١٤﴾

14. Nanyi tutawakalisha katika ardhi baada yao. Haya ni kwa anayeogopa kusi- mamishwa mbele yangu na akaogopa kiaga changu.

وَاسْتَفْتَحُوا وَخَابَ كُلُّ جَبَّارٍ عَنِيدٍ ﴿١٥﴾

15. Na wakaomba ushindi na akashindwa kila jabari mkaidi.

مِّن وَرَائِهِ جَهَنَّمُ وَيُسْقَىٰ مِن مَّاءٍ صَدِيدٍ ﴿١٦﴾

16. Nyuma yake iko Jahannam atanyweshwa maji ya usaha uliochanganyika na damu.

يَتَجَرَّعُهُ وَلَا يَكَادُ يُسِيغُهُ وَيَأْتِيهِ الْمَوْتُ مِن كُلِّ مَكَانٍ وَمَا هُوَ بِمَيِّتٍ وَمِن وَرَائِهِ عَذَابٌ غَلِيظٌ ﴿١٧﴾

17. Atayagugumia wala hataweza kuyameza. Na yatamfikia mauti kutoka kila mahali na wala yeye si maiti, Na nyuma yake kuna adhabu kali.

## TUTAKUTOA KWENYE ARDHI YETU

**Aya 13-17**

### MAANA

Na wale ambao wamekufuru waliwaambia mitume wao: Tutawatoa katika ardhi yetu au mrudi kwenye mila yetu.

Mitume walitoa mwito wa haki kwa hekima na mawaidha mazuri, wala hawakumlazimisha yeyote kwenye dini na itikadi yao, kwa sabau mwito wao umesimama kwenye misingi ya kutolazimisha kwenye dini; ingawaje hali halisi ni kuwa mwito wao ni mapinduzi kwa maadui na wakandamizaji.

Ndio maana nao wakatangaza vita dhidi yao; wakawapa mambo mawili: wartadi au wawafukuze.

Umetangulia mfano wa Aya hii mwanzoni mwa Juz.9 (7:88).

Mola wao akawapa wahyi: Hakika tutawangamiza madhalimu nanyi tutawakalisha katika ardhi baada yao. Haya ni kwa anayeogopa kusimamishwa mbele yangu na akaogopa kiaga changu.

Baada ya washirikina kufikia kuwatisha mitume, yakaja matakwa yake Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuwamaliza mataghuti na kuwarithisha waumini ardhi, majumba na mali zao.

وَأَوْرَثَكُمْ أَرْضَهُمْ وَدِيَارَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ ﴿٢٧﴾

Na tukawarithisha ardhi yao na majumba yao na mali zao (33:27)

## HAKI MBADALA

Itakuwa ni vizuri, kudokeza, kutokana na mnasaba huu, mambo Mawili:

Kwanza; kwamba yeye Mwenyezi Mungu, aliyemtukufu na kutuka baada ya kutaja majigambo ya wafisadi na madhalimu na kuendelea kwao kwenye upotevu, amesema kuwa mwisho wa hawa ni maangamizi, ikiwa ni natija ya uovu na upotevu wao na kwamba mwisho wa wenye takua ni ushindi na kumakinika ardhini.

Huu ndio mfumo wa Qur'an, kutaja sababu na kisababishi chake na natija pamoja na chanzo chake. Mfumo huu una faida zake; kama vile kuhimiza haki na kuikemea shari na batili. Pia kujua mtu mwisho mzuri na ushindi wa haki; hata kama watu wa batili wataishikilia kwa nguvu, wakajinaki na muda ukawa mrefu.

Wameitumia njia hii mahatibu wengi na waandishi; wanataja uovu wa mtu kisha wanafuatishia, wakiwa na uhakika kabisa, kwamba shari inamrudia mwenye kuifanya[1].

Jambo la pili; kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t), kwa matakwa yake, anaingilia kuinusuru haki kwa masharti ya kutoicha haki, kuitilia shaka au kuridhia haki mbadala na kutaka haki chache na kuridhia batili nyingi.

Majaribio yameonyesha kuwa haki mbadala haina faida isipokuwa kwa wafisadi katika ardhi na kwamba hiyo daima iko kwenye maslahi ya wabatilifu; kwa sababu aina yoyote ya kuipunguza haki ni faida kwa wanyang'anyi na ni hasara kwa haki na watu wake. Hapo ndio inakuwa siri ya Imam Ali (a.s) kutokuwa laini katika haki na kukataa kwake haki mabadala kwa aina zake zote.

Na wakaomba ushindi na akashindwa kila jabari mkaidi ambaye nyuma yake iko jahannam atanyweshwa maji ya usaha uliochanganyika na damu.

Usaha uliochanganyika na damu ni fumbo la ugumu wa kunywa na kumeza, kutokana na harufu mbaya na uchafu wake au uchungu na ukali wake au yote.

Imesemekana kuwa waliotaka ushindi ni mitume, ikasemekana kuwa ni washirikina na pia imesemekana ni wote. Maana yote yanafaa, kwa sababu mwisho ulikuwa, kama inavyotakiwa kuwa, ni ushindi wa haki na udhalili wa makafiri. Zaidi ya hayo mitume walitaka nusura kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.):

قَالَ رَبِّ انصُرْنِي عَلَى الْقَوْمِ الْمُفْسِدِينَ ﴿٣٠﴾

"Akasema: ewe Mola wangu! Ninusuru juu ya hawa watu mafisadi" (29:30)

Washirikina, siku ya Bdri, walisema: "Ewe Mola lipe ushindi jeshi lililo juu zaidi." Mwenyezi Mungu akawajibu:

إِن تَسْتَفْتِحُوا فَقَدْ جَاءَكُمُ الْفَتْحُ ۖ وَإِن تَنتَهُوا فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ﴿١٩﴾

"Kama mnataka ushindi, basi ushindi umekwishawajia, na kama mkiacha, basi itakuwa kheri kwenu; na kama mtarudia sisi pia tutarudia" Juz.9 (8:19)

Atayagugumia wala hataweza kuyameza, kutokana na ukirihi, uchafu, ukali, na uchungu wake.

Na yatamfikia mauti kutoka kila mahali.

1. Hata filamu nyingi huwa zinaonyesha mwisho mbaya wa waovu na maharamia- Mtarjumu.

Yaani sababu za mauti zitamzunguka pande zote sita: Kushotoni, kuumeni, nyuma na mbele, juu na chini yake.

Na wala yeye si maiti.

Lau angelikufa angelistarehe na kukatikikiwa na adhabu na Mwenyezi Mungu anataka awe nayo:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ نَارُ جَهَنَّمَ لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُم مِّنْ عَذَابِهَا ﴿٣٦﴾

"Na wale ambao wamekufuru watakuwa na moto wa Jahanam, hawatahukumiwa wakafa wala hawatapunguziwa adhabu yake." (35:36)

Na nyuma yake kuna adhabu kali.

Miongoni mwa yaliyosemekana katika tafsiri ya ukali hapa ni kuwa adhabu itakuwa inaanza upya kila baada ya kipindi fulani, na kila hali inakuwa mbaya zaidi ya ile iliyotangulia. Ewe Mola! msamehe anayekuamini wewe na pepo yako na moto wako wala hajibari na maasi yako, lakini ana matumaini ya rehema yako.

مَّثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ ۖ أَعْمَالُهُمْ كَرَمَادٍ اشْتَدَّتْ بِهِ الرِّيحُ فِي يَوْمٍ عَاصِفٍ ۖ لَّا يَقْدِرُونَ مِمَّا كَسَبُوا عَلَىٰ شَيْءٍ ۚ ذَٰلِكَ هُوَ الضَّلَالُ الْبَعِيدُ ﴿١٨﴾

18. Mfano wa wale ambao wamemkufuru Mola wao vitendo vyao ni kama majivu yanayopeperushwa kwa nguvu za upepo katika siku ya kimbunga. Hawana uwezo wa chochote juu ya walichokichuma, Huko ndiko kupotelea mbali.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّـهَ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ ۚ إِن يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٩﴾

19. Je, huoni kuwa Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa haki, akitaka atawaondoa na alete viumbe wapya?

وَمَا ذَٰلِكَ عَلَى اللَّـهِ بِعَزِيزٍ ﴿٢٠﴾

20. Na hilo kwa Mwenyezi Mungu si gumu.

وَبَرَزُوا لِلَّـهِ جَمِيعًا فَقَالَ الضُّعَفَاءُ لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ أَنتُم مُّغْنُونَ عَنَّا مِنْ عَذَابِ اللَّـهِ مِن شَيْءٍ ۚ قَالُوا لَوْ هَدَانَا اللَّـهُ لَهَدَيْنَاكُمْ ۖ سَوَاءٌ عَلَيْنَا أَجَزِعْنَا أَمْ صَبَرْنَا مَا لَنَا مِن مَّحِيصٍ ﴿٢١﴾

21. Na wanyonge watawaambia wale waliotakabari: "Sisi tulikuwa wafuasi wenu, je mtatuondolea chochote katika adhabu ya Mwenyezi Mungu?" Watasema: "Lau angelituongoza Mwenyezi Mungu tungeliwaongoza, Ni mamoja kwetu tukipapatika au tukisubiri; hatuna pa kukimbilia.

## MATENDO YAO NI KAMA MAJIVU

**Aya 18-21**

### MAANA

Mfano wa wale ambao wamemkufuru Mola wao vitendo vyao ni kama majivu yanayopeperushwa kwa nguvu za upepo katika siku ya kimbunga.

Wafasiri wengi wamesema kuwa makusudio ya Aya ni kwamba kafiri hapati malipo yoyote kwa kufanya jambo jema; kama vile sadaka n.k. Lakini tuoanavyo sisi ni kuwa mwenye kufanya heri kwa msukumo wa kiutu basi atakuwa amefanya kwa jili ya Mwenyezi Mungu awe amekusudia hivyo au la.

Na hakuna mwenye shaka kwamba mwenye kufanya jambo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu kwa vile yeye ni mwadilifu, na hakimu na atamlipa kwa namna yoyote ile; iwe ni duniani au akhera kwa kupunguziwa adhabu; na si lazima kwamba asimwingize motoni kabisa. Hiyo ni kwa sababu neema za Mwenyezi Mungu hazidhibitiwi kwa kiwango wala ki namna. Tumeyazungumzia hayo kwa ufanuzi zaidi tulipofasiri Juz. 4 (3:178).
Kwa hiyo basi, maana ya Aya ni kwamba mtu yeyote atakayefanya matendo ya kheri kwa lengo la kibiashara, sio kibinadamu, kama yule anayefanya mambo ya kheri siku za uchaguzi, basi vitendo vyake huyo si chochote mbele ya Mwenyezi Mungu; sawa na hewa ndani ya wavu au majivu kwenye upepo; ni sawa awe aliyefanya hayo ni Mwislamu au si mwislamu. Imam Ali (a.s) anasema:

**"Fanyeni mambo bila ya ria wala kusikika; kwani anayefanya kwa ajili ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu, basi Mungu Humwachia huyo aliyemfanyia".**

**Unaweza kuuliza**: Ikiwa hukumu inawaenea makafiri na wasiokuwa makafiri kwa nini Aya imetaja makafiri peke yake?
Jibu: Kutajwa makafiri hakukanushi hukumu kwa wengine; isipokuwa wamehusishwa kutajwa hapa kwa kuwa ndio dhahiri zaidi.

Hawana uwezo wa chochote juu ya walichokichumma, Huko ndiko kupotelea mbali.

Walichokichumma ni kwa maana ya walichokifanya. makusudio ya ambao hawana uweza, kimatamshi, ni makafiri na kimaana ni kila mwenye kufanya wema kwa lengo la kibiashara.
Na makusudio yake ni kwamba anayefanya matendo kwa ajili ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu wala kwa ajili ya ubinadamu, hakika yeye hatanufaika kesho kwa amali yake; kwani ni sawa na majivu yanayopeperuka hewani na mwenyewe atakuwa amepotea kwa sababu matendo yake yameepukana na kila sababu inayo muunganisha na Mwenyezi Mungu na ubinadamu.

Je, huoni kuwa Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa haki na akitaka atawaondoa na alete viumbe wapya! Na hilo kwa Mwenyezi Mungu si gumu.

Maana ya je, huoni ni je, hujui. Msemo unaelekezwa kwa kila mwenye kuisoma Qur'an na mwenye kuisikia. Neno 'Haki' linaashiria kuwa Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu, hakuumba kitu chochote isipokuwa kwa hekima iliyopitisha hivyo.

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَاطِلًا ۚ ذَٰلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ ﴿٢٧﴾

"Na hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina ya hizo bure. Hiyo ni dhana ya wale ambao wamekufuru" (38:27).
Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwataja wale wanaofanya matendo kwa asiyekuwa Yeye, hapa anasema kuwa hana haja na watu na matendo yao; na kama angetaka angeliwamaliza wote na kuleta umma mwingine watakaotenda kwa ajili yake peke yake, bila ya kumshirikisha na kitu chochote; kwa sabu Yeye ni muweza wa kila kitu. Hakuna kitu kinachofahamisha zaidi hivyo kuliko kuumba ulimwengu na maajabu yake.

## DHALIMU NA MDHULUMIWA

Na wamehudhuria kwa Mwenyezi Mungu wote.

Limekuja tamko la muda uliopita, lakini makusudio ni muda ujao; yaani watahudhuria. Kwa sababu ni uhakika kuwa litatokea hilo[1]. Maana ni kuwa watu, majini, malaika na mashetani wote hawa watajitokeza mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu siku ya kiyama.

Hakuna yeyote katika wao ila ana yakini kuwa Mwenyezi Mungu ataifichua hakika yake, hata wale wanaomkufuru na kukana ufufuo.

Na wanyonge watawaambia wale waliotakabari: Sisi tulikuwa wafuasi wenu, je mtatuondolea chochote katika adhabu ya Mwenyezi Mungu?

Kila mwenye akili ana majukumu ya matendo yake awe na nguvu au mnyonge, kiongozi au mwenye kuongozwa:

﴿عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾

Naapa kwa Mola wako! Hakika tutawauliza wote yale waliyokuwa wakiyatenda (15:93)

﴿مَّا يَلْفِظُ مِن قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿١٨﴾

“Hata na yale wanayoyasema pia: “Hatamki kauli yoyote ila karibu yake yuko mngojeaji aliye tayari” (50:18).

Kwa hiyo mfuasi ataulizwa: Je, alifuata uongofu au upotevu? Je, aliwafuata na kuwategema wema au wafisadi? Vile vile aliyefuatwa naye ataulizwa, na majukumu yake yake yatakuwa makubwa zaidi, kwa vile ataulizwa kuhusu yeye mwenyewe, kisha aulizwe kuhusu wale waliomfuata: Je, atabeba mizigi yake na mizigo yao?

Mimi sijui kama kuna mwenye mzigo mzito zaidi, kuliko yule aliyefuata na akamsaidia kwenye dhulma, huku akiwa anajua uhakika wake. Hakika dhulama ya dhalimu sio mbaya sana, mbele ya Mwenyezi Mungu, kuliko uvumilivu wa mwenye kudhulumiwa.

Kuuliwa mwenye kudhulumiwa katika kuitetea haki ni kufa shahidi, na mashahidi, wako hai mbele ya Mola wao, wakiruzukiwa.

Dhalimu hathubutu kufanya dhulma ila kwa kunyamaza mdhulumiwa. Lau dhalimu anajua kuwa ndani ya mwili wa anayetaka kumdhulumu kuna nafsi ya ki-Hussein,[2] basi atamwogopa tu.

Kwa vyovyote iwavyo, makusudio ya wanyonge ni wale wadhaifu wa nafsi ambao wanamfuata dhalimu mpotevu huku wakijua dhulma yake na upotevu wake kwa tamaa ya jaha au mali, au woga wa kutaka raha na usalama.

Wanaingia kwenye hukumu hii ya majukumu na hatia wale wanofuata kwa upofu na kufuata mkumbo, marafiki au ndugu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amaeleta picha ya wafuasi wa upotevu, kwa kujua au kwa kutojua kiupofu, siku ya hisabu pamoja na mataghuti kwa namna hiyi:

1. Hata katika kiswahili linatumika; kwa mfano inaweza kusemwa: ‘vile alivyofanya, amekwisha kufa yule’kwa maana ya uhakika wa matokeo ya alivyofanya.

2. Ni kuashiria kauli ya Hussein bin Ali (a.s): “Sioni mauti ila ni wema na sioni kuishi na madhlimu ila ni kubweteka.

Wadhaifu wa nafsi na wa hima watawambia wale viongozi wa dunia na wadanganyifu katika viongozi wa dini: tulikuwa tukifanya kwa amri zenu na tukiacha kwa makatazo yenu; sasa hivi, kama mnavyoona, tuko mbele ya Mwenyezi Mungu hatuna hila wala uwezo, atatuhisabu na kutuadhibu kutokana na kuwatii nyinyi katika kuwakadhibisha mitume na kumwasi Mwenyezi Mungu. Je mtaweza kutukinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu, angalau kidogo?

Watasema: "Lau angelituongoza Mwenyezi Mungu tungeliwaongoza."

Makusudio ya kuongozwa hapa ni kuokoka na adhabu ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu jawabu linakuja kulingana na swali lenyewe.

Wameuliza wafuasi kupunguziwa adhabu na wale wanaowafuata na wao wanajibu kuwa lau tungeliweza kujiokoa basi tungeliwaokoa na nyinyi. Hayo ndio makusudio ya kuongoka hapa; wala hakuna maana nyingine inayoafikiana nayo ila hiyo.

Ni mamoja kwetu tukipapatika au tukisubiri; hatuna pa kukimbilia, kwani kila kitu kimekwisha, hakuna faida ya kujadiliana wala kusutana, kwani hapa tulipo ni nyumba ya hisabu na adhabu si nyumba ya kauli na vitendo.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

وَقَالَ الشَّيْطَانُ لَمَّا قُضِيَ الْأَمْرُ إِنَّ اللَّـهَ وَعَدَكُمْ وَعْدَ الْحَقِّ وَوَعَدتُّكُمْ فَأَخْلَفْتُكُمْ وَمَا كَانَ لِيَ عَلَيْكُم مِّن سُلْطَانٍ إِلَّا أَ ن دَعَوْتُكُمْ فَاسْتَجَبْتُمْ لِي فَلَا تَلُومُونِي وَلُومُوا أَنفُسَكُم مَّا أَنَ ا بِمُصْرِخِكُمْ وَمَا أَنتُم بِمُصْرِخِيَّ إِنِّي كَفَرْتُ بِمَا أَشْرَكْتُمُونِ مِن قَبْلُ إِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَا بٌ أَلِيمٌ ﴿٢٢﴾

22. Na shetani atasema itakapokatwa hukumu: "Hakika Mwenyezi Mungu aliwaahidi ahadi ya kweli nami nikawaahidi sikuwatimizia. Na sikuwa na mamlaka juu yenu, isipokuwa niliwaita mkaniitikia. Basi msinilaumu mimi, bali jilaumuni wenyewe, Mimi siwezi kuwa mtetezi wenu wala nyinyi hamuwezi kuwa watetezi wangu, Mimi nilikataa tangu zamani kunishirikisha, Hakika madhalimu wana adhabu chungu.

وَأُدْخِلَ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ تَحِيَّتُهُمْ فِيهَا سَلَامٌ ﴿٢٣﴾

23. Na wale ambao wameamini na wakatenda mema wataingizwa katika Mabustani (Pepo) ambayo hupita mito chini yake.

## MIADI YA MWENYEZI MUNGU

**Aya 22-23**

### HOTUBA YA SHETANI

Tumezungumzia kwa ufafanuzi kuhusu fikra ya Iblisi na Shetani, mwanzoni mwa Juzuu ya kwanza na katika Juz.5 (4:38) na katika Aya nyingine zinazozungumzia shetani tumezungumzia kwa ujumla.

Hapa tunarudia kwa upana zaidi; kwa sababu Aya tuliyo nayo ndiyo iliyowazi zaidi kuonyesha dalili za kuweko shetani na kwamba ni hakika yenye kuthibiti; ingawaje haikueleza vile alivyo. Tutaeleza njia zinazoambatana na Aya hii, kama ifuatavyo:

1- Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemtaja shetani, katika Kitabu chake Kitakatifu, kwa ibara mbali mbali. Mara nyingine anasema, Mtukufu, kuwa shetani ni katika aina ya watu na majini; kama pale aliposema:

شَيَاطِينَ الْإِنسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا ﴿١١٢﴾

"Mashetani watu na majini Baadhi yao wanawapa wenzao maneno ya kupambapamba kuwahadaa." Juz.8 (6:112).

Aya hii inaashira kwamba kila kauli ambayo dhahiri yake ni rehema na undani wake ni adhabu, basi hiyo ni kazi ya shetani, hata ikiwa imesemwa na nani.

Mara nyingine anasema Mwenyezi Mungu kuwa shetani ana askari na ana kabila; kama ilivyo katika Aya hizi:

وَجُنُودُ إِبْلِيسَ أَجْمَعُونَ ﴿٩٥﴾

"Na majeshi ya ibilisi yote" (26:95)

يَا بَنِي آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمُ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُم مِّنَ الْجَنَّةِ يَنزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْآتِهِمَا إِنَّهُ يَرَاكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ ﴿٢٧﴾

"Enyi wanaadamu! shetani asiwatie katika fitina, kama alivyowatoa wazazi wenu katika Bustani (Pepo) akiwavua nguo zao ili kuwaonyesha tupu zao. Hakika yeye na kabila lake anawaona, na nyinyi hamuwaoni, Juz.8 (7:27).

Aya hizi zinafahamisha kuwa mashetani hawana idadi kwa wingi na kwamba wao hawaonekani kwa macho wala kuguswa kwa mkono.

Mara ya tatu Mwenyezi Mungu anasema mashetani wana marafiki na wasimamizi; kama ilivyo katika Aya hizi:

وَمَن يَكُنِ الشَّيْطَانُ لَهُ قَرِينًا فَسَاءَ قَرِينًا ﴿٣٨﴾

"Na ambaye shetani amekuwa ndiye rafiki yake, basi ana rafiki mbaya, Juz,5 (4:38).

فَقَاتِلُوا أَوْلِيَاءَ الشَّيْطَانِ ﴿٧٦﴾

"Basi piganeni na marafiki wa shetani" Juz.5 (4:76)

Tamko hili peke yake linafahamisha kuwa kupigana jihadi na wapotufu ni lazima na wajib, wajapokuwa ni waislamu. Mara ya nne, Mwenyezi Mungu, ambaye imetukuka hekima yake na maneno yake, anasema:

هَلْ أُنَبِّئُكُمْ عَلَىٰ مَن تَنَزَّلُ الشَّيَاطِينُ ﴿٢٢١﴾ تَنَزَّلُ عَلَىٰ كُلِّ أَفَّاكٍ أَثِيمٍ ﴿٢٢٢﴾

"Je, niwaambie nani wanawashukia Mashetani? Wanamshukia kila mzushi mkubwa mwingi wa dhambi (26: 221-222).

Inafahamisha Aya hii kuwa Mashetani ni wale waongo wazushi.

Ama wadhifa wa shetani na askari wake, kama ulivyoelezwa, ni kupoteza na kudanganya ili kuzuia njia ya haki na kheri, kwa nguvu na kulazimisha; isipokuwa ni kwa wasiwasi, kupambapamba na kudanganya.

Kwa ajili hii, tunasema na tunaendelea kusema kwamba jambo lolote linalompambia mtu kufanya uovu na kumuhimiza shari na ufisadi kwa njia ya hadaa na shauku, basi hilo ni shetani aliyefukuzwa na ibilisi mlaanifu ni sawa iwe ni mtu, mali, jaha, kitabu, gazeti, wasiwasi, mazungumzo ya ndani ya nafsi au kitu chochote kingine kinachoonekana au kisichoonekana.

Hii ndio picha ya shetani iliyoakisi katika akili zetu, tukiwa tunafuatilia na kuzifikiria Aya za Mwenyezi Mungu katika Kitabu chake, tukiziamini pamoja na mitume wa Mwenyezi Mungu.

Mengineyo yasiyokuwa hayo, katika aina na ufafanuzi, tunaiachia elimu ya Mwenyezi Mungu; wala sisi hatukalifiwi nayo au kuulizwa nayo. La wajibu kwetu ni kutohadaika, kutojiingiza katika matamanio na kuacha kuwasikiliza wadanganyifu na wapotevu. Kikitutokea kitu katika hayo, basi tumkumbuke Mwenyezi Mungu kwa ahadi na miadi yake: "Na kama uchochezi wa shetani ukikuchochea, basi jikinge kwa Mwenyezi Mungu; hakika yeye ndiye asikiaye na ajuaye, Hakika wale wanye takua zinapowagusa pepesi za shetani huzinduka, Juz.9 (7:200-201), Rudia huko.

2- Katika nafsi ya binadamu kuna matamanio na silika, navyo ni vitenda-kazi vinavyopelekea kumuasi Mwenyezi Mungu na kuhalifu amri zake, kwa sababu vinakuja kutoka ndani sio nje na kutoka batini sio dhahiri. Kwa hiyo ikiwa ndani mwa mtu hamna nguvu kubwa na ngumu itakayomzuia

kupondokea kwa ashetani na kudhibiti ukaidi wake, basi mtu bila shaka atakuwa amepigwa mwereka na matamanio.

3- Na shetani atasema itakapokatwa hukumu.

Kila kitu, isipokuwa Mwenyezi Mungu, kina mwanzo na mwisho. Inawezekana mwanzo wenyewe ukaonekana, kwa dhahiri, ni heri na mwisho ukaonekana, kiuhakika, ni shari na kinyume chake. Kwa ajili hii haifai kukihukumu kitu kwa dhahiri yake na mwanzo wake, maadamu mwisho wake uko kwenye elimu ya ghaibu.

Watu walimfurahia Qarun alipowatokea na kipambo chake na wakasema: Hakika yeye ni mwema na mtu adhimu. Ardhi ilipommeza yeye na nyumba yake, walisema ni mtu mbaya na muovu.

Dunia ni mwanzo na Akhera ni mwisho. Huko zitafunuka pazia na vifuniko; atajulikana kila mtu mwishilio wake, ambapo hakutakuwa na kombokombo wala kufungwafungwa. Hiyo ndiyo maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Itakapokatwa hukumu'

4- Hakika Mwenyezi Mungu aliwaahidi ahadi ya kweli nami nikaawahidi sikuwatimizia.

Ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ufufuo, hisabu na malipo:

فَوَرَبِّكَ لَنَسْأَلَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٩٢﴾ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾

Kwa haki ya Mola wako! Tutawauliza wote yale waliyokuwa wakiyatenda (15:92-93).

Ama ahadi ya shetani ni kupinga ahadi ya Mwenyezi Mungu kuwa haku- na hisabu wala ufuo wala Pepo na moto. "Hakuna kingine ila maisha yetu ya dunia, wala sisi hatutafufuliwa, Jz.7 (7:29).

Haya ndiyo anayoyasema shetani kuwaambia marafiki zake hapa duniani, palipo na kupindisha pindisha mambo na kudanganya, lakini huko Akhera hakuna kitu isipokuwa haki na uadilifu; hata shetani mwenyewe atajitokeza wazi na uongo wake, akiri mwenyewe kwa kauli yake kuwa mwanzo alikuwa akiwafundisha watu uongo na uzushi.

5- Na sikuwa na mamlaka juu yenu, isipokuwa niliwaita mkaniitikia.

Kabisa! Shetani anakubali mwenyewe kuwa hana uwezo wala nguvu yoyote isipokuwa vitimbi na hadaa. Wala hawamwitikii isipokuwa wale wadhaifu wa akili, nafsi na imani. Kauli yake hiyo shetani ni ile aliyoambiwa na Mwenyezi Mungu:

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ إِلَّا مَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغَاوِينَ ﴿٤٢﴾

Hakika waja wangu wewe hutakuwa na mamlaka nao, isipokuwa wale wapotofu waliokufuata (15:42).

6- Basi msinilaumu mimi, bali jilaumuni wenyewe.

Ikiwa ni ole wake yule aliyekufurishwa na Namrudi, itakuwaje kwa yule aliyekufurishwa na Iblisi? Ikiwa watu wanajilinda na shetani itakuwaje yule anyemtaka huyo shetani amlinde.

Huu ndio mwisho wa yule anayeidharau haki na watu wema kusaidia ufisadi na wafisadi na mwenye kufuata mlio. Tumewaona wengi katika mashetani watu wakiwahadaa walio wadhaifu, wanawaghuri kwa kueneza vurugu. Hata yakiwapata yale waliyoyafanya wenyewe, mashetani wao huwaambia yale yale atakayowaambia Ibilisi wafuasi wake siku ya hisabu na malipo.

7- Mimi siwezi kuwa mtetezi wenu wala nyinyi hamuwezi kuwa watetezi wangu

Yaani shetani kesho atawaambia wafuasi wake: mimi siwatoshelezi na kitu chochte, wala nyinyi pia hamnitoshelezi. Mimi na nyinyi hatuna mawasiliano yoyote.

Mimi nilikataa tangu zamani kunishirikisha.

Ibilisi anawaambia wale wale waliotikia mwito wake: mlinitii katika yale niliyowalingalia, mkanifanya ni mshirika wa Mwenyezi Mungu katika wajibu wa twaa, na mimi ninajiepusha na shirki na yale mliyoyashirikisha; hata kama mtanifanya ni mshirika wa Mwenyezi Mungu.

Hakika madhalimu wana adhabu chungu.

Hii ni jumla nyingine inayoanza, si katika maneno ya Ibilisi, ikiwa na maana ya kutoa miadi. Inawezekana kuwa ni mwishilio wa hotuba ya Ibilisi. Ajabu ni yaliyoelezwa na baadhi ya wafasiri kwamba Ibilisi atatoa hotuba yake hii kwa watu wa motoni kwenye mimbari atakyowekewa huko! Kama ni hivyo basi, itabidi awekewe spika kubwa, kwa sababu wasikilizaji, ambao ni jeshi lake, ni wengi kuliko idadi ya mchanga.

Na wale ambao wameamini na wakatenda mema wataingizwa katika Mabustani (Pepo) ambayo hupita mito chini yake.

Baada ya Mwenyezi Mungu kutaja wapotevu na adhabu yao, sasa anataja waongofu wenye msimamo na malipo yao; kama iilvyo kawaida ya Qur'an. Umepita mfano wake katika Juz. 11 (10:9).

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ اللَّـهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ أَصْلُهَا ثَابِتٌ وَفَرْعُهَا فِي السَّمَاءِ ﴿٢٤﴾

24. Je, hukuona jinsi Mwenyezi Mungu alivyopiga mfano wa neno zuri; kama mti mzuri, mizizi yake ni imara na matawi yake yako mbinguni.

تُؤْتِي أُكُلَهَا كُلَّ حِينٍ بِإِذْنِ رَبِّهَا وَيَضْرِبُ اللَّـهُ الْأَمْثَالَ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٥﴾

25. Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola wake. Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano ili wapate kukumbuka.

وَمَثَلُ كَلِمَةٍ خَبِيثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيثَةٍ اجْتُثَّتْ مِن فَوْقِ الْأَرْضِ مَا لَهَا مِن قَرَارٍ ﴿٢٦﴾

26. Na mfano wa neno ovu ni kama mti muovu uliong'olewa juu ya ardhi, hauna uimara.

يُثَبِّتُ اللَّـهُ الَّذِينَ آمَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ وَيُضِلُّ اللَّـهُ الظَّالِمِينَ وَيَفْعَلُ اللَّـهُ مَا يَشَاءُ ﴿٢٧﴾

27. Mwenyezi Mungu huwaimarisha wale walioamini kwa kauli thabiti katika maisha ya dunia na katika Akhera, na anawapoteza madhalimu; na Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo.

## NENO JEMA NA NENO OVU

**AYA 24-27**

### MAANA

Je, hukuona jinsi Mwenyezi Mungu alivyopiga mfano wa neno zuri, kama mti mzuri.

Imesemekana kuwa maana ya neno zuri hapa ni tamko la Tawhidi: La ilaaha illa llah 'Hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hapana mwenye shaka kuwa Tawhid ndio msingi wa haki na chimbuko lake.

Ni kutokana na Tawhid na ikhlasi ya Mwenyezi Mungu peke yake ndio tunaweza kulifasiri neno zuri kwa kila neno linalowanufaisha watu na kuwapatia kheri na utengeneo kwa namna moja au nyingine; ni sawa liwe ni neno la dini au sharia, elimu au falsafa na hata fasihi na fani. Mtu yeyote ambaye watu watanufaika na kauli yake au kitendo chake atakuwa, kwa upande huu, anakutana na misingi ya Uislamu na dini, kwa namana yoyote atakavyokuwa.

Kauli na neno bora zaidi ni neno la mapinduzi na kelele za hasira mbele ya mtawala jeuri na wale wanaomsaidia, miongoni mwa vibaraka na wanojiweka nyuma. Kwa sababu wao ndio asili ya ugonjwa na chimbuko la balaa.

Amesema Imam Ali (a.s): **"Haikuwa kazi yoyote nzuri na jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu katika kuamrisha mema na kukataza mabaya ila ni kama upumuo katika lindi la bahari na kwamba kuamrisha mema na kukataza maovu hakukurubiwi na ajali wala hakupungukiwi na riziki na bora yake kabisa ni tamko la usawa mbele ya kiongozi jeuri."**

Kwa sababu kiongozi huyo ndio chimbuko la kila uovu; Kwa hiyo mwenye kumkabili na akampinga atakuwa ameupiga vita uovu wote.

Kuna Hadith kadha za Mtume Mtukufu **(s.a.w.w)** zenye maana ya kauli hii ya Imam Ali, Kila kitokacho kwa Ali Amirul-muminin ni miali ya jua la Muhammad bwana wa viumbe wote.

Hakuna kitu kinachofahamisha kuwa makusudio ya neno zuri ni neno lenye faida na manufaa kuliko kufananishwa kwake na mti mzuri ambao mizizi yake ni imara haungolewi na kimbunga na matawi yake yako mbinguni uko mbali na mabalaa ya dunia na uchafu wake.

Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola wake sio kuwa mara nyingine unakuwa mkarimu na mara nyingine unakuwa bakhili; kama mfanya biashara wa nipe nikupe, Huu unatoa tu wakati wote.

Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano ili wapate kukumbuka.

Hufananisha maana ya ndani kwa maana ya dhahiri ili watu wafahamu njia ya uongofu wapate kuifuata na njia ya uongofu wapate kuiepuka.

Na mfano wa neno ovu ni kama mti muovu.

Kila neno linalodhuru watu wala lisiwanufaishe; hilo ni lenye kulaaniwa; ni sawa liwe linatokana na Mwislamu au asiyekuwa Mwislamu; awe wa hali ya juu au mlalahoi. Bali kunyamazia batili kunahisabika ni katika madhambi makubwa. Kuna hadithi inayosema: "Mwenye kunyamazia haki ni shetani bubu."

Ghandi alimwandikia Taghore "Hakika wewe ni mshairi adhimu lakini unacheza na nyumba inaungua ... nyimbo nzuri nzuri hazimshibishi mwenye njaa wala kumponyesha mgonjwa"

Ulion'golewa juu ya ardhi, hauna uimara.

Huu ni mfano sahii kabisa wa batili na watu wake wanojifanya wakubwa na wajinga wakidhaniwa kuwa wao ni watu wazito kumbe ni kama mti tu uliosimama bila ya mizizi, mara moja unaweza ukalala chini unapopigwa na upepo.

Mwenyezi Mungu huwaimarisha wale walioamini kwa kauli thabiti katika maisha ya dunia na katika Akhera.

Makusudio ya wale walioamini sio waliosema tumemwamini Mungu na siku ya mwisho tu, kisha wasiisimamishe haki na kuipinga batili; isipokuwa makusudio ya wale walioamini ni wale aliowakusudia Mwenyezi Mungu katika kauli yake: “Hakika waumini ni wale tu walio mwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho; kisha wasiwe na sahaka na wakapigania njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao” (49:15)

Lakini wakidai tu kumwamini Mwenyezi Mungu kisha wasiizuie dhulma na ufisadi kwa ushujaa, basi hao ni wenye shaka sio waumini.

Maana ya kuwaimarisha kwa kauli thabiti katika maisha ya dunia ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewapa habari katika Kitabu chake kupitia Mtume wake kuwa wao wako katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu na kwamba Yeye ndiye mlezi wao na msimamizi wao, mwenye kuwahifadhi na kuwanusuru; kama alivyo washujaisha na kuwasifu kwa ukweli na ikhlasi na mengineyo katika fadhila. Ama kuwaimarisha katika maisha ya akhera kwa kauli thabiti ni kauli YakeMwenyezi Mungu:

يَا عِبَادِ لَا خَوْفٌ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ وَلَا أَنتُمْ تَحْزَنُونَ ﴿٦٨﴾

Enyi waja wangu! Hamna hofu leo wala nyinyi si wenye kuhuzunika” (43:68).

Na anawapoteza madhalimu kwa kufuru yao na utwaghuti wao.

Mara nyingi Qur’an hutumia neno dhulma kwa maana ya kufuru na shirki, lakini makusudio ya dhulma hapa ni kuidhulumu mtu nafsi yake kwa kufuru na kumdhulumu mwingine kwa uadui na uzushi; kama ambavyo makusudio ya upotevu hapa ni adhabu; sawa na kauli yake Mwenyezi Mungu:

كَذَٰلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ مُّرْتَابٌ ﴿٣٤﴾

Hivyo ndivyo humpoteza Mwenyezi Mungu yule aliyepita kiasi mwenye shaka (40:34).

Na Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo katika kumpa thawabu mtiifu na kumwadhibu mfisadi, wala hakuna mwenye kuzuia matakwa yake.

Nikiwa kwenye tafsiri ya Aya hii, nimesoma makala katika gazeti la Al-Ahram la Misr la tarehe 2, February 1969, yenye kichwa cha maneno: “Je ubinadamu utashuhudia kummalizika vita vya Atomic na kuanza vita vya sumu?” Miongoni mwa yaliyomo katika makala hiyo ni: “Imejitokeza silaha mpya hatari zaidi na yenye nguvu kulio silaha za nyuklia.

Silaha hiyo ni ya sumu na kwamba athari yake ni mtu anapoigusa chembe tu, basi viungo vyake vinanywea, macho yanamtoka na kufa papo hapo. Na kwamba Amerika na Uingereza tayari ina viwanda vya kutengeneza silaha hizi na kuzihifadhi mpaka pale zitakapohitajika. Wakati mataifa yakitafuta muafaka wa kummaliza silaha za nyuklia, huku mataifa mawili haya yanatafuta silaha hatari zaidi, kama badili ya mabomu ya Atomic na Haidrojeni.”

Je, imani inaweza kuwa pamoja na nia na maazimio ya kutumia silaha hizi? Je swala za wale wanaowaunga mkono wenye nia hizo na maazimio hayo zitawafaa mbele ya Mwenyezi Mungu?

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ ﴿٢٨﴾

28. Je, hukuwaona wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru? Na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamivu?

جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا وَبِئْسَ الْقَرَارُ ﴿٢٩﴾

29. Nayo ni Jahannam watakayoiingia, Ni mahala pabaya pa kukaa.

وَجَعَلُوا لِلَّـهِ أَندَادًا لِّيُضِلُّوا عَن سَبِيلِهِ قُلْ تَمَتَّعُوا فَإِنَّ مَصِيرَكُمْ إِلَى النَّارِ ﴿٣٠﴾

30. Na walimfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili wapoteze katika njia yake, Sema: Stareheni! Kwani hakika marejeo yenu ni motoni.

قُل لِّعِبَادِيَ الَّذِينَ آمَنُوا يُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُنفِقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً مِّن قَبْلِ أَن يَأْتِيَ يَوْمٌ لَّا بَيْعٌ فِيهِ وَلَا خِلَالٌ ﴿٣١﴾

31. Waambie waja wangu walioamini wasimamishe Swala na watoe katika tulivyowaruzuku kwa siri na kwa dhahiri, kabla ya kuwajia siku isiyokuwa na biashara wala urafiki.

## WALIBADILISHA NEEMA YA MUNGU KWA KUFURU

**Aya 28 -31**

### MAANA

Je, hukuwaona wale waliboadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru? Na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamivu? Nayo ni Jahnnam watakayoiingia ni mahala pabaya pa kukaa.

Dhamiri ya wakawafikisha inawarudia viongozi wa kufuru na upotevu. Makusudio ya neema ya Mwenyezi Mungu ni imani na uwongofu. Maana ni kuwa, je, hustajabu ewe Muhammad au ewe msikilizaji na msomaji, hali ya viongozi wa kufuru na upotevu ambao wamehiyari upotevu kuliko uongofu na moto kuliko neema, wakiingia humo wao na wafuasi wao, wakawa ndio kuni zake.

Mfano wa Aya hii ni kama kauli yake Mwenyezi Mungu:

أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ اشْتَرَوُا الضَّلَالَةَ بِالْهُدَىٰ فَمَا رَبِحَت تِّجَارَتُهُمْ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿١٦﴾

"Hao ndio walionunua upotofu kwa uongofu, lakini biashara yao haikupa- ta faida wala hawakuwa ni wenye kuongoka." Juz.1 (2:16)

Tabariy amenukuu, katika kufasiri Aya hii, kwamba Umar bin Al-Khatab alisema: "Wale ambao wamebadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru ni koo mbili ovu katika maqurayshi: Bani Mughira na Bani Umayya. Ama Bani Mughira mliwatosha siku ya Badr na Bani Umayya watajifurahisha muda mchache tu."

Na walimfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili wapoteze katika njia yake.

Walimfanyia Mwenyezi Mungu washirika, wakiwapenda kama kumpenda Mungu na kuwaabudu kama kumwabudu Mungu.

Ilivyo hasa ni kuwa wao walifanya hivyo kwa kukusudia kuongoka si kwa kukusudia kupoteza njia. Kwa hiyo neno kwa 'ili' hapa halina maana ya kuwa ndio lengo bali ni matokeo. Maana yanakuwa kwamba washirikina waliabudu masanamu kwa kukusudia kuongoka nayo na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, lakini natija ikawa ni kupotea, kuangamia na kuwa mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu. Neno 'ili' hapa liko sawa na mfano wa kusema: Amekuja mwenyewe ili afe.

Sema: Stareheni! Kwani hakika marejeo yenu ni motoni.

Mwenyezi Mungu alimwamrisha mtume wake kuwahadharisha washirikina na mwisho mbaya na kuwaambia kuwa starehe za dunia ni chache hata kama zinawapendeza na Akhera ni ya mwenye takua. Lakini lugha ya haki inafaa kitu kwa wale ambao hawatingishwi na lolote zaidi ya faida na chumo?

Waambie waja wangu walioamini wasimamishe Swala ambayo mwenye kuiswali inamkumbusha Mungu na kumhadharisha na adhabu na mateso na kumkataza dhambi na makosa

Na watoe katika tulivyowaruzuku kwa siri na kwa dhahiri.

Zaka ni ndugu yake swala. Swala inamkumbusha Mungu na zaka inamkurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Umepita mafano wake katika Juz 3 (2:74).

Kabla ya kuwajia siku isiyokuwa na biashara wala urafiki.

Biashara hapa ni fumbo la fidia. Maana ni kuwa mwenye kutoa mali yake katika njia ya Mwenyezi Mungu atanufaika nayo huko akhera na mwenye kuifanyia ubakhili atakuwa na hasara na adhabu wala haitamfaa siku hiyo ambapo hakutakuwa na fidia wala urafiki, Umepita mfano wake katika Juzuu hii tuliyo nayo (13:18).

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

اللَّـهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَأَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَّكُمْ وَسَخَّرَ لَكُمُ الْفُلْكَ لِتَجْرِيَ فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ وَسَخَّرَ لَكُمُ الْأَنْهَارَ ﴿٣٢﴾

32. Mwenyezi Mungu ndiye ambaye ameziumba mbingu na ardhi na akateremsha maji kutoka mbinguni. Na kwayo akatoa matunda kuwa riziki kwa ajili yenu. Na akafanya yawatumikie majahazi yanayopita baharini kwa amri yake, na akaifanya mito iwatumikie.

وَسَخَّرَ لَكُمُ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ دَائِبَيْنِ وَسَخَّرَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ ﴿٣٣﴾

33. Na akalifanya liwatumikie Jua na Mwezi daima. Na akaufanya usiku na mchana uwatumikie.

وَآتَاكُم مِّن كُلِّ مَا سَأَلْتُمُوهُ وَإِن تَعُدُّوا نِعْمَتَ اللَّـهِ لَا تُحْصُوهَا إِنَّ الْإِنسَانَ لَظَلُومٌ كَفَّارٌ ﴿٣٤﴾

34. Na akawapa kila mlichomuomba, Na mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu hamuwezi kuzidhibiti. Hakika mtu ni dhalimu mkubwa mwingi wa kukufuru.

## NA AKATEREMSHA MAJI KUTOKA MBINGUNI

**Aya 32 -34**

### MAANA

Aya zote hizi tatu umepita mfano wake kama ifuatavyo:
Kuumbwa mbingu na ardhi: Juz. 7 (6:73).
Kutermshwa maji kutoka mbinguni: Juz. 1 (2:22) na Juz. hii tuliyo nayo (13:18).
Kupita majahazi: Juz. 2 (2:164).
Kunufaika na Jua na Mwezi: Juz. hii (13:2). Usiku na mchana Juz. 11(10: 67).

Mwenyezi Mungu ameweka idadi ya neema nyingi kwa waja wake katika Juz. hii na Juz. 8 (6:143144) na nyinginezo nyingi zilizokwisha tangulia pamoja na tafsiri yake na ufafanuzi wake. Mwenyezi Mungu amerudia hapa au kuzidokeza kwa mnasaba wa kubadilisha neema kwa kufuru.

Kwa ufupi Aya hizi tatu zinamaanisha kuwa neema za Mwenyezi Mungu hazihisabiki; kama vile kuumbwa mbingu na ardhi, kuteremshwa maji kuenda majahazi faida za jua, mwezi, usiku na mchana. Vile vile kuwafadhili watu kwa waliyoomba na wasiyoomba, lakini pamoja na neema zote hizo wengi wanamkufuru na kuzikufuru neema zake huku wakiabudu yasiyowanufaisha wala kuwadhuru.

### JE MTU ANA MAUMBILE YA HATIA?

Kwa mnasaba wa kauli yake Mwenyezi Mungu: Hakika mtu ni dhalimu mkubwa mwingi wa kukufuru, tunadokeza kwamba wataalamu wa saikolojia wametofautiana kuhusu binadamu, kuwa je, ana maumbile ya kufanya hatia, kwamba yeye amezaliwa kumfanyia uadui ambaye

hajamfanyia uadui na kukufuru neema za aliyemfanyia wema (hana shukrani)
Mnamo mwaka 1832 watalamu 528 walikutana huko Amerika wakilijadili suala hili, Wengi wakaonelea kuwa hakuna dalili kuwa mwanadamu anaweza kuepuka kufanya makosa, lakini kundi jingine likapinga.
Sisi tunaamini kuwa binadamu hakuzaliwa kuwa ni mwenye kufanya makosa; vinginevyo angelikuwa hana taklifa yoyote na kuhisabiwa kwake na kuadhibiwa ingelikuwa ni dhulma na uonevu. Vile vile dini na sharia ingelkiuwa ni upuzi na mchezo; kama vile unyoya kwenye mavumo ya upepo. Isipokuwa anakuwa ni mwenye hatia kwa sababu nyingine za nje; kama vile njaa inayofanya awe mwizi, hadaa zinazomfanya awe na hiyana na kuwa kibaraka n.k.
Hapa ndio unapata tofauti baina ya watu katika nafsi zao, Wengine wanakuwa dhaifu mbele ya hadaa na kushindwa na matamnio; kama vile mwenye chakula lakini bado anataka ziada tena kwa hali yoyote; au mwenye mke anayemtosheleza, lakini anazini; au anayeificha haki kwa kupupia cheo au manufaa yoyote katika starehe za dunia. Hakuna mwenye shaka kwamba huyu amefanya dhambi kwa kutaka kwake sio kwa maumbile yake. Hayo ndiyo aliyoyakusudia Mwenyezi Mungu aliposema:
Hakika mtu ni dhalimu mkubwa mwingi wa kukufuru.
Ni wazi kuwa kupondokea haramu hakuifanyi kuwa ni halali, madamu iko nafasi ya kuweza kufanya subira na kushinda mapondokeo haya. Tumetangulia kueleza yanayoambatana na utafiti huu katika kufasiri Juz. 12 (11:9).

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَـٰذَا الْبَلَدَ آمِنًا وَاجْنُبْنِي وَبَنِيَّ أَن نَّعْبُدَ الْأَصْنَامَ ﴿٣٥﴾

35. Na Ibrahim aliposema: Ewe Mola wangu! Ujaalie mji huu uwe wa amani na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu.

رَبِّ إِنَّهُنَّ أَضْلَلْنَ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ فَمَن تَبِعَنِي فَإِنَّهُ مِنِّي وَمَنْ عَصَانِي فَإِنَّكَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ
﴿٣٦﴾

36. Ewe Mola wangu! Hakika hayo yamewapoteza watu wengi, Basi atakayenifuata, hakika huyo ni katika mimi na atakayeniasi basi hakika wewe ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

رَّبَّنَا إِنِّي أَسْكَنتُ مِن ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيْرِ ذِي زَرْعٍ عِندَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُوا الصَّلَاةَ فَاجْعَلْ
أَفْئِدَةً مِّنَ النَّاسِ تَهْوِي إِلَيْهِمْ وَارْزُقْهُم مِّنَ الثَّمَرَاتِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ ﴿٣٧﴾

37. Ewe Mola wetu! Hakika mimi nimeweka baadhi ya dhuria zangu katika bonde lisilokuwa na mmea, kwenye nyumba yako takatifu, ewe Mola wetu, ili wasimamishe Swala. Basi zijaalie nyoyo za watu zielekee kwao na uwaruzuku matunda ili wapate kukushukuru.

رَبَّنَا إِنَّكَ تَعْلَمُ مَا نُخْفِي وَمَا نُعْلِنُ وَمَا يَخْفَىٰ عَلَى اللَّـهِ مِن شَيْءٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ
﴿٣٨﴾

38. Ewe Mola wetu! Hakika wewe unajua tunayoyaficha na tunayoyafichua, na hapana kitu kinachofichikana mbele ya Mwenyezi Mungu katika ardhi wala mbingu.

﴿الْحَمْدُ لِلَّـهِ الَّذِي وَهَبَ لِي عَلَى الْكِبَرِ إِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ ۚ إِنَّ رَبِّي لَسَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٣٩﴾

39. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliyenipa juu ya uzee wangu Ismail na Is-haq. Hakika Mola wangu ni mwenye kusikia sana dua.

رَبِّ اجْعَلْنِي مُقِيمَ الصَّلَاةِ وَمِن ذُرِّيَّتِي ۚ رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَاءِ ﴿٤٠﴾

40. Ewe Mola wangu! Nijaalie niwe mwenye kuisimamisha Swala na katika dhuria zangu pia. Ewe Mola wetu! Na utakabalie dua yangu.

رَبَّنَا اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ الْحِسَابُ ﴿٤١﴾

41. Ewe Mola wetu! Nighufirie mimi na wazazi wangu wawili na waumini siku ya kusimama hisabu.

## EWE MOLA WANGU UJAALIE MJI HUU UWE WA AMANI

**AYA 35-41**

Na Ibrahim aliposema: Ewe Mola wangu! Ujaalie mji huu uwe wa amani.

Ibrahim na Ismail ndio waliojenga Al-ka'ba Makka. Angalia Juz. 1 (2:127).

Ibrahim na Ismail walimwomba Mola wao awajalie watu wawe na amani, na akawaitikia dua yao. Walikuwa na wanaendelea kuwa maadui wanakutana bila ya kuhofiana. Katika hili Mwenyezi Mungu ameashiria kwa kusema:

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا جَعَلْنَا حَرَمًا آمِنًا وَيُتَخَطَّفُ النَّاسُ مِنْ حَوْلِهِمْ ﴿٦٧﴾

"Je hawaoni kuwa tumeifanya nchi takatifu iwe ya amani na hali watu wengine wananyakuliwa kwa majirani zao? " (29:67)

Na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu.

Ni muhali kabisa kwa Ibrahim kuabudu masnamu. Itakuwaje ayaabudu naye aliyavunja kwa mikono yake na akawaambia:

أُفٍّ لَّكُمْ وَلِمَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ ۖ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾ قَالُوا حَرِّقُوهُ وَانصُرُوا آلِهَتَكُمْ إِن كُنتُمْ فَاعِلِينَ ﴿٦٨﴾

Je, mnaabudu badala ya Mwenyezi Mungu yasiyofaa chochote wala kuwadhuru, Kefle yenu! Na mnavyoviabudu badala ya Mwenyezi Mungu, Je, hamtii akili? (21:67-68).

lakini mitume wa Mwenyezi Mungu na manabii wake – pamoja na isma yao – wanaogopa maasi, Hofu hii ndiyo daraja ya juu ya utiifu. Anayejiona ni mtakatifu basi amemfungulia shetani madirisha.

### MITUME NA KUITIKIWA DUA

**Unaweza kuuliza**: kuwa Ibrahim alimuomba Mola wake kuwa watoto wake wawe waumini, asimshirikishe Mwenyezi Mungu hata mmoja wao; na inajulikana kuwa wengi katika kizazi chake walimshirikisha Mwenyezi Mungu, wakaabudu masanamu, wakiwemo maquraish ambao wao ni katika kizazi chake?

Razi amenukuu majibu matano kutoka kwa wafasiri, lakini bado swali liko palepale linataka jawabu.

Tuonavyo sisi ni kuwa dua ni maombi na matarajio; ni sawa iwe inatoka kwa Nabii au mwinginewe. Inaweza kuwa hekima yake Mwenyezi Mungu

inataka kuyakubali maombi na wakati mwingine kuyakataa. Wala hiyo haimaanishi kuwa aliyekataliwa maombi hana uzito wowote mbele ya Mungu kuweza kudhuru cheo cha utume na isma yake.

Hapana! Kwani kukataliwa maombi hakummaanishi hasira za mwenye kuombwa kwa muombaji; bali inawezekana kuwa ni mapenzi zaidi kwake na kuchunga masilahi yake. Nuhu (a.s) alimtaka Mwenyezi Mungu kumuokoa mtoto wake kutokana na kuangamia, Mola wake akamjibu kwa kusema: “Basi usiniombe usilo na ujuzi nalo” Juz.12 (11:46).

Kwa maneno mengine ni kuwa dua ya Nabii Ibrahim haina tafsiri nyingine zaidi ya hamu yake na mapenzi. Hakuna mwenye shaka kwamba manabii wana hamu na wanapendelea watu wote waamini na waongoke kwenye haki. Pamoja na hayo Mwenyezi Mungu alimwambia Bwana wa mitume aliyeadhimu:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَـٰكِنَّ اللَّـهَ يَهْدِي مَن يَشَاءُ ﴿٥٦﴾

Hakika wewe huwezi kumwongoza umpendae, lakini Mwenyezi Mungu humuongoza amtakaye (28:56)

Lau yangehakikia kila wanayoyataka mitume basi asingelipatikana hata kafiri mmoja duniani na mitume wasingelisumbuka; hasa yule bwana wao na wa mwisho wao ambaye alisema: “Hakuudhiwa mtume kama nilivyoudhiwa mimi”

Ewe Mola wangu! Hakika hayo yamewapoteza watu wengi.

Makusudio ya hayo ni ya masanamu. Maana ni kuwa wengi katika watu wamepotea kwa sababu ya ibada ya masanamu; sawa na kusema: mali imempoteza fulani; yaani amepotea kwa sababu yake.

Basi atakayenifuata, katika kizazi changu, hakika huyo ni katika mimi kinasabu na kidini. Na atakayeniasi basi hakika wewe ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

Atakayemuasi Ibrahim (a.s) basi yuko mbali naye sana hata kama ndiye aliyekaribu zaidi kiudugu kuliko watu wengine; Kwa sababu atakayemuasi atakuwa amemuasi Mwenyezi Mungu.

Lakini, pamoja na hayo, Ibrahim ni mpole mno mwenye kurudi kwa Mwenyezi Mungu; kama alivyomsifu yule aliyemchagua kuwa kipenzi na akamtakasa. Ndio maana hakuwatakia adhabu waasi katika kizazi chake, bali alimwachia Mwenyezi Mungu mambo yao kwa masamaha wake na maghufira yake.

Ilivyo ni kuwa akili haizuwii kusamehewa washirikina, kwa sababu adhabu ya washirikina ni haki ya Mwenyezi Mungu. Akitaka atwaadhibu na akitaka atawasamehe. Ama kauli yake Mwenyezi Mungu: “Hakika Mwenyezi Mungu hasamei kufanyiwa mshirika, lakini husamehe yasiyokuwa hayo” Juz.5 (4:48), ni dalili ya kiusikilizaji si dalili ya kiakili, Angalia tafsiri yetu huko, tumefafanua zaidi.

Ewe Mola wetu! Hakika mimi nimeweka baadhi ya dhuria zangu katika bonde lisilokuwa na mmea, kwenye nyumba yako takatifu, ewe Mola wetu, ili wasimamishe Swala.

Aliyasema haya Ibrahim (a.s) pale alipomwacha Ismail na mama yake Makka, pakiwa ni bonde kavu, halina chochote, si maji wala mmea; isipokuwa nyumba tu inayosimamishwa swala ndani yake na kukaririwa talbiya. Ni kwa lengo hili Ibrahim aliiweka baadhi ya famila yake mahali

hapa pa kame. Lakini binadamu haishi kwa swala peke yake, bali hana budi apate mkate vile vile, ndipo Ibrahim akasema:

Basi zijaalie nyoyo za watu zielekee kwao na uwaruzuku matunda ili wapate kukushukuru.

Ikiwa kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu hakuna mmea wala kiwele, basi watu waelekee huko kwa ibada au biashara wakiwa na mkate na matunda, ili familia ya Ibrahim nayo ipate kula na kuweza kuswali na kushukuru.

Musa (a.s) alisema: "Mola wangu! Hakika mimi ni muhitaji wa heri utakyoiteremsha" (28:24). Imam Ali (a.s) anasema: **"Wallahi hakumuomba isipokuwa mkate atakokula"** Alisema mshairi aliye faqih: Fadhila ni za mkate lau si huo kamwe hata siku hakuna aabaduo.

Ewe Mola wetu! Hakika wewe unajua tunayoyaficha na tunayoyafichua, na hapana kitu kinachofichikana mbele ya Mwenyezi Mungu katika ardhi wala mbingu.

Baada ya Ibrahim kuuomba watu wafike nyumbani kwake wakiwachukulia familia yake mkate na matunda ili wapate nguvu na uchangamfu wa kuabudu, baada ya haya alisema maombi yangu haya si lolote ila ni unyenyekevu na kukiri kuwa wewe ni Muumba Mwenye kuruzuku. Ama haja yetu na masilahi yetu wewe unayajua zaidi kuliko sisi; tuwe tumekuomba au hatukuomba.

Kwa hiyo kauli ya Ibrahim 'tunayofichua' maana yake ni tunayoyaomba na maana ya 'tunayoyaficha' ni yale tusiyoyaomba.

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliyenipa juu ya uzee wangu Ismail na Is-haq. Hakika Mola wangu ni mwenye kusikia sana dua.

Shukrani hii kutoka kwa Ibrahim imechanganya maombi ya msaada wa Mwenyezi Mungu kwa wanawe, Ismaili na Is-haq. Kwa vile Ibrahim amekwishakuwa mzee na muda wake umekurubia, ndipo akawakilisha mambo ya familia yake kwa Mwenyezi Mungu; wala hakuwabainishia kitu au kuwalimbikizia mali watoto wake ili wastarehe na kuwanyima wengine.

Ewe Mola wangu! Nijaalie niwe mwenye kuisimamisha Swala na kati- ka dhuria zangu pia. Ewe Mola wetu! Na utakabalie dua yangu.

Swala ya Ibrahim sio aina ya hii swala tunayoiswali sisi; bali ni katika aina ya swala amabyo Mwenyezi Mungu ameiainisha kwa kusema:

﴿إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنكَرِ ﴿٤٥

Hakika Swala huzuia mambo machafu na maovu (29:45).

Ndio hapa mafakihi wakaigawanya swala katika mafungu mawili: Swala ya kutekeleza wajibu tu, lakini mtekelezaji halipwi kitu; na Swala ya kutekeleza wajibu na mtekelezaji analipwa. Hiyo ni ile ambayo inaleta ikhlasi katika matendo na ukweli katika kuamiliana na watu.

Ewe Mola wetu! Nighufirie mimi na wazazi wangu wawili na waumini siku ya kusimama hisabu.

Tumetangulia kueleza katika Juz, 7 (6:74) tofauti baina ya Sunni na Shia kuhusu imani ya baba wa Ibrahim Al-khalil (a.s). Miongoni mwa tuliyoyasema ni kuwa mzozo huu na mfano wake ni tasa, na kwamba linalotakikana kwa Mwislamu ni kuitakidi isma ya mitume, Ama kuamini kuwa mababa zao walikuwa waumini si itikadi ya uislamu kabisa.

Lau mtu atasema mimi ninamwamini Mungu na umoja wake, mitume na isma yao na siku ya mwisho na hisabu, lakini sithibitishi wala si kanushi imani ya mababa wa Mitume, Atakayesema hivi, tutamwambia kuwa wewe ni Mwislamu, unastahiki wanyostahiki waislamu nawe unawajibu wa kuwafanyia wanayostahiki waislamu wenzako.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّـهَ غَافِلًا عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ ۚ إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ الْأَبْصَارُ ﴿٤٢﴾

42. Wala usidhani kuwa Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayoyafanya madhalimu, Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku yatakapokodoka macho.

مُهْطِعِينَ مُقْنِعِي رُءُوسِهِمْ لَا يَرْتَدُّ إِلَيْهِمْ طَرْفُهُمْ ۖ وَأَفْئِدَتُهُمْ هَوَاءٌ ﴿٤٣﴾

43. Nao wako mbioni, vichwa vyao viko juu, macho yao hayapepesi na nyoyo zao ni tupu.

وَأَنذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ الْعَذَابُ فَيَقُولُ الَّذِينَ ظَلَمُوا رَبَّنَا أَخِّرْنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ نُّجِبْ دَعْوَتَكَ وَنَتَّبِعِ الرُّسُلَ ۗ أَوَلَمْ تَكُونُوا أَقْسَمْتُم مِّن قَبْلُ مَا لَكُم مِّن زَوَالٍ ﴿٤٤﴾

44. Na waonye watu siku itakapowajia adhabu na waliodhulumu waseme: Ewe Mola wetu! tuakhirishe muda kidogo tutaitikia wito wako na tutafuata mitume, Je, hamkuwa mmeapa tangu zamani kuwa nyinyi hamtaondolewa?

وَسَكَنتُمْ فِي مَسَاكِنِ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ وَتَبَيَّنَ لَكُمْ كَيْفَ فَعَلْنَا بِهِمْ وَضَرَبْنَا لَكُمُ الْأَمْثَالَ ﴿٤٥﴾

45. Na mkakaa katika maskani za wale waliodhulumu nafsi zao? Na ikawabainikia jinsi tulivyowafanya na tukawapigia mifano?

## DHALIMU ANAJISAHAU LAKINI HASAHAULIWI

**Aya 42-45**

### MAANA

Wala usidhani kuwa Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayoyafanya madhalimu, Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku yatakapokodoka macho.

Dhulma ni aina nyingi: Kufru na shirki ni dhulma na kuikeuka haki miongoni mwa haki za watu ni dhulma; ni sawa iwe ni haki ya kitu au hali; hasa ikiwa anayenyanganywa haki yake ni dhaifu.

Kwa sababu kumdhulumu dhaifu ni uovu mbaya zaidi. Na mwenye kumsaidia dhalimu, kuridhia vitendo vyake au kumnyamazia na huku uwezo anao angalau kumtangaza, basi huyo atakuwa mshirika wake. Ni kwa ajili hii ndio Mwenyezi Mungu haghafiliki na wanayoyafanya madhalimu.

Tumezungumzia dhulma katika kufasiri mwanzo wa Juz.6 (4:148). Tukiunganisha tuliyoyasema huko na hapa ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakutuma mitume wala kuteremsha Vitabu isipokuwa ni kwa kupiga vita dhulma na madhalimu. Mwenyezi Mungu amejisifu katika Kitabu chake kuwa Yeye ni mwenye kuadhibu. Lau si dhulma, wasifu huu usingekuwa na athari yoyote.

Kadiri dhulma inavyozidi muda wake ndivyo adhabu yake inavyokuwa kubwa na kali zaidi. Imam Ali anasema: “Mwenyezi Mungu atamwadhibu mwenye kudhulumu tonge kwa tonge na tamaa kwa tamaa”. Mwenye kumdhulumu mtu kwa neno moja tu malipo yake ni makomeo ya chuma,

basi itakuwaje kwa yule aliyeigeuza ardhi kuwa moto na akaweka kambi ya jeshi kila mahali na maghala ya silaha za maangamizi?

Nao wako mbioni, vichwa vyao viko juu, macho yao hayapepesi na nyoyo zao ni tupu.

Wamekodoa macho kwa sababu ya mshangao na wanafanya haraka kuitikia mwito wa anayeita, wamenyanyua vichwa kwa mshangao. Ama nyoyo zao hazina hisia kutokana na hofu. Hivi ndivyo itakavyolipwa kila nafsi kutokana na iliyoyachuma.

Na waonye watu siku itakapowajia adhabu na waliodhulumu waseme: Ewe Mola wetu! tuahirishe muda kidogo tutaitikia wito wako na tutafuata mitume.

Mwenyezi Mungu aliwatuma manabii na mitume wake kwa waja wake watoe bishara ya thawabu na watoe onyo la adhabu. Watu walikuwa na wakati mwingi wa kupewa bishara na onyo, lakini watu wengi walikataa na kupinga, wakawaambia mitume wao: kweli, kuna kufa, kufufuliwa, kisha kukusanywa! Hizi ni ngano tu za watu wa kale. Mpaka watakaposimama mbele ya Mola Mwenyezi Mungu na pazia likiwafunukia watasema: ewe Mola wetu tupe muda kidogo tuweze kuwasikiliza mitume wako na tuwatii, Watasema haya ikiwa hakuna wakati tena.

Mwenyezi Mungu alimwamrisha mtume wake Muhammad **(s.a.w.w)** kuwapa hadhari washirikina na kuwaonya na siku hii, ambayo haina kuahirisha wala kurudi nyuma, kabla haijawafikia.

Na kuwapa habari ya matokeo kama wakiendelea na inadi; na kwamba wao watamwambia Mwenyezi Mungu: Tuahirishie ili tuitikie wito wa mitume, lakini wapi! Mtume amekwishatekeleza ujumbe wa Mola wake akawapa bishara na akawahadharisha, lakini manufaa na tamaa iliwashinda, wakawa miongoni mwa watu waliohasirika.

Je, hamkuwa mmeapa tangu zamani kuwa nyinyi hamtaondolewa? Na mkakaa katika maskani za wale waliodhulumu nafsi zao? Na ikawabainikia jinsi tulivyowafanya na tukawapigia mifano?

Maneno haya yote Mwenyezi Mungu kesho atawaambia wale waliokadhibisha ambao watamwambia Mwenyezi Mungu turudishe mara ya pili duniani ili tuwafuate mitume. Atawajibu, Yule ambaye limetukuka neno lake, kwa kuwauliza swali la kusuta, kuwa nyinyi si mliapa duniani kuwa hakuna kuondoka katika maisha ya dunia kwenda maisha ya Akhera na kwamba hakuna pepo wala moto.

Ameyadokeza hayo Mwenyezi Mungu katika Aya nyingine kwa kusema:

وَأَقْسَمُوا بِاللَّـهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَا يَبْعَثُ اللَّـهُ مَن يَمُوتُ ﴿٣٨﴾

Na wanaapa ukomo wa viapo vyao kwamba Mungu hatamfufua afaye (16:38).

Baada ya swali hili au masuto haya, Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaendelea kuwaambia kuwa mnajua hali ya mwanzo jinsi tulivyowaangamiza walioasi, tukawahadharisha msifate vitendo vyao na tukawapigia mifano yao wala hamkuwaidhika na mkazingatia.

Hivi sasa ambapo hakuna kurejea wala kuakhirishwa, sasa mnasema tungojee kidogo, ni mantiki gani haya? Je si Mwenyezi Mungu aliwaletea mitume mkawachezea mpaka mrudishwe mara ya pili na mtumiwe mitume wengine wapya?

وَقَدْ مَكَرُوا مَكْرَهُمْ وَعِندَ اللَّـهِ مَكْرُهُمْ وَإِن كَانَ مَكْرُهُمْ لِتَزُولَ مِنْهُ الْجِبَالُ ﴿٤٦﴾

46. Na kwa hakika wamekwishafanya vitimbi vyao na vitimbi vyao viko kwa Mwenyezi Mungu, ingawa vitimbi vyao vinaweza kuondosha mlima.

فَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّـهَ مُخْلِفَ وَعْدِهِ رُسُلَهُ ۚ إِنَّ اللَّـهَ عَزِيزٌ ذُو انتِقَامٍ ﴿٤٧﴾

47. Basi usimdhanie Mwenyezi Mungu kuwa ni mwenye kuwavunjia ahadi yake mitume wake. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kushinda, Mwenye kulipiza kisasi.

يَوْمَ تُبَدَّلُ الْأَرْضُ غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَاوَاتُ ۖ وَبَرَزُوا لِلَّـهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿٤٨﴾

48. Siku itakapobadilishwa ardhi kuwa ardhi nyingine na mbingu (pia), Nao watahud- huria mbele ya Mwenyezi Mungu mmoja, Mwenye nguvu.

وَتَرَى الْمُجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ مُّقَرَّنِينَ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٤٩﴾

49. Na utawaona wahalifu siku hiyo wamefungwa katika minyororo.

سَرَابِيلُهُم مِّن قَطِرَانٍ وَتَغْشَىٰ وُجُوهَهُمُ النَّارُ ﴿٥٠﴾

50. Nguo zao zitakuwa za lami na moto utazigubika nyuso zao.

لِيَجْزِيَ اللَّـهُ كُلَّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ ۚ إِنَّ اللَّـهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٥١﴾

51. Ili Mwenyezi Mungu ailipe kila nafsi kwa yale iliyoyachuma. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.

هَـٰذَا بَلَاغٌ لِّلنَّاسِ وَلِيُنذَرُوا بِهِ وَلِيَعْلَمُوا أَنَّمَا هُوَ إِلَـٰهٌ وَاحِدٌ وَلِيَذَّكَّرَ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٥٢﴾

52. Hii (Qur'an) ni ujumbe wazi kwa watu iwaonye na wapate kujua kuwa hakika Yeye ni Mungu mmoja, na wapate kukumbuka wenye akili.

## WALIFANYA VITIMBI VYAO

**Aya 46 - 52**

### MAANA

Na kwa hakika wamekwishafanya vitimbi vyao na vitimbi vyao viko kwa Mwenyezi Mungu, ingawa vitimbi vyao vinaweza kuondosha mlima.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakutuma Mtume ila alifanyiwa vitimbi na kupangiwa njama na watu wafisadi na wapotevu, kuanzia enzi za Nabii Nuh mpaka kwa Muhammad **(s.a.w.w)**:

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَ يَاطِينَ الْإِنسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا ﴿١١٢﴾

Na kama hivyo tukamfanyia kila Nabii adui, mashetani watu na majini. Baadhi yao wanawapa wenzao maneno ya kupambapamba kuwahadaa." Juz.8 (6:112).

Sababu za uadui huo haziko tu baina ya kupingana imani na ulahidi na baina ya shirki na Tawhid, hapana, uadui huu ni matokeo ya maana ya kiujumla, ambayo ni uadui baina ya haki na batili kila mahali na kila wakati. Au kwa maneno ya kisasa ni uadui baina ya mapinduzi na kupinga mapinduzi.

Sababu yoyote ya vitimbi na njama itakavyokuwa na kwa namna yoyote itakavyokuwa na nguvu hata kuweza kusogeza mlima kutoka mahali pake, basi Mwenyezi Mungu anaijua na atawalipa wahusika wanayostahiki.

Kwa mnasaba huu tunadokeza kuwa wanaume wengi wanawasifu wanawake kuwa wana vitimbi na hadaa kwa kutoa ushaidi wa Aya isemayo:

﴿إِنَّ كَيْدَكُنَّ عَظِيمٌ ﴿٢٨﴾

Hakika vitimbi vyenu ni vikubwa Juz. 12 (12:28).

Wanawake nao wanaweza kuwajibu wanaume kuwa vitimbi vyao vinaondosha mlima na watoe ushahidi kwa Aya hii.

Zaidi ya hayo ni kwamba wasifu wa wanawake kuwa wana vitimbi umekuja katika Qura'n kupitia kwenye ulimi wa waziri, lakini wasifu wa wanaume kuwa wana vitimbi umekuja kutoka kwa Mwenyezi Mungu moja kwa moja.

Jambo la kushangaza ni kuwa badhi ya wanaume wanatoa dalili ya vitimbi vya wanawake kwa Aya hii inayowahusu wanume kwa kuweka dhamir ya wanawake (Hunna) mahali pa dhamiri ya wanaume (hum).

Basi usimdhanie Mwenyezi Mungu kuwa ni mwenye kuwavunjia ahadi yake mitume wake kwa kuinusuru haki na watu wake na kuidhalilisha batili na wasaidizi wake. Mwenyezi Mungu anaishiria ahadi yake kwa mitume kwa kusema:

﴿كَتَبَ اللَّـهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي ﴿٢١﴾

"Mwenyezi Mungu ameandika hakika Mimi na Mtume wangu tutashinda" (58:21).

Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kushinda, Mwenye kulipiza kisasi.

Anawalipizia kisasi wenye haki kwa wenye batili.

Siku itakapobadilishwa ardhi kuwa ardhi nyingine na mbingu (pia).

Hiyo ni kwa kugeuzwa ardhi kuwa vumbi kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

﴿فَكَانَتْ هَبَاءً مُّنبَثًّا ﴿٦﴾

Ikawa mavumbi yanayopeperushwa (56:6).

Ama nyota za mbinguni ni kuwa zitapukutika na kuanguka kama ilivyoelezwa katika Sura ya, 75, 71 na 82.

Nao watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu mmoja Mwenye nguvu mahali wazi hakuna mlango wala nguo, Miongoni mwa maelezo ya mahali watakapokusanyika na sifa zake ni kuwa ni uwanja mweupe ulio mtupu, hauna miti wala wala mabonde na milima, ardhi nyeupe kama fedha, haijamwagikiwa na damu, wala kufanywa makosa. Mbingu itakuwa kama shaba iliyoyeyuka, Jua, mwezi na nyota zitaondoka, na mlima itakuwa kama sufi.

### JAHNNAM NA SILAHA ZA MAANGAMIZI

Na utawaona wahalifu siku hiyo wamefungwa katika minyororo, Nguo zao zitakuwa za lami na moto utazigubika nyuso zao.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja picha kadhaa za watu wa motoni. Kuzisoma kunaleta kitisho katika nafsi na manywele na damu kusisimka, sikwambii huyo atakyeionja atakuwaje.

Miongoni mwa picha hizo ni kuwa wahalifu watafufuliwa wakiwa wamefungwa minyororo, kivazi ni cha aina inayoshika moto na kwenye nyuso zao mna kifuniko cha moto. Ama chakula chao kinatokana na mti wa zakkum na kinywaji chao ni usaha uliochanganyika na damu. Zaidi ya hayo watakuwa kwenye Jahannam ambayo haibakishi wala haisazi, inatupa cheche kama majumba na milima.

**Unaweza kuuliza**: kuwa aina hii ya adhabu haipingani na upole wa Mwenyezi Mungu na rehema yake? Kweli binadamu aliye dhaifu wa nyama na mifupa na damu anaweza kutosha kwenye adhabu hii?
Baadhi wamejibu swali hili kwamba: aina ya adhabu na picha zake alizozitaja Mwenyezi Mungu si za uhakika; isipokuwa alitaka kuwahofisha watu na makosa.
Mwenye majibu haya lau atairejea Qura'n tukufu atakuta kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) alikwishajua kwamba wengi katika waja wake watapitiwa na swali hili katika mawazo yao, hivyo akawajibu kimbele. Amebainsha hakiki hii katika Aya kadhaa; miongoni mwazo ni le aliyoitaja mara tu baada ya kutaja kifungo cha minyororo na kivazi cha lami, akasema moja kwa moja:

ili Mwnyezi Mungu ailipe kila nafsi kwa yale iliyoyachumma. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.

Nyingine ni hizi zifuatazo:

هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤٧﴾

"Kwani watalipwa isipokuwa yale waliyokuwa wakiyatenda?" Juz.7 (7:147).

وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٤٩﴾

"Nao hawatadhulumiwa hata kilicho kwenye uwazi wa kokwa ya tende." Juz. 5 (4:49).

وَأَنَّ اللَّـهَ لَيْسَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿١٨٢﴾

Na kwamba Mwenyezi Mungu si dhalimu kwa waja, Juz. 4 (3:182).

وَمَن جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦٠﴾

Na mwenye kufanya vibaya hatalipwa ila sawa na hivyo tu. Nao hawatadhulumiwa Juz, 8 (6:160).

وَالَّذِينَ كَسَبُوا السَّيِّئَاتِ جَزَاءُ سَيِّئَةٍ بِمِثْلِهَا ﴿٢٧﴾

"Na wale waliochuma maovu, malipo ya uovu ni mfano wake Juz, 11 (10:27).

فَمَنِ اعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ فَاعْتَدُوا عَلَيْهِ بِمِثْلِ مَا اعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ ﴿١٩٤﴾

Basi wanaowachokoza, pia nanyi wachokozeni kwa kadiri walivyowachokoza, Juz.2 (2:194).
Maana ya Aya hizi kwa ujumla ni kuwa uhalifu na maovu yako aina nyingi: kuna yale madogo na makubwa na kwamba yeye Mwenyezi Mungu ameliwekea kila kosa na adhabu yake kwa misingi ya haki na uadilifu bila ya kuzidisha; pengine kupunguza kulingana na hekima yake itakavyotaka. Kauli yake Mwenyezi Mungu "Hatalipwa isipokuwa mfano wake," inaliweka wazi hilo.
Naam! Kuna swali ambalo kila mwenye akili anapaswa kujiuliza, nalo ni nani basi anayestahiki adhabu hiyo kali kiasi hicho? Je, kuna kosa linalowajibisha aina yote hii ya mateso ambayo yana mwanzo lakini hayana mwisho? Kama alivyosema Mwenyezi Mungu: "Na wale ambao wamekufuru watakuwa katika moto wa Jahannam, hawatahukumiwa wapate kufa wala hawatapunguziwa adhabu yake" (35:36).

**Jibu**: ndio wako watu wanostahiki aina hiyo ya adhabu kali na zaidi ya hiyo. Miongoni mwao ni wale wanaoipiga vita haki au kuificha na huku wanajua; ni sawa haki hii iwe ni ya Mwenyezi Mungu au ya watu.

Na wenye hatia kubwa zaidi katika watu ni wafanya biashara wa vita ambao wanandaa kumwaga damu na kuharibu maisha kwa silaha za maangamizi; kama vile mabomu ya atomiki, haidrojeni na silaha za sumu ambazo zinaua mamia, bali hata mamilioni katika dakika chache.

Adhabu yoyote watakayopewa wauaji hawa haiwatoshi, Minyororo na nguo za moto si chochote kulinganisha na kuvunja miji, kuwafukuza watu kwenye miji yao na kuwaua kwa maelfu.

Kisha Je, cheche za moto wa Jahannam ni mbaya zaidi kuliko bomu la atomic lililotupwa Hiroshima? Na inajulikana hivi sasa mabomu wanayomiliki wauaji, ni mara elfu zaidi kulinganisha na hayo ya Hiroshima.

Je, chakula cha Zakkum na maji ya usaha uliochanganyika na damu unamaliza watu kuliko silaha za sumu wanazozitumia maadui wa Mwenyezi Mungu hivi sasa huko Vietnam na kabla yake Korea?

Yametangulia maelezo katika kufasiri Aya ya 8, ya Sura hii kwamba kuna silaha ambazo mtu ikimgusa chembe tu, basi viungo vyake vinanywea, macho yanamtoka na kufa hapo hapo.

Baada ya yote haya, mwenye akili anaweza kuwa na shaka kwamba kuwahurumia wanaomiliki silaha hizi ni dhulma na dhambi? Na kwamba wao lau wataadhibiwa na adhabu kali zaidi ya Jahannam ingelikuwa adhabu yao ni haki na uadilifu?

Je, adhabu yoyote itaonekana ni zaidi kwa yule ambaye ana kiu cha damu ya maelfu wala hashibi isipokuwa kwa kunyonya chakula cha wanyonge na kuiba mali zao?

Lau kusingelikuwa na dalili yoyote ya kufufuliwa watu isipokuwa kupatikana madhalimu hawa, ingelitosha; kwamba lau dunia ingelikuwa ndio kila kitu na kusiweko ulimwengu mwingine ambao haki itarudishiwa wenyewe na apate kila dhalimu stahiki yake, basi ingelikuwa mauti ni bora kuliko uhai na dhulma ni bora kuliko uadilifu.

Hii ni ujumbe wazi kwa watu iwaonye na wapate kujua kuwa hakika Yeye ni Mungu mmoja na wapate kukumbuka wenye akili.

Hii ni ishara ya Qur’an na yaliyomo ndani yake miongoni mwa makemeo na ahadi. Makusudio ya ujumbe wazi ni kutosheleza. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameteremsha Qur’an kwa nabii wake ikiwa ni tosha na yenye kutekekeleza kila mahitaji ya watu katika mambo ya dini yao na dunia yao. Vile vile inawafundisha ummoja wa Mungu na uadilifu wake na kuwaonya wasihalifu amri Yake na makatazo Yake.

## SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

## MWISHO WA JUZUU YA KUMI NA TATU

## YALIYOMO


**1 TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
IMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYA 1
1 ................. IMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA
1 ........ IMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED
1 IMEPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU
1 ................................. UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI
2 ............................................... MAKOSA YA CHAPA
**3 TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
3 ..............................................................NAFSI
4 .....................................YUSUF NI MUHESHIMIWA MISR
4 ............................................................... MAANA
6 ..........................................WAKAJA NDUGUZE YUSUF
6 ............................................................... MAANA
7 ..............................MTUME NDUGU YETU PAMOJA NASI
8 ............................................................... MAANA
9 ......................................... MSIINGIE MLANGO MMOJA
9 ............................................................... MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
**11** ............................................................................
11 .............................. MIMI NI NDUGUYO, USIHUZUNIKE
14 .........KAMA AMEIBA BASI NDUGUYE PIA ALIIBA ZAMANI
14 ............................................................ MAANA
17 ........................HATUTOI USHAHIDI ILA TUNAYOYAJUA
17 ............................................................ MAANA
HAKUNA KUNGOJA MEMA YAJE YENYEWE WALA MABAYA
18 ...................................................................
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
**20** ............................................................................
20 ...................................................MIMI NI YUSUF
20 ............................................................ MAANA
22 ................................... NASIKIA HARUFU YA YUSUFU
22 ............................................................ MAANA
24 ..................................KUKUTANA YUSUF NA YA'QUB
24 ............................................................ MAANA
27 .......................JE, KISA CHA YUSUF NI CHA MAPENZI?

**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU** ........................................ **30**
NA WATU WENGI SI WENYE KUAMINI AYA .................... 30
MAANA ........................................ 30
SEMA HII NI NJIA YANGU ........................................ 32
MAANA ........................................ 32
MWISHO WA SURA YA KUMI NA MBILI ........................ 34
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU** ........................................ **35**
HIZO NI AYA ZA KITAB ........................................ 35
MAANA ........................................ 35
AMEINUA MBINGU BILA YA NGUZO ............................ 36
MAANA ........................................ 36
SAYYID AFGHANI NA WANAOMKANA MUNGU ............. 39
KWELI TUTAKUA KATIKA UMBO JIPYA? ........................ 40
MAANA ........................................ 40
WANAOAMINI MAADA NA MAISHA BAADA YA MAUTI ... 41
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU** ........................................ **44**
MWENYEZI MUNGU ALIJUA ........................................ 44
MAANA ........................................ 44
HABADILISHI MPAKA WAJIBADILISHE ....................... 46
ANAYEWAONYESHA UMEME ........................................ 47
MAANA ........................................ 47
KIPOFU NA MWENYE KUONA ........................................ 49
MAANA ........................................ 49
AKILI ZA WATU HAZIWATOSHELEZI ......................... 50
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU** ........................................ **52**
POVU HALIDUMU ........................................ 52
MAANA ........................................ 52
YALIYOTEREMSHWA KUTOKA KWA MOLA WAKO NI HAKI 54
MAANA ........................................ 54
HUKUNJUA RIZIKI ........................................ 57
MTU NA RIZIKI ........................................ 57
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU** ........................................ **59**

59 ................................... TUMEKUTUMA KATIKA UMMA
59 .............................................................. MAANA
59 ..........................................FIKRA YA MATAGHUTI
62 ................................MITUME WALIFANYIWA STIHZAI
62 ........................................................... MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
**64** ...................................................................
64 ..............................................MFANO WA BUSTANI
64 ........................................................... MAANA
65 ................................ SHIA IMAMIYA NA SWAHABA
MWENYEZI MUNGU HUFUTA NA HUTHIBITISHA AYATAKAYO 68
68 ........................................................... MAANA
69 ............................. RAHA YA DHAMIRI NA MAWAZO
70 ....................... MWISHO WA SURA YA KUMI NA TATU
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
**71** ...................................................................
71 .......................................................DINI NI NURU
71 ........................................................... MAANA
74 ................................................ TULIMTUMA MUSA
74 ........................................................... MAANA
76 .....................................JE HAZIKUWAFIKIA HABARI
76 ........................................................... MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
**79** ...................................................................
79 ............................ TUTAKUTOA KWENYE ARDHI YETU
79 ........................................................... MAANA
80 ..................................................HAKI MBADALA
81 ...............................MATENDO YAO NI KAMA MAJIVU
81 ........................................................... MAANA
83 ..................................DHALIMU NA MDHULUMIWA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
**85** ...................................................................
85 ................................... MIADI YA MWENYEZI MUNGU
85 ............................................HOTUBA YA SHETANI
88 ........................................NENO JEMA NA NENO OVU
88 ........................................................... MAANA

91 ……… WALIBADILISHA NEEMA YA MUNGU KWA KUFURU
91 …………………………………………………… MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
**93** ………………………………………………………………
93 ………………NA AKATEREMSHA MAJI KUTOKA MBINGUNI
93 …………………………………………………… MAANA
93 …………………… JE MTU ANA MAUMBILE YA HATIA?
95 ……EWE MOLA WANGU UJAALIE MJI HUU UWE WA AMANI
95 …………………………… MITUME NA KUITIKIWA DUA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TATU**
**99** ………………………………………………………………
99 ……………DHALIMU ANAJISAHAU LAKINI HASAHAULIWI
99 …………………………………………………… MAANA
101 ……………………………… WALIFANYA VITIMBI VYAO
101 …………………………………………………… MAANA
102 ………………… JAHNNAM NA SILAHA ZA MAANGAMIZI
104 ……………………………………SHARTI YA KUCHAPA
104 …………………MWISHO WA JUZUU YA KUMI NA TATU
105 …………………………………………………YALIYOMO